SUPA JACKPOT
TZS.1,037,361,877
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MAWAKILI** binafsi watajwa kuchangia migogoro ya ardhi




UKURASA 13

Ijumaa Oktoba 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581091

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# TISHIO AFYA AKILI

**TAKWIMU** mpya zashtua, wagonjwa 30 hadi 70 wapokewa kila siku Mirembe... *Endelea ukurasa 2*



UKURASA WA 4

## SHEHENA MAGENDO YA SUKARI, MAFUTA YAYEYUKA

SHEHENA ya magendo ya sukari na mafuta ya kula, iliyokuwa imeingizwa katika bandari bubu ya Kasera, jijini Tanga kwa ajili ya kusambazwa nchini, imetoroshwa na watu wasiojulikana katika mazingira ya kutatanisha...

UKURASA WA 4

## WATUHUMIWA WA 'PANYA ROAD' WAFIKISHWA KORTINI



WATUHUMIWA 40 wanaokabiliwa na kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kuvunja nyumba usiku, maarufu kama 'panya road' wamefikishwa katika Mahakama...

UKURASA WA 5

## RC: WANAWAKE WANAOPIGWA WAJE KWANGU

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amewataka wanawake wanaopigwa na waume zao kwenda kushtaki ofisini kwake ili wachukuliwe hatua. Aidha, amesema ni marufuku kwa mwanaume kumpiga mwanamke mkoani humo na watakaofanya...



Rais Samia Suluhu Hassan, akishuhudia Rais wa Chemba ya Biashara ya Tanzania, Paul Koyi (wa pili kushoto), akibadilishana hati na Makamu Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara ya Qatar, Muhammed bin Ahmed Al Kuwari, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano, jijini Doha, Qatar jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC), Ali Suleiman Amour. **PICHA: IKULU**

## Tume yapendekeza kodi vileo zisaidie wananchi bima ya afya

UKURASA 2

## Adai kukiri kuua kuogopa kuingizwa spoku sehemu za siri

UKURASA 3

**MICHEZO** MAYELE, AZIZ KI WAONGEZEWA DOZI UK. 32

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Rais mstaafu Jakaya Kikwete, akipata maelezo ya miradi ya Kwala Satellite City kwa Mwenyekiti wa Kampuni ya Sino Tan, Jensen Huang, katika maonyesho ya tatu ya viwanda, biashara na uwekezaji, mjini Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TISHIO AFYA YA AKILI

## •Wagonjwa 30 -70 hupokewa Mirembe kila siku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, imesema inapokea wagonjwa kati ya 30 hadi 70 kwa siku wanaofika kupatiwa matibabu ya afya ya akili.

Ofisa Ustawi wa Hospitali hiyo, Anewa Sewani, alitoa takwimu hizo katika mkutano wa uongozi wa hospitali na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili ambayo hufanyika kila mwaka Oktoba 10.

Alisema kati ya idadi hiyo inayopokelewa kupitia kitengo cha wagonjwa wa nje, wagonjwa wenye dalili za kuhitaji kulazwa ili kupata matibabu zaidi ni wastani wa watu tisa hadi 15 kwa siku.

“Kitengo cha wagonjwa wa nje wanapokea idadi ya watu 150 hadi 250 kati yao 30 hadi 70 wanakuja kwa ajili ya matibabu ya afya ya akili kwa siku, wengine waliobaki ni wa magonjwa ya kimwili,” alisema.

Kwa upande wake, Daktari wa Afya ya akili, Dk. Veronica Lyimo, alisema wanapokea wagonjwa wenye matatizo mbalimbali ya afya ya akili huku akiainisha maeneo matatu makubwa ambayo ni wa kibailojia, kisaikolojia na kijamii.

Alisema kwenye kibailojia wengine wanapata ugonjwa wa afya ya akili kwa kurithi na mwingine kutokana na magonjwa ya ndani.

“Kwenye kijamii mtu kutokuwa na uwezo mzuri kiuchumi, kuzungukwa na makundi ambayo sio rafiki, hiyo hali inasababisha ubongo kushindwa kufanya kazi vizuri, unapokuwa mtu mwenye mawazo, msongo na matumizi ya pombe sana au madawa ya kulevya yanachangia hali hiyo,” alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, alisema kwa sasa kwenye jamii kuna wingi wa matukio ya kutisha ambayo yanachangiwa na tatizo la afya ya akili.

“Kwa sasa haipiti wiki moja hujasikia tukio limetokea kwenye familia au jamii fulani, ni matukio ambayo kwa siku za nyuma tulikuwa hatujayazoea sana na ni sehemu moja wapo ya tatizo la afya ya akili,” alisema.

Alisema katika kuelekea siku ya afya ya akili Oktoba 10, mwaka huu, hospitali hiyo inatoa wito kwa wananchi kufika kupata huduma zitakazotolewa bila malipo.

“Kuanzia kesho (leo) hadi Oktoba 10 huduma zitatolewa bure, tutatoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya akili na huduma zingine ikiwamo za kisaikolojia,” alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na idadi ya wagonjwa wanaopokewa, hospitali inahitaji uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu na wataalamu ambao kwa sasa bingwa wa afya ya akili ni wanne pekee.

Alisema hospitali kwa sasa ina wagonjwa waliolazwa 400, na waliokuja kupata tiba kupitia mfumo wa kisheria 250.

“Tuna waraibu wa madawa ya kulevya 500 kule Isanga na wagonjwa 250 tunawaona kama wagonjwa wa huduma za nje,” alisema.

### SABABU MAGONJWA YA AKILI

Kwa mujibu wa Ripoti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Kituo cha Afya, magonjwa ya akili ni matatizo ya ubongo ambayo humfanya mtu kuwa na hisia, fikira na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii na kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha.

Magonjwa ya akili yanaweza kusababishwa na sababu za kibaiolojia au kisaikolojia.

### SABABU ZA KIBIOLOJIA

Ilitaja sababu za kurithi na vinasaba kutoka kwa wazazi, magonjwa ya muda mrefu kama degedege, malaria kali, ugonjwa wa UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya.

### SABABU ZA KISAIKOLOJIA

Aidha, ripoti hiyo imeeleza kuwa majanga, ubakaji, uvamizi, ajali, utekaji nyara, kukosa elimu, kukosa ajira ni visababishi vya tatizo la afya ya akili kisaikolojia.

Vile vile, kufiwa, kutengana, talaka, ugoni, kufungwa, kufukuzwa kazi, kukosa mishahara na kustaafu kazi.

Visababishi vingine ni kutokufanya vizuri kwenye masomo na kufukuzwa chuo/shule ni matatizo yanayowaathiri watoto.

### DALILI ZA KIAKILI

Kukosa umakini wa shughuli za kila siku, kusahau kwa haraka au kupoteza kumbukumbu, kukosa uwezo wa kupambanua mambo kwa mitazamo tofauti, kutokujali, kuwa na imani zisizo za kawaida kama vile; kuwa mtu maarufu au nabii.

Kadhalika, kupokea taarifa kutoka kwenye redio au mitandao ya simu, imani ya kuwasiliana na watu maarufu, kuamini kuwa na nguvu ya ziada kutoka nje ya mwili, imani kuwa kuna watu wanakufuatilia, kutaka kumdhuru na kuwa na mawazo yasiyokuwa na mtiririko unaoeleweka.

# CSSC yapendekeza kodi za vileo zisaidie wananchi bima ya afya

**Na Gwamaka Alipipi**

TUME ya Kikristo ya Huduma ya Afya (CSSC), imependekeza makato ya kodi yatokanayo na bidhaa za vileo, sigara yaelekezwe katika kuwasaidia wananchi kupata huduma ya bima ya afya kwa wote.

Imesema inaunga mkono serikali kuja na wazo la kuanzisha bima ya afya kwa wote na wapo tayari kutoa ushirikiano wa kuboresha huduma hiyo kupitia hospitali zinazomilikiwa na taasisi za dini.

Mratibu wa Uboreshaji Huduma wa CSSC, Dk. David Isaya, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni maandalizi ya kuelekea mkutano mkuu wa masuala ya afya utakaowakutanisha wataalamu wa afya zaidi ya 600 mkoani Dar es Salaam.

Mkutano huo utaanza Oktoba 11 hadi 13, mwaka huu na utakuwa na kaulimbiu ‘Uimarishwaji wa huduma za afya’, viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi binafsi ambao ni wadau wa sekta ya afya wanatarajiwa kuhudhuria.

Dk. Isaya alisema kila Mtanzania ana wajibu wa kupata bima ya afya, kwa ambao hawana uwezo serikali inapaswa kuchukua jukumu la kuwasaidia.

“Wananchi wengi wanaishi vijijini, kitu pekee kitakachowakomboa ni kupata bima ya afya. Ili kila Mtanzania apate bima ya afya serikali inapaswa kuelekeza mapato yatokanayo na kodi za vilevi na sigara kwenye kuwasaidia Watanzania ambao hawatakuwa na uwezo wa kupata bima ya afya.

“Kwenye mkutano wa mwaka huu tutajikita zaidi katika namna ya kuongeza ufanisi, utoaji wa huduma kwa hospitali zinazomilikiwa na taasisi za dini,” alisema Dk. Isaya.

“Hospitali zinazomilikiwa na taasisi za dini zimekuwa na mchango mkubwa katika kutoa huduma za afya hapa nchini, Hivyo serikali ina wajibu wa kuzikwamua hospitali za umma kutoka katika tatizo la utoaji wa huduma za afya bora, pamoja na kuboresha miundombinu na vitendea kazi.”

Mratibu wa Huduma za Ubora, Idara ya Afya, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Pius Kagoma, alisema serikali imejielekeza uboreshaji, utoaji wa takwimu katika vituo vya utoaji wa huduma za afya.

Alisema bima ya afya kwa wote itakapopitishwa TAMISEMI itahakikisha huduma za afya zinaboreshwa ili kila mtu aweze kuhudumiwa.

Alisema serikali imejiwekea mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa hospitali za umma kupitia takwimu hususani kwa hospitali zilizoko vijijini.

HABARI KITAIFA

# Mshtakiwa adai kukiri kuua kwa kuogopa kuingizwa spoku

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Hemed Ally ameieleza Mahakama kuwa alikiri kumuua Farihani Maluni na kumfukia mbele ya nyumba iliyopo Sharif Shamba, Ilala baada ya kuogopa kuingizwa spoku ya baiskeli na askari wa kike kwenye uume wake.

Ally alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aloyce Minde wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati akitoa utetezi wake katika kesi ya mauaji inayomkabili, anayotuhumiwa kumuua Maluni, Juni 12, 2014.

Alidai kuwa, Februari 9, 2022 majira ya asubuhi akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi cha Msimbazi, alikwenda afande Apolinary na askari wengine watatu, mmoja kati yao alikuwa wakike.

Alidai walifungua mlango wakamueleza kuwa maelezo aliyoyatoa Februari 8, 2015 mbele ya wakili wake, Juma Mtatiro, hawayataki na kudai wanataka maelezo wanayoyataka wao.

Mshtakiwa huyo akiongozwa na wakili wake, Caroline Kigembe, alidai kama wanataka atoe maelezo upya basi wampigie wakili wake, lakini hawakumpigia na wakamueleza akiri kitu ambacho yeye hakifahamu.

Ally alidai askari wa kike alimshika sehemu zake za siri za mbele, huku mkono wake mwingine ukiwa umeshika spoki ya baiskeli, ikabidi amuulize vipi spoku na sehemu zake za siri? Akamjibu kwani yeye hataki kumuingilia mwanamke?

"Kwa sababu nilimuona mtu mmoja akiwa mahabusu ana vuja damu sehemu zake za siri, nilihofia kuwa na mimi nitakuwa kama yule, niliwaambia nitaandika kama wanavyotaka wao kuliko kuingiziwa spoki," alidai Ally.

Alidai kwa wakati huo tayari walishaandika maelezo yao na afande Apolinary (marehemu) alikuwa nayo mfukoni, na kwamba alisaini maelezo hayo na baada ya hapo walimrudisha mahabusu na kumfungia milango wakaondoka.

Baada ya nusu saa, Ally alidai alikwenda afande Chenga, Apolinary pamoja na askari wengine wasiofahamu wakamfunga kitambaa usoni wakamuweka ndani ya gari, walipomfungua kitambaa alijikuta kwenye nyumba ambayo alishapanga huko Ilala Sharif Shamba, Dar es Salaam.

Alidai kuwa hakujua chochote na hakuambiwa jambo lolote akafungiwa kwenye chumba kimoja na ilipofika majira ya saa 10 au 11 jioni wakamtoa ndani wakamrudisha kwenye gari.

Pia, kuhusu mapazia 23 yaliyotolewa mahakamani hapo kama kielelezo, alidai hayo sio muhimu na kwamba yametengenezwa maalum kwa ajili yake ikiwezekana mahakama imrudishie mwenyewe kwa sababu yalipokutwa yeye haishi huko.

Ally alidai kuwa swali la kujiuliza ni kwamba hayo mabaki yaliyokutwa kwenye nyumba ambayo alishawahi kuwa mpangaji, je! Ni kweli ni ya Farihani? Jibu ni kwamba sio kweli kutokana na ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mshtakiwa alitoa swali hilo, kwa sababu Mkemia Mwandamizi kutoka ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kaijunga Brassy, wakati anatoa ushahidi kwenye kesi hiyo alidai mabaki ya marehemu Farihani ikiwamo mifupa haikuonesha majibu ya vinasaba (DNA).

Mshtakiwa huyo aliomba mahakama imuachie huru kwa sababu yupo gerezani miaka minane na pia yeye sio muuaji wala hakuwahi kuua na anaomba Mungu amuepushe kwa hilo, anaomba mahakama imuachie huru.

Wakati akijibu swali la Wakili wa Serikali, Aziza Mhina, Ally alidai kuwa Julai 12, 2014 ilimkuta akiwa mahabusu, tarehe anayotuhumiwa kuwa alimuua Maluni.

Ilidaiwa Juni 12, 2014 mshtakiwa Hemed Ally eneo la Sharif Shamba anatuhumiwa kumuua Farihani Maluni.

# Mawakili binafsi watajwa kuchangia migogoro ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema baadhi ya mawakili wa kujitegemea wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi na kushiriki kukwamisha mashauri kwenye mabaraza ya ardhi na mahakamani.

Amesema Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa kinara cha mashauri ambayo mawakili wamefanya mabaraza kama kichaka cha kupotezea muda kwa wakopaji walioshindwa kulipa mikopo.

Mabula aliyasema hayo jana jijini hapo katika kikao kazi cha kuboresha utoaji wa huduma katika mabaraza ya ardhi ya wilaya na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS).

Dk. Mabula alisema baadhi ya mawakili wa kujitegemea wamejikita katika maeneo yenye kero kubwa ya ardhi na wakati mwingine wao wanakuwa ni chachu ya matatizo hayo.

"Kupitia kamati ya uchunguzi iliyoundwa kuchunguza migogoro ya ardhi Kata ya Mapinga Wilaya Bagamoyo waliolalamikiwa na kutajwa mara nyingi kuwa wanahusika na uanzishaji wa migogoro ya ardhi katika Kata ya Mapinga baadhi ya mawakili wamekuwa wakitajwa kama sehemu ya wavamizi," alisema.

Waziri aliuomba uongozi wa TLS kuwachukulia hatua pindi wanapobainika kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali.

"Mfano mzuri ni katika Kata ya Mapinga Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Kamati hiyo imebaini kuwa sehemu kubwa ya wavamizi wa eneo la Mapinga (Bagamoyo mkoani Pwani) wananchi humtumia wakili mmoja kuvamia eneo," alisema.

"Kisha wakili wao anafungua kesi mahakamani, hivyo kuwafanya wamiliki wasipate fursa ya kuingia katika maeneo yao kwa kisingizio cha kesi ipo mahakamani, huku wao wakiendelea kuuza maeneo waliyovamia. Yupo wakili anayejulikana kwa (jina limehifadhiwa) ambaye ametajwa kuhusika katika kesi zote za uvamizi," alisema Mabula.

Alitaja mbinu mojawapo anayoitumia wakili huyo ni kutumia nyaraka za wamiliki wenye haki kujua muda waliopata maeneo yao kisha kuwashauri wavamizi kuandaa nyaraka za kughushi kwa kurudisha tarehe nyuma na kuwasilisha nyaraka hizo mahakamani zinazoonyesha walitangulia kupata maeneo hayo kabla ya wenye haki.


Lodhia group of companies

## LODHIA STEEL INDUSTRIES LIMITED

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

**NAFASI-HSE NA ASST HSE**

KAMPUNI-LODHIA GROUP OF COMPANIES.
KITUO CHA KAZI- KISEMVULE,MKURANGA PWANI
MSHAHARA: UTATOLEWA KWA MAJADILIANO.

- **Sifa**
  1. Shahada ya Kwanza katika HSE au fani inayohusiana na uzoefu wa miaka mitatu hadi minne.
  2. Kiongozi wa timu na ujuzi bora wa mawasiliano na nyaraka
  3. Awe na cheti cha mafunzo ya OSHA
  4. Anapaswa kuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi wa usalama kwa kujitegemea.
- **Maafisa wa Afya, usalama na mazingira (HSE) na ASST HSE wana majukumu mengi, ambayo yatajumuisha haya:**
  a. Kuhakikisha wafanyakazi wamefunzwa juu ya usalama na wanafahamu hatari katika mazingira yao ya kazi.
  b. Kufanya ukaguzi wa maeneo ya kazi ili kuhakikisha wanafuata kanuni za usalama.
  c. Uchunguzi wa ajali na kuripoti na kuchukua hatua za kuzuia kutokea tena.
  d. Kushauriana na wasimamizi ili kuunda sera na taratibu za programu za usalama
  e. Kutayarisha ripoti kuhusu hali ya usalama katika mitambo yake mbalimbali.
  f. Kufuatilia na kufuata sheria za usalama mara kwa mara
  g. Utunzaji wa Rekodi zinazohitajika za majeraha au magonjwa yanayotokea kazini na kutambua hatari zinazoweza kutokea au mifumo ya mienendo isiyo salama.
  h. Mpango wa usimamizi wa mazingira na mradi wa utekelezaji.
  i. Kushiriki habari, mapendekezo, na uchunguzi kwa kushirikiana na wakuu wa idara kila wiki.
  j. Uongozi wa kuunda uthabiti katika viwango vya usalama ndani ya kampuni.
  k. Anapaswa kuwa mtu mwenye nguvu na mtazamo wa kuleta viwango vya usalama vinavyohitajika.

**NAFASI-MUANDAAJI WA MISHAHARA YA WAFANYAKAZI**

KAMPUNI-LODHIA GROUP OF COMPANIES.
KITUO CHA KAZI- KISEMVULE,MKURANGA PWANI
MSHAHARA: UTATOLEWA KWA MAJADILIANO.

- **Sifa**
  1. Diploma/Shahada ya Kwanza katika Uhasibu/benki katika fani inayohusiana na uzoefu usiopungua miaka miwili hadi minne.
  2. Ujuzi bora wa mawasiliano, vipimo, na uwekaji kumbukumbu
- **Karani wa mishahara ana majukumu mengi, sambamba na yaliyoainishwa hapa chini:-**
  a. Kuzingatia maelezo, ustadi wa uchanganuzi na uwezo wa kuchakata data haraka ili kudhibiti wafanyikazi kulipa hundi kwa usahihi kila mwezi.
  b. Uelewa mkubwa wa kifedha na uwezo bora wa mawasiliano ya maneno
  c. Ujuzi wa vitendo na sheria zinazohusiana na uandaaji wa Mishahara
  d. Kusanya kumbukumbu za mahudhurio za kila siku, za wiki au za kila mwezi
  e. Kujibu maswali ya wafanyakazi kwa uvumilivu na utulivu.
  f. Suluhisha hitilafu zozote zinazohusiana na masuala ya malipo.
  g. Majukumu mengine yoyote atakayopewa na Mkuu wa Idara.

**Maombi yatumwe kwa barua pepe: hr@lodhiagroup.co.tz**
**Sanduku la posta: Lodhia Steel Industries, S.L.P 75778**
**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15/10/2022, wenye sifa wataitwa kwa usahili.**

**POSITION-MECHANICAL ENGINEER.**

LODHIA GROUP OF COMPANIES.
**Qualifications and responsibilities**

a. Bachelor degree in Mechanical Engineering (with 3-5 years of experience).
b. Excellent communication, specification, and documentation skills
c. Must have worked in manufacturing industry
d. Advantage if worked in steel industry/plant
e. Must have experience worked into shift
f. AutoCAD knowledge advantage.
g. Must have knowledge in making sketch drawing for any machine part
h. Must have experience working on ground level in production line
i. Must be able to make maintenance report and preventive maintenance schedule.

**POSITION-ELECTRICAL ENGINEER.**

**LODHIA GROUP OF COMPANIES.**
Qualifications and responsibilities.

a. Bachelor degree in electrical engineering/electrical and electronics (with 3-5 years of experience.
b. Must have worked in manufacturing industry
c. Advantage if worked in steel industry/plant
d. Must have experience worked into shift
e. Autocad knowledge advanced
f. Must have knowledge on PLC.
g. Must have experience in fault finding and going online to manufacture for problems solving.
h. Must have ground level working experience.
i. Ac and Dc motors knowledge.
j. Must have knowledge of general wiring of machine and electrical panel.

**Maombi yatumwe kwa barua pepe: hr@lodhiagroup.co.tz**
**Sanduku la posta: Lodhia Steel Industries, S.L.P 75778**
**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15/10/2022, wenye sifa wataitwa kwa usahili.**

217081002

# Shehena magendo ya sukari, mafuta yayeyuka

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SHEHENA ya magendo ya sukari na mafuta ya kula, iliyokuwa imeingizwa katika bandari bubu ya Kasera, jijini Tanga kwa ajili ya kusambazwa nchini, imetoroshwa na watu wasiojulikana katika mazingira ya kutatanisha.

Bidhaa hizo zinaelezwa kutoroshwa muda fupi baada ya kufika bandarini hapo, huku majahazi yaliyobeba mzigo huo yakitelekezwa.

Taarifa ambazo Nipashe imezipata jana kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, ni kwamba alipokea taarifa hiyo kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama.

"Nimeambiwa kwamba mzigo huo, ulishukiwa kuwa ni wa magendo Oktoba 2, mwaka huu, lakini baadaye alipata tena taarifa ya kutoweka kwa mzigo huo," alisema.

Kutokana na ukakasi wa taarifa hiyo, Mgumba alikwenda Kasera na kufanya ukaguzi wa kushtukiza.

"Nimepata taarifa kwa viongozi wangu, kwamba kuna mzigo mkubwa wa shehena ya mafuta na sukari vinaingia katika mkoa wetu. Sasa nmekuja kuangalia lakini kwa bahati mbaya sana, tumekuta mzigo umeshashushwa umeondolewa na wale waliokuwa na mzigo nao wameshaondoka," alisema.

Hata hivyo, Mgumba hakuweka wazi ni bidhaa kiasi gani cha mafuta ya chakula na sukari vilivyotoroshwa.

"Nimewaelekeza walinzi wetu wanaolinda maeneo hayo kuongeza umakini katika kazi zao, lakini nimetaka nipate sababu ya wale waliokuwa lindo usiku wa tukio waeleze kwanini mzigo huo umetoroshwa," alisisitiza Mkuu huyo wa Mkoa.

**TRA YACHUKUA HATUA**

Kutokana na mzigo uliotoroshwa katika bandari bubu ya Kasera, Meneja wa TRA, Mkoa wa Tanga, Specioza Owure, alisema hatua walizochukua mpaka sasa ni kulishikilia boti iliyotumika kubebea mzigo hadi pale mwenyewe atakapokwenda kuifuata.

Aidha, alisema pia hatua nyingine walizochukua ni kuimarisha kwanza doria katika maeneo yote ya bandarini na mipakani.

"Hili limetokea kwa sababu wafanyabiashara baadhi yao si wazalendo na hawafuatu taratibu za usafirishaji kwa kulipa kodi ili kusafirisha mizigo yao kihalali.

"Wasafirishaji waache ujanja ujanja, wafuate sheria na taratibu za kuingiza mizigo nchini. Lakini tunachokifanya sasa ni kuimarisha doria zetu pamoja na kuhakikisha taarifa zinazotufikia hazina utata."



Chifu mpya wa kabila la Wanyakyusa, Edwin Bantemanile Mwakatumbula, akionyesha kwa kugusa sehemu ya chemchemu inaytoa maji ya moto, katika kijiji cha Masoko, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watuhumiwa wa 'Panya Road' wafikishwa kortini

**Na Romana Mallya**

WATUHUMIWA 40 wanaokabiliwa na kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kuvunja nyumba usiku, maarufu kama 'panya road' wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Kinyerezi jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Dawati la Habari la Jeshi la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam jana, ilieleza kuwa watuhumiwa hao walifikishwa mahakamani juzi na kusomewa mashtaka yanayowakabili.

"Mahakama ya Wilaya ya Ilala imemsomea mashtaka Laben Manzi, maarufu kama Master, pamoja wenzake 39 waliofikishwa mbele ya mahakimu wakazi watatu, Glory Nkwera, Fadhili Luvinda na Rehema Liana, wakikabiliwa na mashtaka ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kuvunja nyumba usiku na kujeruhi watu maeneo mbalimbali wilayani Ilala," ilisema taarifa hiyo.

Mawakili wa Serikali, Michael Momboko, Magdalena Kisoka, Aziza Mhina walidai mahakamani hapo kuwa watuhumiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Septemba 19 na 21, mwaka huu, maeneo mbalimbali wilayani humo.

Walidai watuhumiwa hao walivunja nyumba usiku na kupora mali baada ya kujeruhi wananchi kwa kutumia silaha za jadi ambazo ni panga, nondo, visu na kukimbia.

Hata hivyo, watuhumiwa hao walikana mashtaka hayo na kurudishwa rumande kutokana na mashtaka wanayokabiliwa nayo kutokuwa na dhamana.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 19, mwaka huu upelelezi wa shauri hilo utakapokamilika.

Kikundi cha 'panya road' kiliibuka Aprili, mwaka huu, na kufanya matukio katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam yakiwamo Chanika, Kitunda, Tabata, Mbezi, Kinyerezi, Kawe na Kunduchi na katika baadhi ya maeneo hayo, waliwajeruhi wananchi na kuua.

Septemba 15, mwaka huu, wabunge waliitaka serikali ichukue hatua madhubuti kuyadhibiti matukio hayo kwa kuwa yanatishia maisha na usalama wa raia na mali zao.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliiagiza serikali kushughulikia jambo hilo kwa haraka.

# JK asisitiza mazingira rafiki uwekezaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS Mstaafu, Jakaya Kikwete, amesema ili kufikia kwenye uchumi imara ni lazima kuwapo na mazingira rafiki ya uwekezaji.

Pia, ameupongeza mkoa wa Pwani kuwa ndiyo sehemu sahihi ya kuwekeza viwanda kutokana na kuwa na maeneo mengi ya uwekezaji, kulinganisha na Mkoa wa Dar es Salaam ambao umejaa.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua Wiki ya Maonyesho ya Tatu ya Uwekezaji na Biashara mkoani Pwani.

Pamoja na mambo mengine, Kikwete aliishauri serikali kutogawa ardhi yote kwa wawekezaji na kuwasahau wananchi wakiwemo maskini.

Alisema mbali na serikali kuwa na mpango mzuri wa kupima ardhi kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji, kuna haja ya kupima viwanja na kuwauzia wananchi maskini badala ya kujikita kwa matajiri pekee.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema mkoa wa Pwani unaongoza kwa wingi wa idadi nyingi ya viwanda na kwamba kwa sasa una viwanda 1,460, kati ya hivyo 90 ni vikubwa.

Alisema mkoa una zaidi ya vivutio vya utalii 70, huku akiwataka wawekezaji kufika mkoani humo kuwekeza badala ya kwenda maeneo mengine.

Alisema uwapo wa viwanda hivyo umepunguza tatizo la ajira kwa vijana waliokuwa wakitaabika mtaani, huku akiwataka wamiliki wa viwanda hivyo kufanya malipo yao ndani ya mkoa ili kusaidia ongezeko la mapato yatakayosaidia kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ya wananchi wa mkoa wa Pwani.

Kunenge alisema mkoa huo umejipanga kutekeleza sera ya serikali ya uwekezaji kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wengine.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Prof. Sylvester Mpanduji, alisema shirika hilo limefanikiwa kuwakutanisha wajasiriamali wa ukanda wa Pwani, kubadilishana uzoefu na sekta mbalimbali kwa lengo la kuwainua wananchi wa chini.

Prof. Mpanduji alisema huduma za SIDO zimeongeza ari ya wananchi kuanzisha viwanda kwenye maeneo yao na kwamba zaidi ya viwanda vidogo 247 vimeanzishwa nchini.

Alisema shirika hilo limeomba kuendelea kuwezeshwa na serikali ili liweze kutimiza ndoto zake kwa lengo la kufikia azma ya serikali kuwa na nchi ya viwanda.

# RC: Wanawake wanaopigwa waje kwangu

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amewataka wanawake wanaopigwa na waume zao kwenda kushtaki ofisini kwake ili wachukuliwe hatua.

Aidha, amesema ni marufuku kwa mwanaume kumpiga mwanamke mkoani humo na watakaofanya hivyo watachukuliwa hatua kali.

Maelekezo hayo aliyatoa jana wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Jinsia Kanda ya Kaskazini, lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), lililofanyika kwa ushirikiano na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali na kuwaleta pamoja wanaharakati zaidi ya 600.

"Anayetaka kumpiga mkewe aje anipige na mimi, ni marufuku kumpiga mwanamke huo ni ukatili wa kijinsia, taratibu za kisheria zipo kwanini umpige? Yeyote anayepigwa na mume wake aje kushtaki ofisini kwangu ili hatua zichukuliwe," alisema.

Aliwataka wanaotakaokopeshwa mikopo ya halmashauri kulipa kwa wakati, ili wengine wakopeshwe, na inatolewa bila riba, zote zikiwa ni jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kuwakwamua kiuchumi makundi hayo.

Aliagiza vikundi vilivyokopa Sh. milioni 10 na kurejesha vipewe Sh. milioni 20 na wapewe mikopo mikubwa ya kuwawezesha kuondokana na umaskini kwa kuwa wakipewa fedha nyingi watakopa mashine SIDO.

"Mikopo ya mama (Rais) haina riba inalenga kuwaondoa wananchi kwenye umaskini, mimi leo hii wanawake wengi wakiondokana na umaskini nitakuwa na furaha sana, tutaishi kwa amani vizuri," alisema.

Pia, mkuu huyo wa mkoa aliwataka wananchi kutunza chakula na kupunguza sherehe kwa kuwa hali ya mabadiliko ya tabianchi ni kubwa na imesababisha mvua kukosekana.

"Nimesikia wengine wanachukua mahindi wanatengeneza pombe, tulishafanya tathmini kwa wilaya ya Same na tumeshapeleka kwa Waziri Mkuu, muda sio mrefu tutawaletea mahindi ya bei rahisi wananchi," alisema.

Babu alisema mvua sio za kutosha kwa muda mrefu na sasa hali ya chakula sio ya kuridhisha maeneo mengi hasa ya tambarare.

## Sababu nane ajali magari ya serikali zaanikwa

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limetaja sababu nane zinazosababisha magari ya serikali kuhusika kwenye ajali, mojawapo ni madereva wa magari hayo kuvaa ukuu wa kiongozi wake.

Kamanda wa kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, aliyasema hayo jana katika taarifa iliyotolewa kuhusu hali ya usalama barabarani.

Kamanda Mutafungwa alisema sheria ziko wazi na wahusika wanazijua lakini madereva hao wamekuwa wakijiamini na kushindwa kuheshimu sheria za usalama barabarani na kanuni zake. Alisema madereva hao hawaheshimu ishara, michoro na alama pamoja na maelekezo yanayotolewa na askari wa usalama barabarani.

"Kwa sababu unatumia barabara za umma unao wajibu wa kuheshimu sheria kama madereva wengine, dereva kuuvaa ukuu wa kiongozi wake na kufanya vile anataka bila kujali kuwa anatawaliwa na sheria za usalama barabarani na kujisahau, tabia hiyo ni chanzo cha ajali barabarani," alisema Mutafungwa.

Alitaja sababu nyingine ni baadhi ya viongozi wa serikali kutozingatia dhamana waliyonayo kwa vyombo vya umma walivyokabidhiwa hususani magari na kukosa utashi na uelewa wa kutosha juu ya sheria za usalama barabarani.

Alisema viongozi hao wanashindwa pia kukemea makosa hatarishi kama mwendokasi, kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari na kuona kama askari wa usalama barabarani wanawapotezea muda pale wanapochukua hatua kwa makosa hayo.

Kamanda Mutafungwa alitaja sababu nyingine ni baadhi ya madereva wa serikali kushindwa kutumia mbinu na dhana ya udereva wa kujihami hasa pale wanapokuwa na viongozi wao.

Alisema wanapokutana na miundombinu isiyokuwa rafiki wanaamini wao na magari yao wana haki ya kupewa kipaumbele hata mahali ambapo wanapaswa kuheshimu watumiaji wengine wa barabara.

Kamanda Mutafungwa alisema: "Wanaonyesha kupuuza na dharau na kufanya fujo zinazosababisha ajali zisizokuwa za lazima, dereva yeyote akijitambua kwa kujua nafasi yake katika familia na jamii na hali anayokuwa nayo kiafya na akathamini uhai aliopewa na Mungu atachukuwa tahadhari na hatajiweka katika hatari.

"Wako madereva ambao hawajitambui na huogopa kuweka wazi hali zao za kiafya kwa viongozi wao na kulazimisha kusafiri huku wakijua kiafya hawako timamu ama kwa uchovu, maradhi, msongo wa mawazo namna yoyote inayoweza kusababisha kupoteza umahiri katika udereva wao na kuwa hatari kwa watumiaji wa barabara," aliongeza.

Alibainisha kuwa madereva wengi hawapumziki kiasi cha kutosha, huku akieleza kuwa kiafya dereva anatakiwa kuendesha gari si zaidi ya saa nane bila kupumzika, kwamba kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu, ajali zilikuwa ni 1,277 na kati ya hizo 135 zilitokana na magari ya serikali.

Kutokana na sababu hizo, Kamanda Mutafungwa, aliwataka madereva wa magari ya serikali kujitambua na kutii sheria kama madereva wengine.

Pia alisisitiza kuendelea kutolewa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa serikali ili kuwajengea uwezo wa kujitambua kama watumishi wa umma wanaopaswa kulinda uhai wao na wateja wao kwa kuheshimu na kutii sheria.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA**

**ONYO KWA WATUMIAJI WA NAMBA ZA USAJILI WA MAGARI ZISIZOTAMBULIWA NA TRA**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebaini uwepo wa magari barabarani yaliyobandikwa na kutumia namba ambazo hazijatolewa na TRA ama Taasisi nyingine za Serikali ambazo zimepewa jukumu hilo kisheria. Aidha, kumekuwepo na matumizi ya Vibao *(Number Plates)* vya namba vyenye rangi zisizotambulika kisheria vinavyowekwa mbele na nyuma ya vyombo vya moto.

Hivyo, wamiliki wa vyombo vya moto na umma kwa ujumla wanatangaziwa kwamba, utengenezaji na matumizi ya vibati hivyo ni kosa kisheria kama inavyoelezwa kwenye **Kifungu cha 8** cha **Sheria ya Usalama Barabarani** *(The Road Traffic Act, 1973)*. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote **anayekiuka sheria hii** ikiwa ni pamoja na **kutaifisha chombo cha moto husika**.

Kwa maelezo zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu au piga simu bure kwa Kituo chetu cha Huduma kwa Mlipakodi kupitia simu nambari **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016** au WhatsApp **0744-233 333** barua pepe huduma@tra.go.tz.




*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Imetolewa na;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

217080802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vizuri kujihadhari kabla ya hatari ugonjwa ebola

**HABARI** ya kuingia ugonjwa wa ebola katika nchi jirani ya Uganda, lazima ichukuliwe kwa umakini kutokana na ukaribu wa nchi hiyo na Tanzania na vile vile mwingiliano wa watu wake.

Ugonjwa huo ni hatari na unaua watu mara moja na dalili zake ni pamoja na kuumwa kwa kichwa sana na kutoka damu sehemu zenye matundu mwilini.

Katika kutambua umuhimu wa kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo, Wizara ya Afya imeamua kutoa mafunzo kwa baadhi ya waandishi wa habari mkoani Kagera kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao.

Mkoa wa Kagera uko mpakani mwa nchi ya Uganda, hivyo ni muhimu wananchi wake wakapewa tahadhari ya kujikinga na waandishi wa habari ni watu wanaozunguka maeneo mbalimbali na kukutana na watu tofauti.

Hata hivyo, katika mafunzo hayo kwa waandishi wa habari, Wizara ya Afya ilisema ugonjwa huo bado haujaingia nchini, lakini ni lazima hatua za kujikinga zinazotolewa na wataalamu zifuatwe na jamii wakiwamo waandishi wa habari.

Ugonjwa umeelezwa kuonekana wilayani Mubende nchini Uganda ambako ni jirani na Mkoa wa Kagera na wananchi wana mwingiliano wa mipaka kupitia Mtukula kuingia na kutoka na shughuli zinafanyika za kibiashara hivyo tahadhari lazima zichukuliwe.

Kazi ya waandishi wa habari ni kukutana na makundi ya aina tofauti ambayo kwa mwandishi hawezi kutambua wametokea mazingira yapi hivyo tahadhari lazima zichukuliwe.

Hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ni kunawa mikono kila wakati, kuepuka kushikana mikono, kukumbatiana kwa kuwa mgonjwa akipatwa na maambukizi ana asilimia 25 hadi 90 ya kifo.

Dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kuanzia siku mbili hadi 21 tangu mgonjwa anapopata maambukizi.

Pia katika kuhakikisha serikali inachukua hatua kudhibiti ugonjwa huo usiingie nchini, juzi Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitembelea mpaka usio rasmi wa Kashenye jirani na Uganda, Missenyi mkoani Kagera, kuhamasisha wananchi kuzingatia tahadhari zote za ugonjwa huo.

Akiwa kwenye eneo hilo, aliahidi kuweka wataalaamu wa afya katika mipaka isiyo rasmi yenye mwingiliano wa watu ili kuchukua tahadhari ya tishio la ugonjwa huo.

Pia alisema maeneo ya mipaka isiyo rasmi inatakiwa kupewa msukumo mkubwa kwa sababu kuna mwingiliano ambao ni hatari kwa tishio la ugonjwa huo.

Magonjwa ya milipuko ni tishio hasa panapokuwa na mwingiliano na mikusanyiko ya watu na kama hakutaka na tahadhari ya kujikinga ni rahisi watu kupata maambukizo na hatimaye ugonjwa kusambaa kwa urahisi.

Hatari ya kusambaa kwa ugonjwa ni mipaka ya nchi kufungwa, hali itakayosababisha uchumi kuyumba kwa sababu kila nchi hutegemea nchi nyingine katika masoko ya kibiashara.

Uchumi unapoyumba maana yake hali ya maisha huwa ngumu na baadhi ya bidhaa zikiwamo za chakula hupungua na matokeo yake nchi kuingia katika mtikisiko.

Hivyo, tahadhari ya ugonjwa wa ebola lazima ichukuliwe kwa umuhimu wa hali ya juu sana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Anaeli Mbise

# Bodi ya Nyama itupie jicho hoja ya usafi bucha, kasoro tuzionazo

**SUALA** la afya katika maisha ya binadamu ni kitu muhimu cha kuzingatia iwe kwenye chakula, huduma za hospitali au hata sehemu ambayo afya inahitajika.

Tunapozungumzia afya katika chakula, ni kumaanisha uandaaji, utunzaji na upikaji wa chakula hicho unakuwa umekidhi viwango vinavyostahili kwa matumizi ya binadamu.

Moja ya sehemu ambayo inatakiwa iwe na usafi wa hali ya juu, ni katika machinjio ya nyama za ng'ombe, kuku au hata mbuzi.

Aidha, sehemu nyingine ni katika bucha ambazo zinauza nyama hizo ili mlaji anunue na kwenda kupika kwa ajili ya matumizi ya familia.

Hivyo basi, ni vyema bucha zikawa na usafi unaokidhi vigezo ambavyo vimewekwa na Bodi ya Nyama Tanzania.

Moja ya vitu ambavyo mwandishi ameshuhudia katika baadhi ya bucha mkoani Dar es Salaam, ni namna ambavyo nyama zinakuwa zinatunzwa ili mteja anunue.

Baadhi ya wenye bucha wamekuwa wakitumia dawa ya kuua wadudu kama vile inzi ili wasiwe wakirukaruka katika nyama.

Kutokana na utumiaji wa dawa hizo, inasababisha kupungua ubora wa afya uliowekwa na mamlaka husika na kuleta madhara kwa watumiaji kiafya.

Hali kama hiyo, huenda pia ikaleta ongezeko la magonjwa ya kansa pamoja na saratani.

Bodi ya Nyama nchini, inapaswa ijielekeze katika majukumu yake ya kusimamia hili suala kwa sababu hivi karibuni wametoa takwimu zikionyesha ongezeko la uuzaji wa nyama nje ya nchi.

Miongoni mwa majukumu ambayo Bodi ya Nyama, inatakiwa kusimamia, ni pamoja na kuhamasisha, kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo ya tasnia ya nyama.

Pia kuna kuandaa, kutekeleza na kusimamia mpango mkakati wa kuendeleza tasnia ya nyama.

Aidha, bodi hiyo inahamasisha uzalishaji kwa kutumia teknolojia sahihi ili kuzalisha nyama bora itakayokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

**Kujenga uwezo wa ushindani wa kibiashara miongoni mwa wadau wa tasnia ya nyama.**

Vilevile, inakusanya, inachambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa na takwimu muhimu zitakazosaidia kuboresha, au kuongeza uzalishaji, uwekezaji, usindikaji na masoko.

Bodi hii pia inahamasisha uundaji na uimarishaji wa vikundi na vyama vya wadau katika tasnia ya nyama.

Jukumu lingine ni kuendeleza sekta na kusimamia ubora wa mifugo, nyama na mazao yake.

Kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na udhibiti wa ubora, kudhibiti ubora wa viwango vya uzalishaji wa mifugo, nyama na mazao yake kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 na kanuni zake.

Kutafuta, kuendeleza na kufuatilia masoko ya mifugo, nyama na bidhaa zake ndani na nje ya nchi.

Kujenga uwezo wa ushindani wa kibiashara miongoni mwa wadau wa tasnia ya nyama.

Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kufanya utafiti wa masoko ya mifugo, nyama na bidhaa zake na kuyaendeleza.

Bodi hiyo ina jukumu la kusimamia na kufuatilia mikataba ya masoko kati ya wazalishaji na wafanyabiashara, wasindikaji na kusuluhisha pale inapotekea kutoelewana baina ya pande hizo.

Kadhalika, ina kazi ya kufanya ushawishi na utetezi wa wadau wa tasnia ya nyama.

Ni vyema sasa kwa Bodi ya Nyama kukaa na kuwaelekeza ama kuwakumbusha wauzaji na wadau wa nyama namna bora ya kuhifadhi na kuuza kwa usafi unaotakiwa.

Hali hiyo itaondoa uuzaji wa nyama kiholela katika bucha ambazo hazina viwango na ubora unaotakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi, lakini kutaondoa kabisa ama kupunguza upulizaji wa dawa hizo kwenye vitoweo hivyo.

## Taasisi yaadhimisha wiki huduma kwa wateja kwa kuchangia damu

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya huduma za kifedha ya Faidika, imeadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja Duniani kwa kuchangia damu salama kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Uchangiaji huo wa damu uliwahusisha wafanyakazi wote wa Faidika walioko makao makuu, Dar es Salaam na matawi yao ya mikoani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kinondoni Morocco, Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo, Masoko na Mifumo, Asupya Nalingigwa, alisema wanajisikia fahari kubwa kushiriki katika kuchangia damu salama ambayo itatumika kwa ajili ya wagonjwa mbalimbali wenye uhitaji.

Nalingigwa alisema kuwa Taasisi ya Faidika inafanya kazi na jamii ambao ndiyo wateja wao wakubwa, hivyo ni wajibu wao kushiriki katika shughuli za kijamii.

"Faidika ni taasisi ambayo ina wateja wa aina zote na kufanikiwa kuwafikia wateja wengi. Ni wazi kuwa jamii ina kutana na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji msaada. Kuchangia damu ni moja ya shughuli kubwa kijamii kwani damu tunayochangia inakwenda kusaidia wagonjwa wenye uhitaji.

"Tumeamua kuadhimisha wiki ya huduma kwa wateja kwa kuendesha zoezi hili na limefanikiwa sana kwani wafanyakazi wote wamechangia damu salama," alisema Nalingigwa.

Aliongeza kuwa hata wafanyakazi wa matawi yao ya mikoani, wameshiriki katika uchangiaji huo na suala hilo kwao litakuwa endelevu.

"Sisi tumechangia damu kwa ajili ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Wenzetu wa mikoani wamefanya hivyo kwa kuchangia hospitali au vituo vya afya. Ni faraja kubwa sana," alisema.

Nalingigwa alisema Faidika imezidi kupanua wigo wa shughuli zake kwa kutoa mikopo ya aina mbalimbali kwa wafanyakazi wa serikali, sekta binafsi na wajasiriamali.

Alisema mpaka sasa wametumia jumla ya Sh. bilioni 68 kukopesha wafanyabiashara wadogo wadogo na wafanyakazi wa sekta tofauti.

Pia alisema wameboresha huduma zao kwa wateja kwa asilimia 100 ambapo mikopo hiyo inatolewa ndani ya saa 24 tena kwa kidigitali na kwa masharti nafuu.

# TPA yawapa matumaini wadau madini kuhusu ubora huduma

**Mwandishi wetu,** GEITA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imewakikishia wadau wa madini kuendelea kuhudumiwa kwa weledi na ufanisi wakati wote wa kusafirisha nje ya nchi au kuingiza nchini bidhaa na malighafi zinazohusu sekta hiyo.

TPA inashiriki katika Maonyesho ya Tano ya Sekta ya Madini yanayofanyika mkoani hapo yakishirikisha wadau wa madini wa ndani na nje ambayo yanahudhuriwa na mamia ya wananchi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TPA, Nicodemus Mushi, alisema jana kuwa mamlaka hiyo imetumia vyema maonyesho hayo kukutana na wadau muhimu wa sekta ya madini ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa kiwango cha shehena zinazopita katika bandari za Tanzania na hasa Bandari kuu ya Dar es Salaam.

"Shughuli za madini zina mchango mkubwa sana. Tunategemeana kwa kiasi kikubwa bidhaa za madini, mitambo na malighafi za uchimbaji ambazo ni shehena muhimu zinazopita katika bandari zetu," alisema.

Mushi alisema wakati sekta ya madini ikitegemea bandari katika usafirishaji, TPA inategemea shehena hizo katika kuingiza mapato kupitia biashara ya bandari kwa ujumla.

Tanzania inahudumia nchi nane majirani kupitia bandari zake na hasa Dar es Salaam huku nchi zenye utajiri wa madini kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zambia zikiwa wateja wakuu wa TPA. Nchi hizo kwa mwaka 2021/22 zilipitisha zaidi ya tani 450,000 za madini katika bandari hiyo.

Katika mipango yetu ya muda mfupi na mrefu, tutaendelea kushirikiana na wadau wa sekta hii ya madini ili kuhakikisha kuwa, wanapata huduma bora, usalama wa uhakika na gharama nafuu kulingana na mahitaji yao wakati wote.

Pamoja na maonyesho hayo kutawaliwa na shughuli za madini, wananchi waliotembelea banda la TPA wameonyesha shauku kubwa ya kufahamu shughuli za mamlaka hiyo hasa huduma za mafunzo yanayotolewa na Chuo cha Bandari kuhusu uendeshaji wa shughuli za meli na bandari, uingizaji na utoaji wa mizigo bandarini, taratibu za usafirishaji ndani ya maji, matengenezo ya vyombo na mafunzo ya zimamoto na uokoaji.

Wadau wa sekta ya madini walipongeza serikali kwa kuiwezesha TPA kukamilisha miradi kadhaa ya upanuzi wa bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na kukamilika kwa ujenzi wa bandari mpya ya Karema katika Ziwa Tanganyika.

Wakala wa Madini anayefanya shughuli zake kati ya Tanzania na Zambia, Felix Wambali, alisema kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema ni mafanikio makubwa kwa Tanzania kwa kuwa itakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya uchukuzi na uchumi wa taifa.

Bandari ya Karema ni habari njema sana kwetu wafanyabiashara, umbali kati ya Karema na Mji wa Kibiashara wa Kalemii ni mfupi sana na kwa kutumia bandari hiyo, tutaokoa muda na kiasi kikubwa cha fedha ambazo ni gharama za usafirishaji.

Wambali anazishauri serikali za Tanzania na Congo kuunganisha nguvu zao ili kujenga miundombinu ya kibandari upande wa Congo kuwa upande wa Tanzania, kazi kubwa imefanyika katika ujenzi wa miundombinu ya kibandari hali inayohitaji uwekezaji kama huo kufanyika pia upande wa pili ili kuwezesha biashara ya usafirishaji kufanyika.

MAURITIUS - AFRICA: TRADE AND INVESTMENT FORUM

ECONOMIC DEVELOPMENT BOARD MAURITIUS

BUSINESS FORUM & BUYER-SELLER MEETING

JOHARI ROTANA
DAR ES SALAAM, TANZANIA
17-18 OCT 2022



DISCOVER THE MAURITIAN EXPERTISE

Major Sectors: Light engineering | Medical devices | Electronics | Chemicals | Textile & Apparel | Agro-processing | Furniture & Jewellery

Our Partner
OACPS BUSINESS FORUM

R.S.V.P

E: KTB@edbmauritius.org
T: +255 769119859 (Patrick Magai)
Link: http://forms.edbmauritius.org/cn/al935/MATIF2022

217076202

# Shaka akoshwa kasi ujenzi reli SGR

**Na Beatrice Shayo,** KILOSA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unakwenda vizuri na kuna baadhi ya watu waliwaaminisha wananchi kuwa miradi ya kimkakati itakwama na sasa wanaona aibu.

Shaka aliyasema hayo akiwa kwenye ziara yake wakati akizindua msimu wa kilimo kimkoa wilayani ya Kilosa mkoani Morogoro huku akisema ndoto za watu hao haziwezi kutimia.

Alisema hivi karibuni kuna majaribio yaliyofanywa na kamati ya bunge kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam na mambo yameiva, hivyo wananchi wa Kilosa wajiandae kutumia fursa hiyo.

Kukamilika kwa miundombinu ya barabara na reli ya kisasa, alisema kutawasaidia kuongeza chachu katika uchumi kwa kuwa watapokea wageni wengi na kuwapo kwa mzunguko wa fedha.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia na malengo yake ni kuwatoa wananchi katika wimbi la umaskini kwa vitendo na hawajakosea kumpa hiyo nafasi.

"Itashangaza kuona wageni wanatoka nje kufanya uwekezaji Kilosa wakati wananchi wa Kilosa mpo hapa mkawa nyuma kutumia fursa. Nimeona kwa macho yangu katika wale mashahidi wa kuona na mimi nimeona namna ambavyo mradi huu wa reli ya kisasa ulivyojengwa kwa viwango," alisema Shaka.

Aidha, Shaka alisema mpango wa mwaka 2025 wasipate shida wanahangaika na maendeleo hawazungumzii kwa sasa nani atakuwa Rais kwa kuwa yupo ambaye ni Samia Suluhu Hassan.

"Sisi hatuzungumzi tutashindaje mambo mazuri ni kama haya ambayo tunayafanya. Barabara tunajenga, reli ya kisasa inakwenda kufungua uchumi, vituo vya afya, shule tunajenga, maji tunaleta. Mnataka nini tena? Tunakwenda kwa vitendo hatuna taabu mwaka 2025.

"Nataka kuwahakikishia nadhani mmesikia bajeti ya Wizara ya Nishati ifikapo mwaka 2025 tunamaliza vitongoji vyote. Tumejipanga kutafsiri dhana ya maendeleo kwa vitendo na si kwa maneno kwa sababu ndiyo maelekezo ya ilani yanavyotuambia".

Alisema wao walisimama na kuinadi ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/25 walizunguka kata zote katika kila mkoa, hivyo wabunge na madiwani wasiposimamia ilani kwa sasa watajikuta katika wakati mgumu.

"Niwaombe wabunge na madiwani kurudi kwa wananchi sina wasiwasi na wabunge na madiwani wa hapa ila mpo wengine madiwani wajanja wajanja," alisema Shaka.

Aidha, Shaka alisema katika utaratibu wa kugawa maeneo kwa ajili ya kilimo kwa vijana fedha za asilimia 10 za halmashauri waangalie namna nzuri ya kuwasaidia vijana hao.

Shaka alitoa rai kusimamia fedha hizo, wanataja kiasi kikubwa cha fedha kimepelekwa kwa wananchi ukiangalia kwenye marejesho hakuna kitu.

"Mkiwapatia vijana hao mtakuwa na takwimu sahihi kwa sababu serikali imeshawasaidia kuwatambua hawa vijana lakini mtakuwa na uhakika wa marejesho kurudi," alisema Shaka.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, akimkabidhi tuzo ya heshima kama kiongozi kijana wa mfano Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, wakati wa uzinduzi wa msimu wa kilimo kimkoa, wilayani Kilosa, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabadiliko tabianchi yaongeza ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MABADILIKO ya tabianchi yameelezwa kuwa aina mpya ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kutokana na rasilimali muhimu kuendelea kupungua huku nguvu ya uchumi ikiwa kwa wanaume.

Aidha, waathirika wakubwa wa mabadiliko hayo ni wanawake ambao wataenda kutafuta kuni na maji, huku wanaume wengi wakihama kutafuta malisho au kazi na kuziacha familia chini ya mama ambaye anashindwa kupata mazao kwenye kilimo.

Akiwasilisha mada ya Haki ya Kiuchumi: Fursa za Kilimo Zinufaishe Makundi Yote, Ofisa Programu Mkuu wa Jukwaa la Mabadiliko ya Tabia Nchi (Forum CC), Msololo Onditi, wakati wa Tamasha la Jinsia Kanda ya Kaskazini lilioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alisema athari za mabadiliko hayo ni tatizo jipya kufikia usawa wa kijinsia. "Kukiwa na shida ya maji anayehangaika ni mama, kukiwa na kiangazi cha muda mrefu baba atahamisha mifugo na mwanawe wa kiume atamuacha mama na mtoto wa kike ambaye anaweza kujitokeza mtu kutaka kumuoa mama akaona ni namna ya kujipatia kipato," alisema na kuongeza:

"Kama kuna ukame chakula kinacho patikana ni kidogo mama atahakikisha watu wote wa nyumbani kwake wamekula vizuri ila yeye atabaki na njaa, ataathirika kiafya, hivyo wanawake ni wahanga wakubwa."

Onditi alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zimejikita zaidi katika makundi ya kijinsia ambayo ustawi wao uko katika mazingira hatarishi zaidi kuathiriwa na uwezo duni wa kuhimili hali hiyo.

Aidha, alisema athari za mabadiliko hayo ni kubwa zaidi kwa watu, kaya na jamii katika nchi maskini, ambazo unaweza kuta wana wagonjwa, wenye ulemavu na wahitaji wengine kama hawana maji na chakula hali inakuwa ngumu kwao.

"Ni ukweli wa tofauti za jinsia wanaume wana maamuzi kuhusu umiliki na matumizi ya rasilimali za kijamii na kiuchumi tofauti na wanawake ambao ni wategemezi na watumiaji wakuu wa raslimali hizo," alifafanua.

Onditi alisema jamii nyingi wanaume wanahodhi zaidi fursa za kiuchumi wakati wanawake ni wazalishaji wakuu wa chakula,na kwamba kwa kiasi kikubwa majukumu ya wanawake hutegemea maliasili kama ardhi, maji na misitu.

"Wakati wa majanga mara nyingi wasichana huwa wahanga wa kwanza kuachishwa masomo ili kusaidia familia zao kujikimu,ikiwemo uzalishaji mali na kufanya shughuli za nyumbani,"alisema na kuongeza:

"Kipato cha kaya kinapoyumba na kutishia ustawi wa familia,ndoa za utotoni hujitokeza kwa kuwa wasichana wadogo kuozeshwa huonekana kama sehemu ya suluhisho la kadhia hiyo."

Mshiriki kutoka Kigamboni, Subira Kibiga alisema wanawake wengi hawana ardhi wamebaki kuwa vibarua na wakodishwaji,huku akiiomba serikali kufanya tathimini ya umikili wa ardhi kwa wanawake na wanaume ili kujua namna gani wanaweza kuweka usawa.

Naye, mshiriki kutoka Vumari,Same, Hadija Mkwizu, alisema hali ya chakula ni ngumu kutokana na mvua chache,wanakosa fedha za kusomesha watoto kwa kuwa kilimo cha kutegemea mvua kina maumivu kwao.

Naye, Mwakilishi kutoka Mwanga, Justice Msuya, alisema wananchi wanatunza maeneo yao lakini kuna uvamizi wa mifugo kutoka maeneo mengine na kila wanapohoji kwa serikali wanaambiwa watanzania wana haki ya kuishi kokote,lakini wao walishaharibu kwao wanahamia kulikotunzwa..

## Sera ya vijana kupunguza uhalifu Zanzibar

**Na Beatrice Moses**

KUPATIKANA kwa Sera ya Vijana pamoja na kutambua vipaji vyao ni miongoni mwa mambo yaliyotajwa kuwa yanaweza kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kupunguza vitendo vya uhalifu nchini.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, kwenye warsha iliyotolewa mjini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), kwa vyombo vya habari, imebainisha kuwa mafunzo hayo yametolewa yakiwa na ajenda kuu ya 'Upatikanaji wa Haki', ambayo inaakisi ongezeko kubwa la uhalifu wa kijamii miongoni mwa vijana visiwani humo.

Mustafa ambaye alikuwa ni mgeni rasmi katika warsha hiyo, aliwataka vijana kutumia vipaji vyao kufanya mabadiliko chanya katika maeneo yao ya kazi.

Aliipongeza kaulimbiu kwa kuwa inaendana na sera ya serikali ambayo imekuwa ikisaidia kukabiliana na tatizo la ongezeko la idadi ya vijana wanaotumbukia kwenye uhalifu.

Katika mafunzo hayo ambayo yameandaliwa na Jumuiya ya Wahitimu wa JICA Tanzania (JATA) ili kuwapa fursa ya kusambaza ujuzi walioupata kupitia programu za mafunzo ya JICA (KCCP), ikilenga kupunguza idadi ya kesi za uhalifu kwa vijana kisiwani humo.

Gregory Mlay, Mwenyekiti wa JATA alibainisha kuwa JICA imekuwa mstari wa mbele kushiriki katika maendeleo ya nchi, pamoja na kusaidia mafunzo mbalimbali kwa Watanzania.

Aliongeza kuwa JATA imekuwa ikifanya shughuli mbalimbali kila mwaka ili kuendelea kuimarisha ushirikiano wake na Japan pamoja na kuwasaidia Watanzania, hivyo mafunzo hayo ni fursa kwao ya kutumia ujuzi na maarifa waliyopata huko Japan kwa manufaa ya jamii, maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Katika hatua nyingine wanachama wa JATA walijadili njia kadhaa za kuwaelimisha vijana na kuwasaidia katika kukuza ujuzi kupitia mafunzo na ushauri ili kutengeneza fursa za ajira zinazofaa kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Pia kulikuwa na mjadala wenye dondoo za kupunguza kasi ya vifungo kwa vijana pamoja na kuleta uelewa kwa jamii kuacha kuwabagua wanaomaliza vifungo na kurejea kwenye maisha ya kawaida ya jamii.

## Kituo wenye ulemavu chalia ukosefu fedha

**Na Beatrice Shayo**

KITUO cha kulelea watoto wenye ulemavu na wanaoishi katika mazingira magumu cha Amani, Kata ya Chamwino mkoani Morogoro, kinakabiliwa na changamoto ya uchumi na uchakavu wa majengo.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Msimamizi wa Kituo hicho, Padri Beatus Sewando, wakati akipokea msaada wa mchele, maharage, taulo za kike, juisi, biskuti, unga, mafuta na sabuni ya unga ambazo zimetolewa na Umoja wa Waandishi wa Habari Wanawake Dar es Salaam chini ya Asasi ya Sauti ya Matumani Foundation (SAMAF) kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya Itel.

Alisema kituo hicho kilivyoanzishwa walikuwa wanapatiwa misaada mingi na mashirika mbalimbali ya nje na kusababisha kujengwa kwa majengo hayo.

Padri Sewando alisema baada ya mwanzilishi wa kituo hicho kufariki dunia ufadhili ulikwama, hivyo kwa sasa wana changamoto kubwa ya kiuchumi kwa kuwa wanajiendesha kwa kutegemea huruma za watu.

"Kama ninyi mlivyokuja tukiangalia msaada wenu napata faraja watoto watakula tunaishi kwa kutegemea misaada ya humu ndani. Wakati nimeanza kuja hapa mwaka 2007 wazungu walikuwa wanakuja nikawa nawatembeza wanaona makanisani na misikitini wakaniambia watu wanajaa makanisani kweli hawa wanashindwa kuwalisha hawa watoto? Hatuna sababu ya sisi kuwaonea huruma na sisi tunao watu wenye ulemavu nikafikiri utani hawakurudi tena," alisema.

Pia alisema nafasi anayopewa hasa mtoto mwenye ulemavu wa ubongo huonekana katika jamii kama ni mkosi au balaa na kujikuta wanapata malezi magumu kuanzia nyumbani.

Alisema baadhi ya wazazi wanakuwa na imani kuwa ni mkono wa mto na kujikuta wakitunzwa katika mazingira magumu na wengine kuwaficha mazingira hayo husababisha kupata vifo vyao vya haraka.

"Kutokana na hali hiyo Kanisa Katoliki liliamua kuanzisha kituo hicho kwa lengo la kutoa elimu kwa wazazi kuhusu haki ya watoto hawa na kama wanazaliwa na matatizo wanastahili haki zao na sio kuwanyanyapaa ama kuwaficha," alisema.

Naye Mwanzilishi wa Umoja huo, Penina Malundo, alisema kazi yao kubwa ni kurejesha tabasamu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wale wenye ulemavu kwa kuwapatia mahitaji yao muhimu.

Alisema mbali na elimu hiyo pia wamekuwa wakitoa taulo za kike kwa mabinti hao za kipindi cha miezi sita ili ziweze kuwasaidia mabinti hao kuweza kupata hedhi salama ambayo itawafanya kutokuwa wanyonge kwa kuendelea na shughuli zao kama masomo.

# Bashe apiga marufuku wakulima kutozwa fedha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amezindua msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023 na ugawaji wa mbegu za alizeti mkoani hapo huku akipiga marufuku wakulima kutozwa fedha yoyote wakati wa kuwasajili kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku.

Aidha, amegeuka mbogo wakati akikagua mabanda ya maonyesho baada ya kubaini wakala aliyepewa zabuni kusambaza mbolea kwa wakulima wa mkoa wa Singida bado hajaanza kutekeleza jukumu hilo.

Akizungumza na wakulima na viongozi wa wilaya za mkoa wa Singida, alisema serikali imeamua kuwasajili wakulima baada ya kubaini kuwa miaka yote ruzuku inayotolewa na serikali kwa mabilioni ya fedha wanaonufaika si wakulima.

"Ni marufuku mkulima kutozwa hela yoyote kwenye shughuli za usajili na mkulima ukiambiwa na mtendaji au mwenyekiti lipia hiki toa taarifa mfuate diwani au mbunge umweleze," alisema.

Bashe alisema faida watakayopata wakulima kutokana na kusajiliwa kutawawezesha kununua mbolea yenye ruzuku kwa bei elekezi ya serikali.

Pia aliziagiza halmashauri katika mikopo ya asilimia 10 wanayotoa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu, zielekezwe kwenye kilimo badala ya kuzitoa kwa kukopesha bodaboda. Alisema iwapo fedha hizo zitaelekezwa kwenye kilimo, zitasaidia ustawi wa mapato kwenye halmashauri.

Kuhusu mikopo wa wakulima inayotolewa na benki, alisema mkulima yeyote akienda benki kupewa mkopo na kuona riba ni zaidi ya asilimia 10 aende kwa mkuu wa wilaya na nyaraka kutoa taarifa ili hatua zichukuliwe.

Bashe alisema ameziambia benki zote nchini zitakazonufaika na fedha za kilimo ni zile zitakazoweza kuihudumia sekta ya kilimo na kutoa riba chini ya asilimia 10 ndio itafanya biashara na Wizara ya Kilimo.

"Mimi wala sijali kufika hapa kuwaambia wakulima wa alizeti benki yoyote ambayo ni rafiki ni benki hizi zingine hazituelewi kwa hiyo kama mna akaunti kule kazifungeni," alisema.

Bashe aliongeza kuwa haiwezekani wakulima wawe wanalima mashamba madogo sababu ya ukosefu wa mitaji wakati wa msimu wa kilimo benki zinakuwa nyeupe lakini ukifika wakati wa mavuno zinakuwa 'bize'.

"Atakayemiliki sayansi na uwezo wa kuzalisha mbegu maana yake amemiliki uwezo wa watu kula na ndiye atakayetutawala," alisema.

Bashe alisema mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita ni kuweka nguvu kwenye utafiti, uzalishaji wa mbegu, upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani.

Alisema ili tuondoe tatizo la mafuta ya kula nchini zinahitajika tani elfu 15 za mbegu bora ya alizeti ambapo mwaka huu uzalishaji wa mbegu ulifikia tani 2,900 kutoka tani 223 zilizozalishwa mwaka jana.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua mbegu za alizeti kwa ajili ya msimu wa kilimo wa 2022/2023, mkoani Singida juzi. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba na (kushoto) ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa huo, Juma Killimbah. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mdai aeleza sababu kufungua kesi fidia mil. 500/-

**Na Grace Gurisha**

MFANYAKAZI wa Wizara ya Kilimo, Florence Samweli, ameieleza mahakama kuwa kilichomsukuma afungue kesi kudai fidia ya Sh. milioni 500 ni baada ya kutolewa tezi bila kujua na kutumia dawa maisha yake yote.

Samweli alifungua shauri la madai dhidi ya Hospitali ya TMJ, Hindu Mandal pamoja na Daktari Bingwa wa Tezi Tanzania, Dk. Maurice Mavura, akidai fidia ya Sh milioni 500 kwa kupewa majibu ya kansa wakati hana ugonjwa huo.

Alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati akifanyiwa mahojiano na wakili wake, Norbert Mlwale, baada ya kuulizwa maswali na mawakili wa wadaiwa.

Pia alidai kuwa alifungua shauri hilo kutokana na madhara aliyoyapata na dawa alizotumia pamoja na gharama zake zaidi ya Sh. milioni 50.

"Matokeo yaliyoonyesha nilitolewa tenzi. Sikuwa na kansa na madhara niliyopata ya kutumia dawa maisha yangu yote ndiyo yalinifanya nifungue shauri hili," alidai Samweli.

Kadhalika, alidai hakumbuki kama alitia saini kabla ya kufanyiwa upasuaji wa tezi kwa sababu hakuona nyaraka yoyote ya kutia saini na wala kuisoma.

Samweli alidai kuwa hakujua kama ametolewa tezi kwa sababu Dk. Mavura hakuelezwa suala hilo. Pia, alidai kama Dk. Mavura angemshauri madhara ya upasuaji huo, inawezekana asingefanyiwa.

Alidai kuwa Juni 27, 2018 alikwenda katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na alifanyiwa uchunguzi wa koo ndipo alielezwa amwone Dk. Mavura na akamwelekeza aende katika Hindu Mandal kwa kuwa ina vifaa vya kisasa kwa ajili ya upasuaji.

Pia alidai kuwa Julai 9, 2018 Dk. Mavura alimfanyia upasuaji katika koo lake na alitoa sampuli za tezi la kushoto zikapelekwa katika hospitali ya TMJ kwa ajili ya uchunguzi na matokeo kuonyesha kuwa alikuwa na ugonjwa wa 'Rapillary Carcinoma of Thyroid'.

Baada ya kukabidhiwa ripoti hiyo, alidai kuwa Dk. Mavura alimfanyia upasuaji wa pili na kuiondoa tezi iliyoambukizwa ugonjwa huo. Sampuli za tezi zenye ugonjwa huo zilipelekwa TMJ kwa ajili ya uchunguzi mwingine ambapo ripoti ilionesha tezi hizo hazina ugonjwa wowote.

# DAWASA yasambaza majisafi viwanda 42

**Na Joseph Mwendapole,**
KIBAHA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Pwani (DAWASA), inatoa huduma ya majisafi kwa viwanda 42 kati ya 54 vilivyoko katika Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani.

Hayo yalibainishwa jana mkoani hapa na Meneja Mawasiliano wa DAWASA, Everlasting Lyaro, wakati akizungumza kwenye maonyesho ya tatu ya Wiki ya Uwekezaji na Biashara ya Mkoa wa Pwani.

Alisema licha ya wananchi wengi wa Pwani kunufaika na huduma ya maji safi na salama, wawekezaji na wenye viwanda wengi wamenufaika na huduma zinazotolewa na DAWASA.

Lyaro alisema kwenye maonyesho hayo, DAWASA imekuwa ikisikiliza kero za wananchi kuhusu upatikanaji wa maji na kuzitatua papo kwa hapo.

Maonyesho hayo yanayoendelea katika viwanja vya stendi ya zamani Maili Moja mjini hapo, yamebeba kaulimbiu ya 'Pwani ni Sehemu Sahihi kwa Uwekezaji', Pamoja Tujenge Viwanda kwa Uchumi na Ajira Endelevu".

Alisema kupitia maonyesho hayo, DAWASA inatoa elimu mbalimbali ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi wa Pwani wanaofika katika banda la mamlaka pamoja na kupokea changamoto na kuzipatia ufumbuzi wa papo hapo.

Mwitikio wa wananchi wa Pwani, alisema ni mkubwa na alitoa wito kwa wananchi zaidi wanaotembelea maonesho hayo waendelee kufika kwenye banda la DAWASA.

Alisema kwenye banda hilo watapata elimu kwani lengo la DAWASA ni kuhakikisha kila mwananchi aliyefika anahudumiwa kwa viwango vilivyowekwa na mamlaka.

"Tumefurahi kuwa sehemu ya washiriki katika maonesho haya yanayolenga kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya sita katika kuendeleza sekta ya uwekezaji," alisema.

"Pia tunafurahi mwitikio ni mkubwa wananchi wamejitokeza kwa wingi na tunaomba waendelee kufika zaidi kwenye banda letu watapata huduma zote," alisema Lyaro.

Naye Yohana Mwangaya, ambaye ni mkazi wa Lulanzi Kibaha, alisema amefurahishwa na namna mkoa wa Pwani ulivyoweza kuzipata taasisi zote zinazogusa maisha ya watu na kuweza kusikilizwa kwa wakati mmoja.

"Nimefurahi kupata elimu ya namna ya kupata huduma ya maji kutoka DAWASA na taarifa za miradi iliyotekelezwa katika mkoa wa Pwani ambapo hapo awali nilikuwa sifahamu, natoa wito kwa wananchi wenzangu wafike katika maonyesho haya hususani banda la DAWASA wapate maelezo ya uhakika zaidi kuepusha kutapeliwa," alisema.




Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakitoa elimu kwa wananchi kuhusu shughuli mbalimbali za mamlaka hiyo, katika maonyesho ya tatu ya uwekezaji na biashara ya Mkoa wa Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TARI kuanzisha shamba darasa alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imepanga kuanzisha shamba darasa la alizeti katika mkoa wa Singida na kwamba mbolea za aina zote zitatumika ili kuona zinaleta ufanisi gani kwenye zao hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alitangaza mpango huo jana wakati wa uzinduzi wa msimu wa kilimo mwaka 2022/23 na ugawaji wa mbegu za alizeti zenye ruzuku zilizotolewa na serikali.

Alisema, TARI itaanzisha shamba darasa hilo ili kupima afya ya udongo kwa kuwa ziko mbolea za aina mbalimbali ambazo zitatumika katika zao la kimkakati kama alizeti ili kuona zinaleta ufanisi kwa kiasi gani.

Dk. Mkamilo alisema, TARI kwa kushirikiana na sekretarieti ya mkoa wa Singida na Wizara ya Kilimo itatoa mafunzo kwa maofisa ugani na wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji wa alizeti.

Kuhusu upatikanaji wa mbegu, alisema TARI itaendelea kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), kuzalisha mbegu za kutosha hususani zao la kimkakati la alizeti.

"Tayari tumeshakubaliana kiasi cha mbegu ya alizeti kinachohitajika ambacho TARI itazalisha kwa ajili ya kuipa ASA ili kuzalisha madaraja bora ambayo yatawafikia wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji wa alizeti," alisema.

Dk. Mkamilo alisema suala la viuatilifu TARI itahakikisha vinaangaliwa kisayansi kuangalia ni namna gani vitaondoa wadudu.

Mkoa wa Singida umetengewa kilo 500,000 za mbegu bora za alizeti ya ruzuku zenye thamani ya Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya msimu wa kilimo wa 2022/2023.

# Waonywa upandishaji holela wa bei za bidhaa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, amepiga marufuku tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei ya bidhaa za ujenzi pindi wanaposikia serikali imetoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo.

Sendiga amewataka wafanyabiashara hao kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Agizo hilo alilitoa juzi wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuwa serikali ya mkoa huo imepokea fedha zaidi ya Sh. bilioni 3.8 zitakazotumika kujenga vyumba vya madarasa 191 ili kuondoa upungufu wa madarasa mkoani hapo.

Mkuu wa Mkoa alisema kumekuwapo na madai kuwa baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa na tabia ya kupandisha bei za vifaa vya ujenzi pindi wanaposikia serikali imetoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa wakiamini kuwa huo ndio wakati wao wakujipatia faida.

Alisema mfanyabiashara atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria kwa kuwa atakuwa mhujumu uchumi na hawezi kuachwa aendelee kukwamisha jitihada za serikali na kuwaumiza wananchi kwa kuwauzia bidhaa kwa bei kubwa tofauti na bei halisi.

Sendiga alisema serikali imetoa fedha hizo na kupanga kuwa kila darasa moja litajengwa kwa thamani ya Sh. milioni 20 na ni lazima fedha hizo zitoshe lakini kama wafanyabiashara watapandisha bei ya vifaa vya ujenzi, huenda fedha hizo zisitoshe hali ambayo serikali ya mkoa haitakubali hilo litokee.

Pia aliwataka wawekezaji mbalimbali katika sekta ya utalii wajitokeze kwa wingi mkoani Rukwa kwa kuwa mkoa una fursa nyingi za utalii kuna vivutio mbalimbali na vya kipekee vilivyotangazwa na vingine bado havijatangazwa na havijulikani.

Alisema kuna fursa nyingi kwa wawekezaji hao ikiwamo ujenzi wa hoteli za kitalii, kuwafundisha vijana namna bora ya kuhudumia watalii na biashara ya usafirishaji watalii.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, hivi sasa watalii wengi wanamiminika nchini kutokana na Rais Samia Hassan kuvitangaza vivutio vilivyoko nchini kupitia filamu ya The Royal Tour.





## Wanafunzi jamii ya wafugaji wanolewa uhifadhi mazingira

**Daniel Sabuni,** LONGIDO

WANAFUNZI 3,000 wa jamii ya kifugaji wanaosoma katika shule za msingi na sekondari zilizoko kata za Gelai Merugoi na Gelai Lumbwa, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, wameanza kunolewa kuhusu uhifadhi kutokana na kuishi kwenye mazingira asili ya uhifadhi.

Elimu hiyo inatolewa na Mradi wa TUSHUMU unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Oikos East Africa.

Jana, Ofisa Elimu wa Shirika hilo, Rebecca Mnguruta, alisema wamelazimika kutoa elimu kwa wanafunzi wanaotoka kata hizo kwa kuwa zimezungukwa na hifadhi za misitu pamoja na shoroba za wanyamapori.

"Mradi wa utoaji elimu kwa wanafunzi, ulianza kutekelezwa Novemba mwaka 2021 na unatarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu.

Alizitaja shule nne za msingi zinazonufaika na elimu hiyo ni Gelai Bomba, Gelai Lumbwa, Ilchang'itsapukin, Magadini na shule za sekondari za Lekule na Natron Flamingo.

Lengo la kutekeleza mradi huo ni kuongeza maarifa juu ya jinsi ya kusimamia nyanda za malisho kwa uendelevu zaidi, ikijumuisha utambuzi wa mimea vamizi na kuheshimu kalenda za malisho.

Malengo mengine ni kupunguza migogoro, kati ya wafugaji, wakulima na wanyamapori wanaoshiriki mfumo ikolojia sawa na wenye maslahi yanayokinzana.

Kadhalika, lengo lingine ni kutoa elimu mahususi ya kukabiliana kwa usalama na wanyamapori na kuwaelewa wanyamapori hao, mahitaji na tabia zao ili kupunguza hatari.

Mmoja wa wanafunzi waliofaidika na elimu hiyo kutoka Shule ya Msingi ya Gilai Bomba, Sara Musa, alisema elimu waliyopata wameifikisha nyumbani na kujenga maboma hai kwa kutumia mimea yenye miiba kwa lugha ya kimasai 'esilalei' ambayo inazuia wanyama wakali kama fisi, chui na duma kuvamia mifugo na kuiua.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Gelai Meirugoi (WEO), Anna Mtera, akizungumzia elimu hiyo, alisema vijiji vitatu vya Meirugoi, Magadini na Loondoluo, vimetenga kiasi cha hekta 53 za nyanda za malisho ambazo zitaokoa mifugo wakati wa ukame.

Wakati, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Gilai Lumbwa (WEO), Jackson Mollel, aliyefaidika na elimu ya uhifadhi, alisema itasaidia kupunguza madhara ya wanyamapori yaliyokuwa yakikumba jamii hizo, kwani watoto ndiyo wachunga mifugo nyakati za likizo.

# Jela miaka 3 kwa kung'oa miundombinu ya maji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKAZI wa Mtaa wa Osterbey katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Iddy Issa (21), amehukumiwa miaka mitatu gerezani, baada ya kukutwa na hatia ya kosa la kuingilia miundombinu ya maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (BAWASA).

Iddy, alitiwa hatiani kwa kosa hilo jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Victor Kimario, aliyekuwa akisikiliza shauri hilo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kimario, alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 30 mwaka huu katika eneo la Bagara Ziwani.

"Mshtakiwa (Iddy) ametiwa hatiani na mahakama hii, baada ya kukiuka kifungu cha 20 (1) (2) na (3), jedwali la kwanza la Sheria ya Uhujumu Uchumi, Kifungu cha 57 (1) na 60 (2) cha Sheria hiyo iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

"Sasa kwa kuwa kitendo ulichokifanya siyo kizuri, na nia ilikuwa ni kuiangamiza jamii, kwa kukosa huduma ya maji, nakuhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela."

Kwa mujibu wa Hakimu Kimario, mshtakiwa alikutwa akifukua waya wa umeme ambao unasambaza maji kwenye makazi ya watu.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi sita na mshtakiwa alikuwa anajitetea mwenyewe.

Mshtakiwa alikata waya wa umeme wa kusambaza maji wenye ukubwa wa mita 12 na waya huo ulikuwa na thamani ya Sh. 500,000.

Awali, Wakili wa Serikali, Grace Mgaya, aliiomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kwa mshtakiwa, kwa kuwa maji ni muhimu kwa watu, serikali inatumia gharama kubwa kujenga miundo mbinu.



Meneja Uhusiano kitengo cha Bima cha Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Adolph Mushi, akiwahamasisha wachimbaji madini ya Tanzanite katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, kuhusu umuhimu wa kukata bima itolewayo na benki hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yatoa milioni 760/- ujenzi wa madarasa msingi, sekondari

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa Sh.milioni 760 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa katika Shule 15 za Sekondari za Halmashauri ya Arusha. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, alisema kiasi hicho kitatumika kujenga vyumba vya madarasa, kwa kila kimoja kikiwa na thamani ya Sh.milioni 20.

"Ndani ya vyumba hivyo vya madarasa, kutawekwa madawati 40 na kutakuwapo na madawati 1,520 kwa shule hizo.

"Kimsingi haya ni maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ifikapo Januari mwakani" alisema.


Mkurugenzi huyo alisema fedha hizo tayari zimewekwa kwenye akaunti za shule hizo, huku akieleza kuwa ujenzi huo utatekelezwa kwa kuwatumia mafundi jamii (force account) pamoja na matumizi ya ramani za madarasa yaliyojengwa kutokana na Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

Shule zitakazojengwa vyumba vya madarasa ni Bangata (darasa moja, Einoti (vyumba vinne), Endevesi (chumba kimoja), Kiranyi (vyumba viwili) na Likamba (vyumba vitatu).

Nyingine ni Losikito (chumba kimoja), Losinoni (vyumba viwili), Mringa (vyumba vinne), Mukulat (chumba kimoja),Musa (chumba kimoja),Oldadai (vyumba 11),Olemedeye (Chumba kimoja),Oljoro (vyumba viwili),Osiligi (chumba kimoja) na Sambasha (vyumba vitatu).

"Halmashauri ya Arusha inatoa shukrani za dhati kwa Rais, kwa kuwa wanafunzi 9,711 wamefanya mtihani wa darasa la saba mwaka huu, hivyo tunategemea ufaulu wa asilimia 100 kwa kuwa madarasa hayo, yatasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani ifikapo Januari, 2023,"alisema Msumi.

Awali kupitia fedha za mapambano ya UVIKO-19, serikali ilitoa Sh.bilioni 5.3 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 268 kwa shule 88 za sekondari kwa halmashauri saba za Mkoa wa Arusha.





# Mamlaka za ajira zaagizwa kulipa stahiki za watumishi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imeziagiza mamlaka za ajira nchini kuhakikisha zinaendelea kulipa stahiki za kisheria kwa watumishi wa umma ikiwamo likizo, mafunzo na posho mbalimbali.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala, Bora Jenista Muhagama wakati akifungua mashindano yanayohusisha watumishi wa umma.

Alisema serikali inaendelea kushughulikia kero mbalimbali za wafanyakazi ikiwamo malimbikizo ya mishahara, kupanda madaraja pamoja na ajira mpya.

Hivyo, aliwataka waajiri nchini kuzingatia kuwapandisha madaraja wafanyakazi na kulifanyia kazi suala la ubadilishaji kada ili kuimarisha ufanisi.

Pia aliwataka waajiri wote wahakikishe wanafuatilia kwa karibu mienendo ya watumishi wa umma nchini na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kila mtumishi anapanda daraja bila kucheleweshwa na upendeleo.

Waziri Mhagama alisema wizara inaendelea kusimamia maagizo ya serikali ya kuhakikisha kuwa watumishi wote wenye sifa za kupandishwa madaraja yanatekelezwa.

"Niwaambie ndugu zangu katika mambo ambayo Rais anaendelea kusimamia moja wapo ni kuhakikisha kwamba serikali inaendelea kusimamia haki na stahiki za watumishi wa umma katika sekta zote inatekelezwa kwa vitendo," alisema.

Aliongeza: "Niwatake waajiri kote nchini kuhakikisha mamlaka za ajira katika utumishi wa umma wahakikishe wanatenga bajeti ya kutosha kila mwaka katika mafungu yao, kulipa stahiki za kisheria ikiwamo likizo, mafunzo na posho.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), Henry Mkunda, alisema kuwa jukumu lao ni kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa mafunzo mbalimbali ili kuwajengea tabia ya kuwekeza hususani kwenye kilimo kabla ya kustaafu.

"Tunafanya mafunzo ya wafanyakazi kuhusu kujiandaa kustaafu kwani wanataka wafanyakazi wasisubiri chama cha wafanyakazi kiendelee kuwafundisha mambo mbalimbali yanayohusu haki zao katika sehemu za kazi wameona ni vyema wawaandae wafanyakazi kujua wataishije hata watakapostaafu," alisema.

# Samia kukabidhiwa takwimu za sensa ndani ya mwezi huu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi nchini, Anne Makinda, amesema kwa sasa wanakamilisha mchakato wa tathmini ya jumla kuhusu sensa ya mwaka huu ilivyofanyika na wataikabidhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, mwezi huu.,

Makinda alieleza kuhusu mchakato huo jana, alipokutana na kufanya kikao kazi na Kamati ya Sensa ya Mkoa wa Kilimanjaro. "Agosti 23, mwaka huu, Tanzania tulifanya Sensa ya Watu na Makazi, kwa sasa tunapita na kukutana na kamati hizi ili kuona matatizo waliyokutana nayo, kwa sababu tunataka kumpa Rais (Samia), uhalisia na tunatarajia kumkabidhi ripoti hiyo mwezi huu,"alisema.

Kwa mujibu wa tathmini hiyo, Makinda ameeleza kuwa walichobaini ni kwamba mikoa mingi walikopita, tatizo kubwa limeonekana ni watumishi wa umma waliopata nafasi za kufanya kazi hiyo, hawakuwa wazalendo.

"Waliongoza baadhi ya makarani kufanya mgomo wa kudai malipo zaidi, hii siyo sawa na hatua zitachukuliwa kuthibiti hilo," alisisitiza Makinda.

Katika Wilaya za Same na Mwanga, makarani wetu walikabiliwa na tatizo la tembo walipokuwa kazini na halmashauri kulazimika kutoa magari kwa ajili ya watumishi hao ili kuhakikisha wananchi wote wamepata huduma.

Katika hatua nyingine, Makinda, amemwelekeza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kutatua tatizo la mipaka ya kiutawala inayofukuta kati ya Wilaya ya Siha na Arumeru ya Mkoa wa Arusha.

Alisema katika suala la mipaka lilikuwa ni tatizo kubwa, kwamba lilifanya baadhi ya kaya kuhesabiwa katika mikoa mingine, akiahidi kulifanyia kazi kupitia mamlaka zilizoko.




Ofisa Elimu Mkoa wa Tanga, Newaho Mkisi (kulia), akikabidhi mwongozo wa utoaji wa chakula shuleni kwa Ofisa Afya Wilaya ya Mkinga, Bertha Mwakyusa, wilayani humo mapema wiki hii, ulioandaliwa na Shirika la Save the Children kupitia mpango wa utoaji wa chakula shuleni. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wakulima, wafanyabiashara wa ndizi kujadili uwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

KIKAO maalum cha wadau wa ndizi, wanaolima na wafanyabiashara katika masoko ya ndani na nchi jirani ya Kenya, watakutana kujadili mikakati ya uwekezaji na ukuzaji kilimo cha kisasa cha zao hilo.

Mbunge wa Rombo, ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema kwa kuwa ndizi ndio zao kubwa la biashara na chakula, serikali itahakikisha linatumika vizuri kubadili uchumi wa mkulima na taifa kwa ujumla wake.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wakazi wa Kata ya Mamsera wilayani humo, alipokwenda kuzindua mafunzo ya siku saba ya uzalishaji wa ndizi, yanayochagizwa na kauli mbiu ya 'ndizi kwa afya bora na kipato zaidi'.

"Niwadokeze tu kwamba tutafanya roundtable discussion (kikao cha meza ya pamoja) cha wadau wa ndizi wa Wilaya ya Rombo ili kujadili mikakati ya kukuza kilimo cha kisasa cha ndizi," alisema na kiongeza:

"Ni lazima tuangalie ndizi kama zao la biashara ambalo linatupa chakula cha uhakika. Tulishafanya mkutano wa ndizi Moshi na tulipanga kufanya mkutano wa kitaifa wa mkakati wa kukuza zao hilo nchi nzima, lakini hata hivyo ndizi bado ni uti wa mgongo wa uchumi wa Wilaya ya Rombo."

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, nchi ya Ecuado katika Amerika ya Kusini inauza ndizi kwa wingi na taifa hilo linapata zaidi ya Dola za Marekani bilioni mbili kwa mwaka, ambayo ni zaidi ya fedha ambazo Tanzania inapata kwa kuuza kahawa nje ya nchi.

Mwezi uliopita, kuliibuka mjadala baina ya wajasiriamali wadogo na vikundi vya wanawake na vijana, vyenye malengo ya kujiinua kiuchumi katika Wilaya ya Rombo na Moshi mkoani Kilimanjaro, juu ya jasho lao linalonyonywa na watu wa kati, maarufu madalali.

Mjadala huo uliibuka, wakati wa kikao kazi cha mradi wa mwanamke imara kilichoketi Moshi, kufanya tathmini ya shughuli zilizofanyika robo ya Julai hadi Septemba mwaka huu, chini ya Shirika la kiraia la KWIECO linalotekeleza mradi huo kwa ubia na mashirika wenza.

Lakini Ofisa Biashara Mkoa wa Kilimanjaro, James Bwanali, aliingilia kati na kutoa ufafanuzi akisema, serikali inakuja na mfumo wa uratibu wa taarifa mbalimbali za masoko, kama vile bidhaa mbalimbali zinazopatikana kwenye masoko, bei na sehemu ambayo bidhaa hizo zinaweza zikauzwa.

Ukurasa 17




Uwakilishi wa wazee bungeni sawa,lakini...!



**JICHO LA JIJINI MWANZA**

**Huu hapa mzizi daladala kukatisha'ruti', hoja ya Latra ilikosimamia**

Ukurasa 18



MADHILA YA AJIRA ZA WATOTO

# DC: Mwanza tunapokea watoto saba wa Ngara kila siku wa kazi nyumbani

## •Mamlaka yaanika 'madudu' wakutana nayo

**Na Neema Emmanuel,**

**MWANZA**

NENO umaskini ndio mara zote linatajwa chanzo kikuu cha wazazi na walezi kuangukia kisingizio cha kuruhusu watoto wao kusafirishwa kwenda mijini kuajiriwa kwa kazi, mbalimbali zikiwamo za ndani, bila ya kujali madhara yake.

Inatajwa takribani watoto saba hadi 10 walio na umri chini ya miaka 14, husafirishwa kila mwezi kwa mabasi kutoka wilaya ya Ngara na kufikishwa jijini Mwanza kwa ajili ya kufanya kazi za nyumbani.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, amefafanua kwenye mdahalo wa pamoja na wadau kuhusu haki za wafanyakazi wa nyumbani na kuvunja ukimya juu ya ukatili na unyanyasaji dhidi yao.

Anasema, takwimu hiyo inaashiria tatizo la watoto kuajiriwa chini ya umri ni kubwa, pia kwa mujibu wa taarifa walizo nazo Shirika la WoteSawa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba 22 mwaka huu, wamepokea jumla ya kesi 77 za wafanyakazi wa nyumbani.

Anafafanua, kati ya hizo 54 zinahusu madai ya mishahara, 23 watoto waliokuwa wameajiriwa chini ya umri miaka 14, huku watoto 54 ni wenye umri kati ya miaka 14 hadi 24, hivyo waajiri na walezi wana jukumu la kudhibiti wimbi la watoto hao kuajiriwa chini ya umri huo.

"Waathirika 51 kati ya 77 waliokolewa na kupita katika makao ya muda ya wote sawa kwa ajili ya huduma mbalimbali, watoto tisa miongoni mwao walirejeshwa shule, wakati watoto 41 waliunganishwa na familia zao," anaeleza Makilagi.



Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi. **PICHA: MAKTABA.**

Anasema, wafanyakazi wa majumbani ni kundi muhimu katika ustawi wa jamii na nguvu kazi ya taifa, japo wanaonekana kufanya kazi katika sekta isiyo rasmi, hivyo ni muhimu kuhakikisha wanapata ulinzi wa kisheria kwa kuzingatia wengi ni wanawake na watoto.

Anarejea sheria za nchi, kwamba ni marufuku kwa watoto wenye umri chini ya miaka 14 kuajiriwa na wale wanaoajiriwa katika umri sahihi, wanastahili ulinzi kisheria katika ajira zao.

"Ningependa kuona Jeshi la Polisi likichukia hatua stahiki kwa wale wote ambao wanakuwa wakiajiri watoto chini ya umri wa kufanya kazi za nyumbani," anaeleza Makilagi.

Ramadhani Musabi, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Majengo, Kata ya Mkolani, Mwanza, anasema kuna haja ya kukabiliana na madalali wa wafanyakazi nyumbani, kuchunguza watoto wanavyoingizwa mkoani humo hasa maeneo ya stendi ndio, jambo lenye tija na litakaloweza kupunguza ama kumaliza tatizo hilo na kuhakikisha kazi zinafanyika kwa kuzingatia kanuni na sheria.

Katika hilo, Elisha David, Meneja Mradi kutoka Shirika la Wote-Sawa, anarejea Sheria ya Mtoto, inayoagiza chini ya umri miaka 14, haruhusiwi kuajiriwa kwa kazi yoyote na kati ya 14 hadi 17 hutakiwa kufanya kazi nyepesi isiyozidi saa sita.

"Leo tumekutana na wakuu wa wilaya wanne, mwakilishi kutoka Idara ya Kazi Mkoa, mwakilishi kutoka CHODAWU (Chama cha Wafanyakazi), ofisa ustawi wa jamii, watendaji wa kata, mwenyekiti wa mtaa na ofisa wa polisi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto.

"Lengo la kuangalia namna bora ya kushughulikia kesi za wafanyakazi wa nyumbani pamoja na kuweka mikakati ya kudhibiti ajira kwa watoto," anaeleza David.

**WANALONENA WAZAZI**

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa Nyegezi Susana Arbogasti, anasema familia nyingi zinapenda kuajiri watoto, kwa sababu wanaweza kuwaendesha na hawana mengi tofauti na mtu mzima, ambaye ameshajitambua.

"Kwanza (watu wazima) wana gharama ndogo. Hiyo inamlazimu mtu kuajiri mtoto kuliko mtu mzima atakayehitaji kiasi kikubwa bila ya kujali madhara kwa mtoto na sisi wazazi tunahusika kuchochea ajira hizi tunapompeleka mtoto kufanya kazi. Sisi ndio tunapokea mshahara wake na yeye anafanya kazi tu," anaeleza.

Mchango kama huo, anao

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

# DC: Mwanza tunapokea watoto saba wa Ngara kila siku wa kazi nyumbani

INATOKA UK.13

Omary Ibrahim mkazi wa Nyamagana, anayeaimbia gazeti hili kuwa, suala la ajira kwa watoto, halifuatiliwi kwa kina na kila mara, jambo ambalo linawaacha watoto hao waendelee kuajiriwa katika sehemu wakidhalilishwa.

"Sasa hivi ukihitaji mfanyakazi unapiga simu tu unaletewa huwa naona mke wangu anaagiza na analetewa tunaishi naye, japokuwa siyo mdogo, lakini hatupajui kwao. Zaidi tunawasiliana na wazazi na ndugu zake kwa njia ya simu najua ni 'riski' hatuna namna muda wa kwenda kutafuta hatuna," anaeleza.

Anasema kwamba, licha ya wakati fulani vijana hao wanakumbana na matatizo mbalimbali ikiwamo manyanyaso, kutokujua sheria ni mwanya mkuu ambao waajiri hutumia, wakiamini hata wanapodhulumiwa, bado hawafiki popote. Katika hilo, anatumia mfano hukatwa mshahara hata pale mfanyakazi huyo anapovunja walau sahani nyumbani, anaishia kukatwa mshahara.



Mwonekano wa stendi ya mabasi yaendayo mikoani ya Nyegezi, Mwanza. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

**KUTOKA KWA WATENDAJI**

Sabina Mbunda ni Ofisa Kazi wa Mkoa wa Mwanza, anayesema wao Idara ya Kazi wanaamini katika ajira, lazima kuzingatia sheria na kanuni zilizoko kwa pande zote mbili, mwajiri na mwajiriwa.

Hapo anatoa mfano wa mkasa wa kuelimisha: "Kulikuwa na watoto wawili waliajiriwa wanatokea Kigoma, walikuwa wanauza duka wakafukuzwa na wakawa hawana hela.

"Kwa ushirikiano wa Mwenyekiti (mtaa) alitusaidia sana. Kesi nyingi tunazipata mtu anafanya kazi miezi saba hadi nane hajapatiwa malipo yake. Tunaomba mtusaidie kufikisha elimu na kuielimisha jamii itasaidia kupunguza migogoro na matukio mengi ya ukatili yanayotokea katika familia mbalimbali."

Hoja hiyo inaungwa mkono na Mkuu wa Polisi Dawati la Jinsia Mkoa wa Mwanza, Kagemulo Muhula, anayesema uzoefu alioapata katika utendaji wake, wanapokea kesi nyingi kutoka katika jamii, baadhi ni za wafanyakazi wa nyumba kubebeshwa tuhuma zikiwamo za wizi, ili kujengeke kigezo cha kudhulumiwa.

"Muwe makini mnapoenda kusuluhisha hiyo migogoro kati ya mwajiri na mwajiriwa, wengi wanabambika kesi kuwa ameniibia. Ukija kuangalia lengo lake ni kumdhulumu mshahara wake.

"Kuna kesi moja nilikutana nayo kituoni (polisi), nilikuta imefunguliwa. Ni kesi ya wizi. Pale ofisini kwangu nilikuta kuna begi, nikauliza hili begi la nani?' Nikaambiwa ni la binti ana miaka 17 ameshtakiwa ameiba kwa mwajiri wake.

"Nikasema 'hapana ebu nileteeni huyo binti' wakamleta pamoja na faili lake! Nikasoma maelezo yaliyoandikwa, nikapiga simu kwa huyo mlalamikaji aje," anasimulia na kuongeza:

"Alipokuja niliwakalisha wote wanieleze tatizo ni nini. Kila mtu alieleza na mwajiri alisema 'huyo binti ni mwizi, ameniibia nguo za mtoto na zake tulipoangalia kwenye lile begi tukakuta nguo mbili na kitenge kimoja.

"Hapo ukiangalia huyo msichana hajalipwa mshahara kwa miezi mitatu, ukilinganisha alichokiiba, hakiwezi kufikia mshahara wake.

"Bahati nzuri yule mama alikuwa na mume wake, kibaya zaidi mume wake ndio alikuja kushtuka palepale kuwa msichana wa kazi hajalipwa, wakati yeye alishatoa fedha zote. Hivyo mjue, kinamama kule nyumbani baba akitoa wao wanazitumia," anaeleza Muhula.

Paulo Magong'ho, ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyabiti, katika Kata ya Buhongwa, jijini Mwanza, anasema mafunzo hayo yamekuwa msaada kwao, hivyo wamejifunza mbinu mbalimbali siyo kwa ajili ya kukabiliana na wafanyakazi hao.

Anafafanua manufaa kufika mbali, hata kwenye kesi nyinginezo, kwa kuwa wao ndio viongozi, pia muhimu kwa jamii, elimu iendelee kutolewa kwa jamii ili itambue kuajiri mtoto chini ya umri elekezi ni kosa.

**NAMNA YA KUTATUA**

Bhoke Leo anatoa darasa la njia mbadala utatuzi wa kesi za wafanyakazi hao, akifafanua alieleza eneo mojawapo ni matumizi ya lugha sahihi na nyepesi katika mjadala.

Anaeleza lingine ni kuwapa wahusika usemaji mkuu na kusiwepo upendeleo, bali hoja ijengwe, huku ukipunguzwa makali ya mgogoro husika na kuonyesha tabia chanya kwa pande zote mbili za mjadala.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi ya Mwaka, 2004, mtoto wa umri chini ya miaka 14 hawastahili kuajiriwa walio na umri chini ya miaka 18 katika maeneo ya migodi, viwanda, kubaharia, kazi za meli au kazi na nyinginezo zinazotambulika kuwa hatarishi.

Sheria inaruhusu ajira kwa watoto wa miaka 14 katika kazi nyepesi pekee, zisizo hatarishi kwa afya ya watoto na maendeleo yao au mahudhurio shuleni, au kwenye mafunzo mengineyo, pia programu za ustawi wao.




Maandamano kudai haki za wafanyakazi wa majumbani. **PICHA: MTANDAO**

UCHUMI

# Waziri Mbarawa: Mradi wa bil. 62.7/- utafungua barabara na anga Kigoma

## •Biashara ndani, nchi jirani kufunguka

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa Kigoma**

MIRADI mikubwa ya Maendeleo iliyokamilika mkoani Kigoma, hivi sasa inatajwa kuwafanya wakazi wa eneo hilo kunufaika kiuchumi kutokana na biashara mbalimbali ambazo wakazi hao wanatarajiwa kuzifanya.

Mojawapo ni ujenzi wa Barabara ya Kidahwe - Kasulu, yenye urefu wa kilomita 63 kwa kiwango cha lami, ambayo imekamilika, sasa inasubiri kuzinduliwa, kwani ilishakabidhiwa serikalini tangu mwaka 2020 kwa ajili ya matazamio.

Pia, kuna mradi wa ujenzi barabara ya Kibondo - Nyakanazi kilomita 50 kwa kiwango cha lami, nayo imeshakamilika, jambo linalotajwa kuwa suluhisho la wakazi wa eneo hilo, sasa ikijenga sura ya kuifanya Kigoma izidi kuinuka kiuchumi, kwa sababu wakazi wake watafanikiwa kibiashara nje na ndani ya mkoa.



Sehemu ya ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kibondo, mkoani Kigoma. Picha ya chini, Waziri Profesa Makame Mbarawa, akikagua barabara mkoani humo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, anaiambia Nipashe katika mazungumzo maalum kwamba, kazi nyingine za pembeni zimekamilika kwa asilimia 98 na kulikobaki ni sehemu chache, ambazo nazo zipo katika sura ya kukamilika, hata kuufanya mkoa huo kuimarika kiuchumi.

Anafafanua kuwa, taarifa ya utekelezaji miradi mikubwa ya maendeleo ya mkoa Kigoma hadi Agosti mwaka huu, inaonyesha ujenzi wa barabara sehemu ya Uvinza- Malagarasi ni kilomita 51.1 kwa kiwango cha lami.

Waziri Mbarawa anafafanua kwamba, kukamilika barabara hiyo, kutawasaidia kwa kiasi kikubwa wakazi wa mkoa, hususan eneo hilo la Uvinza, kufanya kazi zao vizuri bila kikwazo chochote.

"Tunakwenda kuubadilisha mkoa wa Kigoma kutokana na barabara za viwango vya lami zinazojengwa," anasema Profesa Mbarawa, akifafanua kwamba, wameamua kufanya hivyo katika mkoa wao, ikizingatiwa uko mpakani na nchi jirani kama Burundi na Rwanda, hivyo barabara bora ni msaada mkubwa katika kukuza biashara baina yao.

### MAENDELEO YA MRADI

Profesa Mbarawa anasema, ujenzi huo unatokana na ufadhili wa mradi wa 'Opec Fund +Abudhabi Fund +GOT Fund' wenye thamani ya Sh. bilioni 62.7 na kuchukua miezi 24, kukitarajiwa mnamo Septemba mwaka ujao utakamilika.

Waziri pia anataja miradi iliyoko katika matarajio, kwamba ni ya Kazilambwa (Tabora) hadi Chagu (Kigoma) yenye urefu wa kilomita 36, pamoja na barabara nyingine nyingi ambazo zinajengwa ndani ya mkoa huo ambazo zote kwa pamoja zinalenga kuinua mkoa wa Kigoma zaidi katika suala zima la kiuchumi.

Waziri Mbarawa anasema mradi wa ujenzi wa barabara ya Buhigwe-Nyamaguli-Muyama-Katundu kwa kiwango cha lami kilomita 120, inajengwa kwa gharama ya Sh bilioni 726.

Anafafanua kwamba, katika hilo serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa katika kila mkoa, wananchi wanapata barabara zenye viwango na ubora unaotakiwa ili kufanikisha majukumu yao ya kila siku kirahisi.

Kuhusu taarifa za upanuzi wa barabara na viwanja vya ndege, anasema serikali inatarajia kufanya upanuzi wa barabara za kuruka na kutua ndege, katika Uwanja wa Kigoma kutoka urefu wa mita 1,800 uliopo sasa, hadi kufikia mita 3,000 zitakazowezesha ndege kubwa kama vile Dreamerliner, Bombardier na Boeing kutua bila changamoto yoyote.

Anasema serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), imeendelea kufanya upembuzi yakinifu, kwa ajili ya kufanya upanuzi, ili kuhakikisha wanazidi kuuboresha mkoa wa Kigoma.

Anasema serikali ilitangaza zabuni kumpata mhandisi mshauri, ili afanye upembuzi yakinifu , kutaka kuinua mkoa huo kiuchumi kupitia sekta ya anga.

### BODI WAHANDISI

Bodi ya Uhandisi, nayo inasema inaendelea kutathimini viwango vya wahandisi wanaotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo mkoani Kigoma.

Mhandisi Bernard Kavishe, anasema wataendelea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanatekeleza miradi mbalimbali wanayokabidhiwa na serikali kutimiza malengo iliyojiwekea.

Anataja wamejipanga mwaka huu wa fedha, kuhakikisha miradi yote waliyokabidhiwa, inatekelezwa kwa kiasi kilichopangwa na kuelekezwa.

### KATIBU MKUU UJENZI

Mhandisi Aisha Amour, anasema wizara hiyo itaendelea kusimamia suala zima la utendaji kazi wenye weledi ambao utalipeleka taifa mbele katika sekta ya ujenzi wa miundombinu.

Amour anasema,wizara hiyo inawajibika kuangalia viwango vya wahandisi nchini visimame katika ubora, hata akienda katika nchi nyingine basi aweze kufanya kazi pasipo matatizo yoyote.



### WAKAZI KIGOMA

Kauli ya awali ni kwamba, wanaishukuru serikali kwa kuwakumbuka katika suala zima la miundombinu ya barabara, itakayowawezesha kufanya vizuri kwa mustakabali wote wa uchumi.

Mkazi, Julieth Malisa, anasema kutengenezwa miundombinu ya barabara ndani ya mkoa huo, una maana ya kuwasaidia wakazi wa maeneo mbalimbali kujiimarisha kwa majukumu yao ya ujenzi kitaifa.

Lingine anataja kwamba, litawasaidia wananchi wa mkoa huo na jirani, kufanya biashara zao kirahisi, kutokana na kuimarishwa miundombinu hususani katika barabara za ndani kimkoa na nje ya mkoa, kitendo kitakachowarahisishia nyendo zao wafanyabiashara mkoani humo.

Naye Erick Jackson, mkazi wa Uvinza, Kigoma anaishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wake, husussan katika suala la uboreshaji miundombinu mbalimbali ndani ya mkoa, akisema awali barabara hizo hazikuwa katika hali nzuri.

Anasema, hivi sasa biashara na huduma nyingine katika mkoa huo zitapatikana kwa urahisi kwa sababu barabara za kiwango cha lami ndiyo ambazo zitatumika kwa ajili ya usafiri wa ndani na nje ya mkoa huo, pale wanapohitaji kwenda kufanya matumizi mbalimbali ya kijamii.

Jackson anaeleza kwamba, barabara hizo zitawasaidia kwa kiasi kikubwa wakazi wa Kigoma, kupiga hatua katika maendeleo kutokana na miundombinu

rafiki ya barabara inayowawezesha kufanya biashara na wananchi watapata urahisi wa kusafiri kati ya sehemu moja na nyingine.

Itakumbukwa ni moja ya miradi iliyoufungua mkoa wa Kigoma na inafanana na kinachoendelea sasa, ilikuwa wastani wa miongo mwili iliyopita, katika miundombinu ya barabara, kuunganisha na jirami zake.

BIASHARA

# Ruzuku ya serikali ya bil. 100/- ilivyoleta nafuu bei za mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

MAFUTA ni nishati muhimu kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu. Umuhimu huo unatokana na ukweli kwamba shughuli mbalimbali ziwe za kiuchumi au za kijamii, zikiwamo afya, elimu na uzalishaji viwandani, zinahitaji nishati hiyo.

Kukosekana kwa nishati hiyo, yaani petroli na dizeli, kwa kiasi kikubwa kunasababisha shughuli mbalimbali kuathirika na hata kufanya uchumi kuyumba. Mitambo mingi ya viwanda hutegemea mafuta ya dizeli kwa ajili ya uendeshaji na hata sehemu kubwa ya mitambo ya umeme, hutegemea mafuta ili kuwezesha usambazaji wa nishati hiyo katika maeneo mbalimbali.

Kwa mantiki hiyo, bidhaa za petroli ni kiungo muhimu katika kuwezesha shughuli mbalimbali kufanyika kwa ufanisi. Hata vyombo vya moto kama magari, meli na treni hutegemea mafuta ndiyo maana yanapokosekana au bei yake kupanda kutokana na sababu mbalimbali, huwafanya watu kupata taharuki na mambo kadhaa kusimama.

Tangu kuanza kwa mwaka huu bei za mafuta zimekuwa zikipanda na kushuka lakini kwa kiasi kikubwa zilipanda na kusababisha vilio na maumivu kwa watumiaji wa nishati hiyo katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kupanda huko na kushuka kwa mafuta, kumekuwa kukionekana kila mwezi wakati Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ikitangaza bei mpya.

Kupanda au kushuka kwa bei hizo hutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mwenendo wa soko la dunia, gharama za usafirishaji na umbali kutoka bandari ambazo mafuta hushushiwa.

### JANUARI NJEMA

Mwaka huu, kwa mfano, Watanzania walianza na neema baada ya bei za mafuta kushuka kulinganisha na zile zilizotangazwa Desemba mwaka jana.

Katika bei zilizoanza kutumika Januari 5, mwaka huu, EWURA ilitangaza kwamba bei za rejareja na jumla za bidhaa za mafuta ya petroli na dizeli yaliyopokewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam, zilipungua kulinganisha na bei za Desemba kwa Sh. tisa kwa petroli sawa na asilimia 0.35 na dizeli kwa Sh. 67 kwa lita (asilimia 2.80). Hata hivyo, bei ya rejareja kwa mafuta ya taa iliongezeka kwa Sh. 99 kwa lita ambayo ni sawa na asilimia 4.44

Kwa upande wa bei za jumla, kwa petroli, zilipungua kwa Sh. 8.82 kwa lita (asilimia 0.37) na kwa dizeli Sh. 66.71 kwa kipimo hicho hicho sawa na asilimia 2.95, mafuta ya taa yaliongezeka kwa Sh. 99.04 kwa lita ambayo ni sawa na asilimia 4.70.

Kushuka kwa bei hiyo ya mafuta pia kuliinufaisha mikoa ya kaskazini - Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Katika mikoa hiyo bei za rejareja zilipungua kwa Sh. nne kwa lita ya petroli (asilimia 0.17) na Sh. 44 kwa lita ya dizeli ambayo ni asilimia 1.80.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa mikoa inayopata nishati hiyo kupitia bandari za Tanga na Dar es Salaam, hali ilikuwa tofauti kwa mikoa ya kusini inayopokea mafuta kupitia bandari ya Mtwara. Katika mikoa hiyo ambayo ni Lindi, Mtwara na Ruvuma, bei ya petroli ilipungua kwa Sh. 35 sawa na asilimia 1.38 wakati dizeli iliongezeka kwa Sh. mbili (asilimia 0.07).

Kutokana na mabadiliko hayo ya bei, bei ya lita moja katika mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa Sh. 2,501 kwa petroli na dizeli Sh. 2,325 kwa lita wakati Arusha ilikuwa Sh. 2,277 kwa petroli na Sh. 2,426 kwa kipimo hicho hicho.

Kwa Dodoma bei ilikuwa Sh. 2,560 na 2,384 kwa petroli na dizeli mtawalia huku Geita ikiwa Sh. 2,667 (petroli) na Sh. 2,490 kwa dizeli. Kwa Bukoba, bei ilikuwa Sh. 2,717 na Sh. 2,541 kwa petroli na dizeli. Bei hizo zilikuwa kwa rejareja ambazo watumiaji wa kawaida, ambao ni wengi, wamekuwa wakitumia kwa ajili ya kuweka kwenye magari yao au kuendesha mitambo katika viwanda.

Kwa mwezi wa Februari, bei za petroli na mafuta ya taa zilipungua kwa Sh. 21 sawa na asilimia 0.83 na Sh. 44 kwa lita (asilimia 1.90) mtawalia wakati bei ya rejareja ya dizeli iliongezeka kwa Sh. 13 kwa lita sawa na asilimia 0.57.

Vilevile, bei za jumla ya petroli na mafuta ya taa ilipungua kwa Sh. 21.00 ambayo ni asilimia 0.89 na Sh. 43.80 kwa lita sawa na asilimia 1.99 huku bei ya jumla ya dizeli ikipanda kwa Sh. 13.20 kwa lita ( asilimia 0.60). Kwa mikoa inayotumia bandari ya Tanga, yaani Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara, bei za rejareja za petroli na dizeli zilipungua kwa Sh. 123 Sh. 92 kwa lita.






### MACHI JUU

Hali ya kupanda kwa bei za mafuta ilianza kujitokeza Machi baada ya bei ya rejareja ya petroli kupanda kwa Sh. 60 kwa lita na Sh. 65 kwa dizeli huku mafuta ya taa yakiwa Sh. 83 kwa lita ikiwa imepungua kwa asilimia 3.63 kulinganisha na mwezi uliopita.

Katika mikoa ya kaskazini, bei za rejareja kwa mafuta ya petroli na dizeli ziliongezeka kwa Sh. 165 (asilimia 6.88) na Sh. 207 (asilimia 9.09), mtawalia kwa kipimo cha lita. Bei za jumla za petroli na dizeli ziliongezeka kwa Sh. 164.76 (asilimia 7.26) na Sh. 206.62 (sawa na asilimia 9.62) kwa lita.

Bei za mafuta ziliendelea kupanda kwa Aprili hivyo kuongeza makali kwa watumiaji. Katika mafuta yanayopitia bandari ya Dar es Salaam, bei za rejareja za petroli, dizeli na mafuta ya taa ziliongezeka kwa Sh. 321, Sh. 289 na Sh. 473 kwa lita kulinganisha na mwezi uliopita.

Aidha, bei za rejareja kwa mafuta ya petroli na dizeli kwa mikoa ya Kaskazini, ziliongezeka Sh. 285 (asilimia 11.12) na Sh. 295 kwa lita sawa na asilimia 11.90, huku bei za jumla za petroli na dizeli zikiongezeka Sh. 284.22 (asilimia 11.68) na Sh. 294.66 (asilimia 12.52) kwa lita. Ongezeko la bei za mafuta liliendelea kutikisa Mei, mwaka huu. Kwa mujibu wa EWURA ongezeko hilo lilitokana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia, hivyo kuchangia kwa takribani asilimia 93 ya bei hizo kuongezeka na gharama za uagizaji (premium) ambazo zilichangia takribani asilimia nne.

Kutokana na ongezeko hilo, bei rejareja za petroli zilipanda hadi kufikia Sh. 3,148 kwa lita kwa Dar es Salaam, Sh. 3,161 kwa Tanga na Sh. 3,177 kwa lita kwa Mtwara na dizeli zikawa Sh. 3,258 kwa Dar es Salaam, Sh. 3,264 kwa Tanga na Sh. 3,309 kwa lita kwa Mtwara.

### HATUA ZA SERIKALI

Ongezeko la bei za mafuta ambalo lilionekana ni mzigo mkubwa kwa wananchi, lilisababisha serikali kuchukua hatua kwa kutoa ruzuku ya Sh. bilioni 100 kwa mwezi ili kupunguza makali hayo.

Iwapo hatua hiyo isingechukuliwa bei za mafuta kwa Juni, 2022 kwa Dar es Salaam bei za petroli na dizeli zingekuwa Sh. 3,301 na 3,452 wakati Tanga zingekuwa 3,137 kwa petroli na Sh. 3,639 ikiwa ni dizeli na Mtwara zingekuwa Sh. 3,262 na Sh. 3,652 kwa petroli na dizeli, mtawalia.

Baada ya kuwekwa ruzuku hiyo, bei za petroli na dizeli zilibadilika na kuwa Sh. 2,994 na 3,131 kwa Dar es Salaam, Sh. 2,985 na 3,162 kwa Tanga na Sh. 2,979 na 3,165 kwa Mtwara.

Serikali iliendelea kuweka ruzuku kwa mwezi Julai hivyo kufanya bei kwa Dar es Salaam kuwa Sh. 3,220 na 3,143; Tanga Sh. 3,412 na Sh. 3,150 na Mtwara Sh. 3,204 na Sh. 3,172.

Kama ruzuku isingetolewa ili kupunguza makali, bei zingekuwa Dar es Salaam Sh. 3,497 na 3,510 kwa petroli na dizeli, Tanga Sh. 3,486 na Sh. 3,527 na Mtwara Sh. 3,504 na Sh. 3,624.

Ruzuku hiyo ilipunguza bei hizo kwa kati ya Sh. 272 na 299 kwa petroli na Sh. 367 na 452 kwa dizeli. Ruzuku ilielekezwa kwa kiasi kikubwa katika mafuta ya dizeli ili kudhibiti mfumuko wa bei kwa sababu hutumika kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kiuchumi zikiwamo usafirishaji na viwandani.

### AGOSTI YAPANDA

Katika mwezi Agosti, mafuta yalipanda kidogo kulinganisha na Julai, mwaka huu licha ya kuwekwa ruzuku ya serikali ya Sh. bilioni 100 kutokana na kupanda kwa mafuta katika soko la dunia.

"Bei ya mafuta katika soko la dunia imeendelea kupanda na bei ya mafuta katika soko la ndani kupanda vilevile. Lakini katika kupunguza kupanda kwa bei hizo, serikali imetoa ruzuku ya Sh. bilioni 100 kupunguza makali ya bei hizo," imesema taarifa ya EWURA.

Kutokana na hali hiyo, bei ilipanda na kuwa Sh. 3,410 kwa lita moja ya petroli na Sh. 3,322 kwa dizeli huku mafuta ya taa yakifika Sh. 3,765. Katika mkoa wa Tanga, bei ilikuwa Sh. 3,435 kwa lita ya petroli na Sh. 3,349 kwa huku Mtwara ikiwa Sh. 3,393 kwa petroli na dizeli Sh. 3,351.

Maumivu yalikuwa makali zaidi kwa mkoa wa Kagera hasa wilaya ya Bukoba ambako lita moja ya petroli iliuzwa kwa Sh. 3,625 na dizeli Sh. 3,950 huku mafuta ya taa yakiwa Sh. 3,981.

Iwapo ruzuku hiyo isingetolewa, lita ya petroli ingeuzwa Sh. 3,630, dizeli Sh. 3,734 na mafuta ya taa Sh. 3,765 jijini Dar es Salaam wakati Bukoba ingekuwa Sh. 3,845 kwa petroli na Sh. 3,950 kwa dizeli.

### SEPTEMBA, OKTOBA BEI CHINI

Kwa Septemba, bei za mafuta zilishuka kulinganisha na Agosti sababu kubwa ikiwa ni kupungua kwa bei katika soko la dunia. Hatua hiyo ilifanya kupungua kwa bei za mafuta katika soko la ndani kwa jumla na rejareja kati ya Sh. 271 na Sh. 362 kwa petroli Sh. 430 kwa lita kwa mafuta ya taa.

Kutokana na kushuka huko pamoja na ruzuku, bei za rejereja kwa Dar es Salaam zilikuwa Sh. 2,969 kwa petroli na Sh. 3,125 dizeli wakati Tanga zilikuwa Sh. 3,033 petroli na Sh. 3,131 kwa dizeli. Mtwara zilikuwa Sh. 3,083 petroli na Sh. 3,213 dizeli. Ruzuku ilipunguza bei za bidhaa hizo kwa kati ya Sh. 40 na 80 petroli na Sh. 205 na 234 kwa dizeli.

Bei kwa Oktoba zilizotangazwa wiki hii, zilibainisha gharama za uagizaji wa mafuta ziliongezeka kwa kati ya asilimia 50 na 163 kwa kutegemea bandari na bidhaa husika ikilinganishwa na Septemba, hivyo kuathiri mwenendo wa bei za mafuta nchini.

Hata hivyo, kutokana na serikali kuendelea kupunguza madhara ya ongezeko la bei za mafuta nchini kwa wananchi na uchumi kwa ujumla, ilitoa ruzuku ya Sh. bilioni 59.58.

Bei za mafuta zinazotumika sasa zimeshuka kulinganisha na mwezi uliopita ambapo kwa Dar es Salaam petroli kwa lita inauzwa Sh. 2,886 wakati dizeli ikiwa Sh. 3,083. Katika mkoa wa Tanga, bei ya petroli ni Sh. 2,024 na dizeli Sh. 3,108 wakati Mtwara ni Sh. 2,908 na Sh. 3,099. Ruzuku hiyo imepunguza kwa kati ya Sh. 118 na Sh. 204 kwa petroli na Sh. 275 na 360 kwa lita ya dizeli.

Kwa kiasi kikubwa, ruzuku iliyotolewa na serikali imesababisha kuwapo kwa ahueni kubwa ya bei za mafuta kwa wananchi, vinginevyo hali ingekuwa mbaya, hivyo kusababisha athari kubwa kiuchumi na kijamii.



TAFAKURI YA MLALAHOI

## Uwakilishi wa wazee bungeni sawa,lakini...!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

WATANZANIA kama kawaida yao, ni wepesi kuunga mkono jambo na hata kujiapiza kulitekeleza kwa asilimia 120; na hayo hufanyika kwenye mikusanyiko ya hadhara au hata ya ndani, ili mradi kuna macho ya wengi.

Si mara moja si mara mbili au tatu, kusikia Watanzania hao wakijiapiza kuenzi wazee na kuwapangia mipango kedekede ya kuwasaidia na kuwahudumia katika maisha yao ya baadaye ya kuelekea mwisho wa kuishi kwao duniani.

Mipango mingi imekuwa ikipangwa kwa ajili ya wazee hao, na mara nyingi katika siku ambayo inaweza kupachikwa jina la Siku ya Wazee ili kuonyesha umakini, hapo ndipo ahadi kemkem hutolewa na ikiwezekana zikifuatana na zawadi kwa wazee.

Kiongozi akutanapo na wazee siku fulani, ndipo hujitoa kimasomaso na kuwapigia magoti, kuonyesha heshima ya hali ya juu na kuwatia moyo wa kuwasaidia katika mambo haya na yale, ili mradi kuhakikisha kuwa maisha yanakuwa mazuri.

Lakini,mara nyingi kama si zote, baada ya mikusanyiko, kila mzee akitawanyika kwenda kwake na kiongozi kwake, mambo huishia mlangoni na maisha kuwa yale yale na hata maapizo yaliyotolewa ya kuwasaidia nayo hupeperushwa na upepo wa nje ya ukumbi au uwanja.

Nani ambaye hajasikia wazee nchi hii wakililia pensheni zao na haki hizi na zile ambazo ni stahiki zao? Nani hajasikia wazee waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya zamani wakililia haki zao zilizofia tumboni mwa jumuiya hiyo?

Wazee wetu hawakosekani kwenye viambaza na mabenchi ya ofisi za mifuko ya hifadhi ya jamii, wakifuatilia haki na stahiki zao baada ya utumishi uliotukuka, wazee hao hawakosekani katika viambaza mabenchi ya hospitali na zahanati wakiteteme-ka kwa homa, bila msaada.

Ndio hao hao, utawasikia katika baadhi ya mikoa wakiuawa kwa eti kosa la kuwa na macho mekundu yanayohusishwa na ushirikina! Tena bila kufanya utafiti baadhi ya wenzetu huamua kujichukulia sheria mikononi kukatiza maisha ya wazee hao ambao ni wa damu yao, kisa imani za kishirikina!

Vituo vya kuwalea vimejengwa, lakini havina huduma zinazoahidiwa na wanaovijenga na kuvisimamia, na hivyo wazee badala ya kujiona wameokoka na madhila mengine ya upweke katika jamii, lakini kumbe wanaangukia kwenye lindi la majuto.

Yote haya, yanafanyika huku kukiwa na wizara, idara, vitengo na taasisi zenye dhima ya kuhakikisha wazee wanapata wanachostahili kupata, kwa kuwa tu na umri walio nao na kuzingatia mchango wao katika jamii waliyomo.

Wanaofanya haya ya kukengeuka wazee ni ama watoto au wajukuu, vitukuu na hata vilembwe wanaojisahaulisha kuwa bila watangulizi hawa, wao wasingekuwapo na hata kupata nafasi wanazotambia na kuwaona wazee "wana weweseka na muda wao umepita!"

Wazee wetu hawa wameendelea kuvumilia na hatimaye kuchoka ahadi na viapo vya kuwasaidia na sasa kupitia Baraza la Wazee la CHADEMA (BAZECHA), wanasema sasa wanataka uwakilishi bungeni, ili waliyonayo yasikike na kufanyiwa kazi.

Ukiona hivi ina maana yamewafika shingoni na hawana kwingine kwa kusemea, hivyo pengine wakiwa na mzee mmoja wao bungeni, yatasikika na kuchukuliwa hatua na kuwapa afueni ya kimaisha na kumalizia maisha yao duniani wakiwa na unafuu fulani.

Lakini cha kujiuliza, hivi wakimpata huyo mwakilishi, kweli mambo yao yatakuwa mazuri kama wanavyotarajia? Kwani, humo bungeni hapana wazee wanaoweza kuwasaidia kama nia ni kuwa na mwakilishi bungeni? Mbona wamo wazee wengi tu?

Inapaswa kujulikana kwamba yawezekana kweli wakampata mtu huyo na wakamwamini, lakini akifika bungeni atajikuta anabadilika na kuchumia tumbo zaidi, kama tunavyoona baadhi ya wawakilishi wa wananchi wanavyofanya.

Tukumbuke hadithi ya mtu aliyetumwa nchi za mbali kwenda kuwatafutia chakula ndugu zake waliosalia wakifa njaa na matokeo yake alipofika huko akapewa chakula, akala na akasahau kurudi kwao na chakula na matokeo yake...! Alamsiki!

BIASHARA

## JICHO LA JIJINI MWANZA

# Huu hapa mzizi daladala kukatisha 'ruti' na hoja ya Latra ilikosimamia

**Na Anthony Gervas, MWANZA**



Daladala zikiendelea na kazi jijini Mwanza. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU.**

MAGARI madogo ya usafirishaji abiria maarufu kama daladala, ni muhimu katika huduma za usafiri wa kila siku kwa wananchi mijini,ambao asilimia kubwa wana maisha ya kawaida.

Ni usafiri unaobeba nafasi kubwa ya usafirishaji na kufanya wananchi kupata urahisi wa kusafiri kwa gharama nafuu kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya mkoa au nje ya jiji la Mwanza na ndivyo ilivyo kitaifa, katika shughuli mbalimbali kiuchumi na maendeleo.

Wananchi wengi vipato vyao ni vya kawaida, hivyo hutegemea huduma hiyo ya daladala kila siku, ambayo hupunguza makali ya gharama kubwa za maisha kila siku.

Jijini Mwanza, daladala nyingi zinazofanya safari zake za njia ndefu, kama vile kutoka Nyashishi kwenda Kisesa,kutoka Uwanja wa Ndege hadi Nyashishi na Bwiru hadi Kisesa.

Inaelezwa, asilimia kubwa huduma hiyo inakuwa kero kwa abiria, kutokana na kuwa zinakatisha ruti kufika mwisho wa vituo vilivyopangwa katika mamlaka za serikali.

Hali hiyo dereva, kondakta husababisha kuibua migogoro,maneno ya kuwakashfu abiria wao,ambao kimsingi wanatakiwa wawafikishe kituo husika kwa kufuata sheria,kanuni za leseni zilizowekwa na mamlaka ya udhibiti wa usafiri ardhini (Latra).

MADEREVA NA MAKONDAKTA

Aman Masalu, ni dereva wa daladala aina ya Toyota Hiace linalofanya safari njia ndefu kutoka Bwiru hadi Kisesa, anaeleza sababu mojawapo ya kukatisha safari kufika mwisho wa vituo, ni maslahi kuwa kidogo wanayopata kila siku.

Masalu anasema, wanalazimika kugeuza gari njiani kabla ya kufika mwisho na hapo ndiyo tafurani inapoanzia dhidi yao  na abiria, lakini lengo lao na kondakta ni kuokoa mafuta yasitumike mengi kwenye gari.

Anasema mara nyingi wamekosa abiria au kubaki wachache ndani ya gari wakati wakiwa bado wanaendelea na safari kwenda kituo cha mwisho, pia posho wanazolipwa na matajiri wao au mishahara havitoshelezi kumudu hali ya maisha.

Mfano hai ni kwamba, mtu huyo anaweza kuwa analipwa mshahara mathalan shilingi 100,000 kwa mwezi ikiwa ni kiasi kidogo, kulinganishwa na gharama za maisha ya kila siku, lakini asilimia kubwa wengi ni vibarua wa kulipwa kutwa hawana mishahara.

Anaeleza, hata akikamatwa na askari wa usalama barabarani (polisi Trafiki) faini hulazimika kulipa pesa za makusanyo katika hali inayovuruga 'hesabu za tajiri' jioni wakati wa kwenda kukabidhi, wanakatwa posho zao na kondakta wake au kukosa kabisa chochote.

Ibrahim Hussein, ni dereva wa gari la daladala aina ya Costa, linalofanya safari za njia ndefu kutoka Nyashishi hadi Kisesa, umbali wa kilomita 35 kutoka kituo cha kwanza hadi mwisho.

Anataja changamoto inayosababisha kile ambacho ni 'kuchora' yaani kukatisha safari, inatokana na abiria kubaki wachache  kabla ya kuwafikisha wanakokwenda.

Hivyo, wanalazimika 'kuwafaulisha' wateja wao katika gari jingine linaloelekea kule, ili wao waweze kuokoa gharama kubwa ya kutumia mafuta mengi bila faida, ingawa nauli ya kutoka mwanzo wa kituo hadi mwisho ni shilingi 1,000.

Ibrahim anafafanua kwamba, wanapofika stendi kuu mpya ya mabasi akielekea Kisesa, anakuwa amebakiza pengine kilomita takribani 11 kufika kituo cha mwisho, inabidi kugeuza ruti kurudi alikotoka, ili kuokoa mafuta ya gari lake na abiria kuwatafutia usafiri mwingine.

“Madereva wengi na makondakta hawana mikataba ya ajira,mfano mimi nalipwa mshahara wa shilingi 150,000 kwa mwezi, badala ya shilingi 200,000, lakini kwa siku ikifika jioni tunatakiwa kupeleka shilingi 80,000 kwa tajiri ambazo ni makusanyo ya gari,anasema.

Anaeleza kwamba pesa hizo zinapopungua,anakatwa kwenye mshahara wake, kwa sababu ndiye aliyekabidhiwa gari hilo kusimamia.

Pia, inatajwa anapotokea amekamatwa na askari wa usalama barabarani kwa makosa ya uzembe, hulipa faini pesa zake za mfukoni siyo za tajiri, katika hilo anakuwa hana ujanja wa kumudu kuendesha maisha ya kila siku na familia yake.

Kondakta wa gari hilo, Bilal Bilal, naye anasimulia yake kwamba suala la kukatishwa kwa safari ya daladala, isiyofika kwenye kituo husika, ni kutokana na shida ya uchache wa wateja, hali inayobidi kutumia njia ya kuwapandisha lingine ila wanapogoma kushuka wanalazimika kuwapeleka kwa mujibu wa sheria.

Bilal anasema, hawezi kutumia lugha chafu kuwatukana wateja wao bila maelewano, au kuwashusha kwa nguvu wakati kufika wanakokwenda ni haki yao,anatambua ni kosa kufanya vile kisheria.

**KAULI YA LATRA.**

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini Mkoa wa Mwanza,(LATRA) Halima Lutavi, anaeleza kwamba suala la kukatisha 'ruti' madereva wa daladala ni ukiukaji sheria  za leseni ya usafirishaji wa abiria.



Mandhari ya barabara za Mwanza.

Halima anataja changamoto nyingi zinazoripotiwa kwenye mamlaka hiyo, ikijumuisha madereva na makondakta kushindwa kufuata taratibu na kanuni za leseni za usafirishaji huo, katika magari yao, jambo lililo kinyume cha sheria.

Anasema Latra, imeshajipanga kwa kushirikiana na Polisi jijini Mwanza, kuhakikisha kunakuwepo mkakati kabambe wa kuwakamata wanaokiuka sheria za leseni na usalama barabarani.

Adhabu za ukikajki huo, kwa mujibu wa kiongozi huyo wa Latra, ni faini ya shilingi 100,000.

Kuhusu kupanda nauli mwaka huu za daladala, anasema kunachangiwa na mambo mengi, ikiwamo kupanda bei mafuta ya petroli, dizeli, vipuri vya magari, akitoa mfano wa tairi, ambazo bei huongezeka kwa shinikizo la soko la dunia.

”Kiuchumi, mpango wa upandaji nauli unatakiwa kuchukua muda mrefu,mfano bei ya nauli iliyokuwepo awali, ilipanda tangu mwaka 2013 hadi 2022, ndipo imepanda tena hivyo imechukua miaka mingi,” anafafanua.

**WAUZAJI MAFUTA**

Amina Yassin, ni Meneja wa Kituo cha Mafuta Puma kilichopo jijini hapa, anayebainisha kwamba kuanzia mwezi Julai mwaka huu, bei ya mafuta ya petroli ilipanda kutoka shilingi 3,370 kwa lita moja hadi shilingi, 3,560 na hivi sasa yameshuka na kuuzwa shilingi, 3,119 lita moja.

“Vilevile, mafuta ya dizeli bei ya zamani ilikuwa shilingi 3, 293, baadaye ikapanda hadi shilingi,3,472, na sasa yakishuka shilingi 3,276 lita moja,” anasema Amina.

Kushuka gharama hizo za mafuta, kumesaidia wananchi hususani wamiliki wenye magari ya usafirishaji abiria, watu binafsi pia kupungua maumivu ya uendeshaji wa biashara na gharama za maisha.

Anaeleza kuwa, mafuta yanaposhuka gafla bila taarifa za Serikali,kunasababisha hasara kubwa kwenye kampuni husika kwani inaweza kuwa ilinunua mzigo mkubwa,hivyo inalazimika kuuza bei ndogo isiyokuwa na faida.

Hapo anatahadharisha kuwa, kampuni inaweza kuyumba katika uendeshaji wake,akiomba serikali kuweka mpango kazi mzuri  kuhakikisha inakuwa inatoa taarifa muda mrefu, ili wahusika waweze kujiandaa kukabiliana na changamoto hiyo,ikiwemo kununua bidhaa kidogo.

Anaeleza kuwa yanapopanda bei kwao ni furaha tupu, hata wateja huendelea kununua sababu hawana namna kwani hawawezi kuyapaki  magari yao, ingawa hubaki wakilalamika ongezeko hilo.

Aidha, anaeleza kwamba hivi sasa hajui kama mwezi huu yatapanda tena bei,au kushuka zaidi wanasubiri  kuona.

BIASHARA

# Tabasamu la wakulima wa Shinyanga waliokopeshwa trekta walime kibiashara

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

SEKTA ya kilimo ndiyo inayotegemewa kwa kiasi kikubwa na wakazi wa mkoa wa Shinyanga, kwani zaidi ya asilimia 75, wanategemea kilimo kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku na kuwakwamua kiuchumi.

Kilimo kina uhusiano wa moja na sekta zisizo rasmi, na hata zilizo rasmi. Hapo kuna usafishaji kwenda kwenye usindikaji mazao yake, matumizi na soko la ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kutoa malighafi kwa viwanda na soko kwa bidhaa zilizotengenezwa.

Mkoani Shinyanga, marekebisho ya kiuchumi yamesababisha kufunguka sekta hiyo kwa uwekezaji binafsi katika uzalishaji na usindikaji, uagizaji pembejeo za kutoka nchi za nje na usambazaji na masoko ya kilimo na serikali imebaki na kazi ya usimamizi na usaidizi wa umma na dhima ya uwezeshaji.

Mkakati uliopo ni kuendelea kufanya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji kadiri bajeti itakavyoruhusu kwa lengo la kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa mazao yanayozalishwa kama mpunga, choroko, dengu, vitunguu, mtama, mahindi, pamba na uwele.

Aidha mkoa huo una eneo la kilometa za mraba 18,555 sawa na hekta 1,855,500 ambapo hekta 1,220,090 zinafaa kwa kilimo na kina nafasi kubwa katika kuajiri wananchi wengi, upatikanaji wa chakula, mauzo ya mazao ndani na nje ya nchi na malighafi za viwanda.

Kwa kuona umuhimu wa kilimo kwa wananchi, mashirika ya umma na yasiyokuwa ya kiserikali ikiwemo kampuni ya uwezeshaji wa zana za kilimo na viwanda (PASS Leasing), Agricom, Relliance Group na Kanu Equipment yamejitoa kusaidia wakulima kwa kuwapatia zana za kilimo ili kuongeza uzalishaji.



.Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema akizungumza na wakulima wa Kanda ya Ziwa, katika hafla ya kuwakabidhi matrekta 21. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

### NENO LA MKOPESHAJI

Killo Lussewa, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Uwezeshaji wa Zana za Kilimo na Viwanda (PASS Leasing) anasema, wamekuwa na utaratibu wa kuwatembelea wakulima wanaojihusisha na kilimo cha chakula na biashara nchi nzima na kutatua changamoto wanazokutana nazo, ikiwamo kuwakopesha zana za kilimo.

Anasema, wakulima wengi wanatumia zana duni na wanyama kazi kama vile punda na ng'ombe wawapo shambani na kupata mavuno kidogo ikilinganishwa na nguvu wanazotumia inawafanya wao kuwatembelea na kuwakopesha matrekta kwa wale wenye uhitaji na kuongeza uzalishaji.

Lussewa anasema, msimu ujao wanataka kuufanya mkoa wa Shinyanga kuongoza kwa kilimo cha biashara, hususani zao la mpunga na itasaidia kuwa na chakula kingi na viwanda kupata malighafi za kutosha zitokanazo na kilimo kwa wingi hivyo kila mmoja anatakiwa kujitokeza kulima.

### UGAWAJI ZANA

Anasema, wakulima 21 wa mazao mkoani Shinyanga, wamekopeshwa matrekta ya kilimo kila mmoja na yenye thamani ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo na uwezeshaji wa zana hizo umekuwa ukifanyika pasipo kuweka dhamana yoyote.

Anasema Septemba mwaka jana, 2021 walitoa trekta 50 kwa wakulima 50 zenye thamani ya Sh.bilioni tatu, zimekuwa zikitolewa kwa ushirikiano wa kampuni zinazojihusisha na kilimo.

"Tunahitaji nchi yetu iwe kinara kwa mazao ya chakula na biashara ndio maana tunawatembelea wakulima wote kuwasikiliza changamoto zao na kuwakopesha zana za kilimo na mpaka sasa tumeshakwisha kutoa trekta 300 kwa wakulima nchi nzima zenye thamani ya Sh.bilioni 13," anafafanua Lussewa.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Agricom Alex Duffar, anasema, wakulima wengi katika uzalishaji shambani wanatumia wanyamakazi hali inayosababisha kupata mavuno kidogo hivyo matrekta hayo yataongeza uzalishaji ipasavyo na mkulima kuinuka kiuchumi.



Sehemu ya matrekta waliyokopeshwa wakulima .

Hapo anawataka wakulima hao kuhakikisha wanayatumia yaliyopangwa sio vingine kwani yatakapoleta shida yoyote ndani ya miaka miwili wao kuanzia sasa watawajibika kuyarekebisha kwa gharama za kampuni ili mkulima asikwame kuendelea na kilimo.

### RC WA SHINYANGA

Sophia Mjema, ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anasema serikali imetoa shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kata ya Chela Msalala ili kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi mara tatu kwa mwaka na kuwataka maofisa ugani kila kata kujenga desturi ya kuwatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya kulima kisasa.

Anasema, watabiri wa hali ya hewa wanasema mwaka huu wa kilimo kutakuwa na uhaba wa mvua na anawataka wakulima kutunza chakula na wasiuze chote, ili kutakapokuwa na upungufu waweze kutumia na familia zao kwani misimu ya kilimo imekuwa ikitofautiana kulingana na majira yake.

Mjema anasema, mwaka uliopo wa fedha mkoa huo ulipokea Sh.bilioni 190 kwa ajili ya usambazaji wa maji, kilimo cha umwagiliaji na kutunza mazingira, hivyo sehemu zote hususani vijijini ambako kunauhaba wa maji wananchi wake watakwenda kunufaika na fedha hizo.

"Maofisa ugani wetu hakikisheni mnawatembelea wakulima mara kwa mara na kutoa elimu ya kulima kisasa kulingana na hali ya maeneo yao ya kilimo, tunataka msimu ujao tuongoze kwa uzalishaji nchi nzima mazao yote kwa kutumia trekta na kituo cha kilimo Chela cha umwagiliaji, "anasisitiza Mjema.

### DC WA KAHAMA

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga anaahidi kufanyia kazi agizo lililotolewa na atahakikisha wakulima wote hawauzi chakula holela nchi za jirani na amekuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wakulima kuzalisha zaidi mazao ya biashara hasa alizeti, tumbaku na pamba.

Anasema,msimu wa kilimo uliopita wakulima wa pamba walizalisha kilo 800,000 tofauti na kipindi cha nyuma na msimu ujao makisio waliyoweka wanatarajia kuzalisha zaidi ya kilo milioni tano na hii ni baada ya mazingira ya kilimo kuwa rafiki kwa kilimo na wakulima kupata fedha za kutosha.

### WAKULIMA SHINYANGA

Mkulima kutoka halmashauri ya Ushetu, Gemu Doto anasema, zana za kilimo za kisasa cha kutumia trekta walizokopeshwa zitawasaidia kuongeza uzalishaji kwao, hata kufikia malengo waliyonuia.

Anasema, wakati wa kuandaa mashamba, wamekuwa wakitumia zana duni na wanyamakazi na kuzalisha mavuno kidogo kulingana na wanyama hao kuchoka kwa haraka na kwamba sasa wameondokana na adha hiyo baada ya kukopeshwa matrekta ya kilimo.

Mkulima Mawazo Mangu, anaomba utoaji wa zana hizo za kilimo uwe endelevu kwa kuwa wakulima wengi wana uhitaji wa zana za kisasa katika maeneo mengi nchini ikiwa ni pamoja na kutembelewa na maofisa ugani katika kata na kupewa elimu ya kilima kisasa kulingana na jiografia ya maeneo yao ya kilimo.

UCHUMI

# Ni hali mbaya ya njaa, ukame na mparanganyiko hadi vifo Somalia

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya watoto wanaofariki inaongezeka nchini Somalia ikikabiliwa na ukame mbaya zaidi kuwahi kushuhudiwa katika kipindi cha miaka 40.

Maofisa wa serikali wanasema janga kubwa zaidi linaweza kuikumba nchi hiyo ndani ya siku chache au wiki zijazo endapo msaada zaidi hautawasili.

Mwana wa pili wa kiume wa Fatuma, aliyekuwa na umri wa miaka 10- Salat, alifariki kutokana na njaa wiki mbili zilizopita, muda mfupi baada ya familia kufika Baidoa kutoka kijijini kwao, baada ya kutembea umbali wa siku tatu.

"Siwezi kuomboleza kwa ajili ya mwanangu. Hakuna wakati. Ninahitaji kutafuta kazi na chakula ili kuwafanya wengine waendelee kuishi," Fatuma analalama.

Kwa upande mwingine wa barabara ya vumbi inayoelekea Kusini-Mashariki, kuelekea pwani na mji mkuu wa Somalia, Mogadishu, familia nyingine zilizohamishwa zilisimulia hadithi za kuhuzunisha zaidi za safari ndefu katika mazingira yenye ukame wakitafuta chakula.

Utafiti mpya umeonyesha kuwa karibu theluthi mbili ya watoto wadogo na wanawake wajawazito katika kambi hizo wanakabiliwa na utapiamlo mkali, ambao, pamoja



Ilivyo hali mbaya ya Ukame wa Somalia. **PICHA: MTANDAO.**

na kiwango kikubwa cha vifo, unaweza kuashiria kwamba tamko la nyumbani la njaa tayari limechelewa.

Katika wodi ya wagonjwa katika hospitali kuu ya jiji, Dk Abdullahi Yussuf alipita katikati ya vitanda, akiangalia wagonjwa wake wadogo waliodhoofika. Wengi wao walikuwa watoto kati ya miezi miwili na miaka mitatu.

Wote walikuwa na utapiamlo mkali. Wengine walikuwa na homa ya mapafu na wengi walikuwa wakipambana na mlipuko mpya wa surua pia.

Watoto wachanga wachache walikuwa na nguvu za kulia. Kadhaa walikuwa na ngozi iliyoharibika vibaya, iliyovunjwa na uvimbe ambao wakati mwingine huambatana na hali mbaya zaidi za njaa.

"Wengi sana wanakufa kabla hata hawajafika hospitali," alisema Dk Abdullahi, akitazama timu yake ikihangaika kuunganisha mrija wa mishipa kwenye mkono wa mtoto wa miaka miwili anayeomboleza.

Ingawa maofisa wa Somalia na mashirika ya kimataifa yamekuwa yakiangazia kwa miezi kadhaa kuhusu tishio la njaa katika eneo hili la kusini-magharibi, Dk Abdullahi alisema hospitali yake tayari ina upungufu wa vifaa vya msingi ikiwa ni pamoja na virutubisho vya lishe kwa watoto.

"Wakati mwingine tunakosa vifaa. Inatisha, kwa kweli, kwa sababu watu wanakufa, na hatuwezi kuwaunga mkono. Serikali yetu ya mtaa haishughulikii hili vizuri. Haijapanga kukabiliana na ukame au kuwasili kwa familia zilizokimbia makazi," alisema. Alisema, kwa kuchanganyikiwa. Waziri wa serikali za mitaa alikiri kumekuwa na mapungufu.

"Tunahitaji kuwa na kasi zaidi kuliko tulivyo, na tunahitaji kuwa sahihi...na ufanisi zaidi," alisema Nasir Arush, Waziri wa Masuala ya Kibinadamu katika jimbo la Kusini Magharibi, katika ziara fupi katika moja ya kambi karibu na Baidoa. Lakini msaada zaidi wa kimataifa, alisisitiza, ulikuwa muhimu.

"Kama hatutapokea misaada tunayohitaji, maelfu ya watu watakufa. Mambo tunayofanya sasa tulihitaji kufanya miezi mitatu iliyopita.

Alidokeza kuwa wakati wa ukame wa 2011 "nusu ya vifo 260,000 vilitokea kabla ya njaa kutangazwa".

Mjumbe wa rais anayeongoza juhudi za kimataifa za Somalia kupata ufadhili zaidi aliishukuru serikali ya Marekani, hasa, kwa ufadhili mpya wa hivi karibuni, akisema "imetupa matumaini".

Lakini Abdirahman Abdishakur alionya kwamba bila msaada zaidi, mgogoro wa ndani katika sehemu moja ya Somalia unaweza kutoka nje ya udhibiti haraka.

"Tulikuwa tunapaza sauti ... lakini mwitikio wa jumuiya ya kimataifa haukuwa wa kutosha," Abdishakur alisema.

"Njaa inakadiriwa lakini tayari inashuhudiwa katika baadhi ya maeneo nchini Somalia, hata hivyo tunaweza kuzuia janga hilo," aliendelea kusema, akizungumza kwa simu wakati alipokuwa Toronto, Canada.

Ingawa makadirio yanatofautiana, idadi ya wakazi wa Baidoa imeongezeka takribani mara nne katika miezi michache iliyopita, hadi karibu watu 800,000.

Na mgeni yeyote atang'amua ukweli mmoja wa kushangaza: karibu watu wazima wote wanaowasili ni wanawake.

Wanawake wengine walizungumza kuhusu waume na watoto wa kiume wakubwa kuzuiwa kuondoka katika maeneo yanayodhibitiwa na wanamgambo, na kuhusu unyang'anyi wa miaka mingi wa kundi hilo.

Ukame, unaochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa, sasa unatishia kukomesha mtindo wa maisha wa kichungaji ambao umedumu kwa karne nyingi katika Pembe ya Afrika.

Katika wodi ya wagonjwa katika hospitali kuu ya jiji, mtaalamu Dk. Abdullahi Yussuf alipita katikati ya vitanda, akiangalia wagonjwa wake wadogo waliodhoofika. Wengi wao walikuwa watoto kati ya miezi miwili na miaka mitatu.

• ***Na Sabato Kasika, kwa msaada wa mtandao.***

## CHEMSHABONGO NA -00 11 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. nishati ya mitambo
7. kinyume cha maovu
8. eneo wazi
9. jina la kale Afrika mashariki
10. kagua 11.menya
13.baba, mama na wana
14.au 15.sema kwa siri habari isienee 19.mtu mdanganyifu
20.Rabat ni mji mkuu
23.kuwa juu ya maji 25.omba ruhusa ya kuondoka 26.josho
27.pata majeraha 28.Ugwe

Chini:
1. ng'ata
2. fanicha ya kuandikia
3. kijiji alipoonekana Yesu baada ya ufufuko 4. chakula cha Israeli jangwani 5. mambo ya uwongo 6. mtu asiye mwenyeji
8. mji alikozaliwa Kikwete
12.ng'atana 13. ustawi 16.daraja 17.mafuta 18.walau 20.mja
21.maoni 22.safisha mwili
23.kwepa

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | | | | 5 | | 6 | |
| 7 | | | | | 8 | | | | | |
| 9 | | | | | | | | | | |
| | 10 | | | | 11 | 12 | | | | |
|  | | | | 13 | | | | | | |
| | | | | 14 | | | | | | |
| | | | | 15 | | | 16 | 17 | | 18 |
| | | | | 19 | | | | | | |
| 20 | | 21 | 22 | | | | 23 | | 24 | |
| | | 25 | | | | | 26 | | | |
| 27 | | | | | 28 | | | | | |

## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| ANGALIA | GUSA |
| MASHINA | OKOTA |
| SHOKA | MIKASI |
| MLIMA | AWAMU |
| ASANTE | SOKA |
| ASUBUHI | TAUSI |
| ATAMIA | IBARA |
| SOKA | KASHA |
| UKIWA | MKAA |
| GOMA | OKA |
| KAMBA | |
| AFANDE | |
| HAMASA | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | K | A | M | B | A |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | Z | U | N | G | U | M | Z | A | J | I |
| B | | T | | U | | K | | | | D |
| U | K | U | T | A | | U | | M | | H |
| | A | | | | H | U | R | U | M | A |
| M | Z | I | N | G | A | | | M | J | A |
| | E | | | | K | A | M | B | I | |
| S | H | A | N | G | I | L | I | A | | T |
|  | | | | O | M | A | N | I | | A |
| | | | | B | U | S | H | | | M |
| | | | | I | | K | A | M | B | A |
| | | | | | | A | | | | A |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | G | A | | M | A | K | O | S | A |
| G | | F | | L | | A | | H | |
| I | S | R | A | E | L | I | | A | |
| Z | A | I | D | I | | D | A | K | A |
| A | M | K | A | | K | I | M | A | |
| | B | A | A | D | A | | A | | M |
| | A | | | | N | | Z | A | A |
| U | Z | A | O | | Y | | O | | Z |
| | W | | K | I | W | A | N | D | A |
| K | A | A | A | | A | | I | | O |



# Taasisi yatoa msaada wagonjwa 100 Hospitali ya Kanda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAGONJWA 100 wanaopata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na Kitengo cha Wazazi Meta, wamepatiwa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo sabuni na vitunzia taka.

Taasisi ya Twende wote Foundation iliyoko jijini Mbeya ndiyo iliyotoa msaada huo lengo kuu likiwa ni kuwasaidia wagonjwa wanaotoka kwenye mazingira magumu.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Davule Mwambije alisema msaada huo ni kwa ajili ya kuwapa faraja wagonjwa wanaotoka kwenye mazingira magumu wakiwamo kina mama, watoto na wazee.

Katibu wa taasisi hiyo, Elizabeth Kaponela, alisema wamekuwa na utaratibu wa kuwatembelea watu wenye uhitaji.

Alisema watoto hao wanashindwa kupata mahitaji muhimu kutokana na wazazi wao kushindwa kumudu gharama za mahitaji, hivyo akawaomba wadau wengine kuwasaidia watoto hao.

Ofisa Uhusiano kutoka hospitali hiyo, Archad Mosha alisema msaada huo umekuja wakati muafaka na kwamba utasaidia kupunguza uhitaji kwa wagonjwa hospitalini hapo.

**Taasisi ya Twende wote Foundation iliyoko jijini Mbeya ndiyo iliyotoa msaada huo lengo kuu likiwa ni kuwasaidia wagonjwa wanaotoka kwenye mazingira magumu.**

# Ubovu barabara wasababisha wajawazito kujifungua njiani

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

BAADHI ya wanawake wajawazito wa Kijiji cha Mwala kilichopo Kata ya Ilembo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanajifungulia njiani kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara inayosababisha washindwe kufika kwa wakati kwenye vituo vya afya.

Wananchi wa Kijiji hicho waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya iliyofika katika kata hiyo iliyokuwa na lengo la kukagua miradi ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa shule ya wasichana iliyopewa jina la Pareto.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Nalapa Kasule alisema kijiji hicho hakina barabara ya uhakika ambayo inawaunganisha na makao makuu ya kata hiyo ambako kipo kituo cha afya.

Alisema kipindi cha kiangazi barabara inayotumika ina vumbi ambalo linasababisha vyombo vya usafiri hasa pikipiki kushindwa kupita na hivyo kusababisha wajawazito wanaopelekwa kwenye kituo cha afya kushindwa kufika kwa wakati. "Kama mlivyojionea wenyewe barabara yetu ni mbovu sana, kwa sasa kuna vumbi lakini wakati wa masika ndiyo haipitiki kabisa maana huwa na makorongo makubwa, sasa wake zetu wanapata shida sana," alisema Kasule.

Aliiomba Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na vijijini (TARURA), kuwaboreshea miundombinu hiyo ili waweze kusafiri kwa urahisi.

Diwani wa Kata ya Ilembo, Abel Mpyambala alisema endapo barabara hiyo itaboreshwa itwasaidia wananchi wa eneo hilo kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa tija zaidi tofauti na ilivyo sasa hivi.

Alisema wananchi wa eneo hilo wanalima zaidi mahindi na pareto lakini wanashindwa kusafirisha vizuri pembejeo kupeleka shambani na kuyatoa mazao mashambani kwenda nyumbani na sokoni, huku akieleza kuwa wanatumia gharama kubwa kwenye usafirishaji.

Alisema barabara hiyo ni muhimu pia kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa kufika kwenye shule ya sekondari inayojengwa katika kijiji hicho, huku akieleza kuwa endapo barabara hiyo haitaboreshwa kutakuwa na shida shule hiyo kufikika.

Alisema kwenye ujenzi wa shule wananchi wamekuwa wakishirikiana na kampuni ya ununuzi wa pareto pamoja na halmashauri kujenga na kwamba wazo hilo lilianzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Peter Homera aliwapongeza wananchi wa eneo hilo kwa kujitolea kufanya shughuli za maendeleo bila kulazimishwa na kwamba hali hiyo inairahisishia serikali pia kwenye utekelezaji wa shughuli zake.

Alisema atazungumza na Meneja wa TARURA Mkoa wa Mbeya ili wakala huo uboreshe barabara hiyo na kuwarahisishia wananchi kufanya shughuli za maendeleo.

Hivyo, aliwataka viongozi wa serikali wa eneo hilo kuendelea kuwahamasisha wananchi kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule pamoja na zahanati.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akifurahia jambo na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa huo (Viwanda na Biashara), Mwajuma Nyamkomola, wakati wa mkutano wa hadhara na wakazi wa wa Kijiji cha Mwala, Kata ya Ilembo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TAMISEMI kuboresha miundombinu barabara, elimu Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeahidi kuboresha miundombinu ya barabara na elimu katika Jiji la Mbeya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi.

Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha baraza la madiwani wa Jiji hilo baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi ya kutembelea na kukagua miundombinu ya barabara shule za msingi na sekondari.

Prof. Shemdoe alisema kuwa ya Mbeya kuwa Jiji bado lina matatizo mengi ambayo alijionea na kueleza kwamba Serikali imedhamiria kufanya maboresho.

Alisema serikali imeshaanza kutekeleza baadhi ya miradi ndani ya Jiji hilo na kwamba miradi inayojengwa kwa sasa ina thamani ya Sh. bilioni mbili hasa kwenye sekta ya elimu.

Profesa Shemdoe alisema katika kutelekeza hayo Serikali imepanga kutangaza zabuni ya kuboresha barabara, uwanja wa ndege na mifumo ya maji mwishoni mwa Oktoba mwaka huu.

"Baadhi ya miradi ambayo ipo kwenye mipango ni pamoja na ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi na stendi ndogo katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani, upanuzi wa barabara ya Iziwa yenye urefu wa kilomita 5.75, upanuzi wa barabara ya Block T-Makunguru na Juhudi yenye urefu wa kilomita 3.3," alisema Prof Shemdoe.

Vilevile aliitaja miradi mingine kuwa ni upanuzi wa barabara ya Uyole-Itezi yenye urefu wa Kilomita mbili, upanuzi wa barabara ya Airport-Samora-TANESCO-Sae-Kisanji na Kabwe Block T-Sido yenye urefu wa kilomita 3.2.

Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson alisema kuwa Jiji la Mbeya linayo imani na serikali kuwa itasaidia wananchi wa Mbeya kuboresha miundombinu hiyo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma wanazostahili kama ilivyo kwa wananchi wa maeneo mengine.

Hivyo, aliiomba serikali kuharakisha miradi hiyo kwa maelezo kuwa kwa sasa Jiji la Mbeya lina hali mbaya ya miundombinu ambayo haiendani na hadhi yake ya Jiji.





## FAO kuisaidia Tanzania kiwango unywaji maziwa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) limeeleza dhamira yake ya kuisaidia Tanzania katika jitihada endelevu za kuongeza kiwango cha unywaji wa maziwa ili kuboresha hali ya lishe kwa wananchi.

Inapendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mtu mmoja kunywa angalau lita 200 za maziwa kwa mwaka ambapo Tanzania ipo nyuma sana kufikia kiwango kilichopendekezwa, kwa kuwa rekodi zinaonyesha mpaka sasa Mtanzania mmoja anakunywa lita 62 tu za maziwa kwa mwaka.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa wa Chakula na Lishe wa FAO, Stella Kimambo, alisema shirika hilo litaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha unywaji wa maziwa unaongezeka nchini.

"FAO imedhamiria kufanya kazi kwa karibu kwa ushirikiano na mashirika, wachakataji wa maziwa na taasisi mbalimbali ndani ya nchi ili kuongeza upatikanaji wa maziwa pamoja na kuongeza utamaduni wa unywaji wa maziwa nchini," alisema.

Kimambo alisema kuwa FAO pia itajitahidi kuweka jitihada zaidi za kusaidia nchi kuendesha programu endelevu za utoaji wa maziwa kwa kuanzia angalau kwa wanafunzi wa shule za msingi na wenye mahitaji maalumu.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Dk. George Msalya, alisema; "Mwaka jana, tulianza mradi wa majaribio wa utoaji wa huduma za unywaji wa maziwa katika wizara zisizopungua 10, maendeleo ambayo hadi sasa yameshuhudia utoaji wa zaidi ya lita 12,000."

Alisema bodi hiyo inajitahidi kuongeza vituo vya maziwa vilivyotengwa kwa ajili ya zoezi hilo muhimu linaloendelea hadi kufikia angalau vituo 20 kutoka 10 vilivyopo kwa sasa.

# DP yakumbusha kuboreshwa sekta ya kilimo, mifugo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Democratic Party (DP), kimewataka mawaziri wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuboresha sekta hizo ili ziwe na tija kwenye maisha ya watu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Abdul Mluya, alisema; "Tunajua kuwa asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima na wafugaji hivyo serikali kwa kupitia sekta ya kilimo na wafugaji wakae na wadau ili kujua nini changamoto wanazokumbana nazo badala ya kukaa ofisini na kutunga sera."

Alisema kilimo ndiyo uti wa mgongo na serikali inapaswa kuliangalia kwa kina suala hilo kwa sababu linagusa maslahi ya watu wote nchini.

Pia chama hicho kimezindua kampeni yenye kaulimbiu 'Mlete mzalendo twende pamoja kuijenga nchi'.

Alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha wanaimarisha chama kwa kufanya kampeni ya kuzunguka nchi nzima wakinadi sera za chama hicho.

Aliseleza chama hicho kwa sasa kimejipanga kushika dola pamoja na halmashauri wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. "Kwa sasa DP, imekuja na mikakati mingine ya kuhakikisha chama hicho kinazunguka nchi nzima kwa ajili ya kunadi sera za chama nchi nzima kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi juu ya kazi ambazo zinafanywa na chama hicho."

"DP itahakikisha inatoa elimu kwa viongozi wote wa chama hicho kwa ngazi zote kwa nia ya kuwafundisha namna ya kufanya siasa zenye tija ambazo zinalenga kuking'oa chama kikongwe cha CCM," alisema Mluya.

Alisema malengo makubwa ya chama ni kuhakikisha kinafanya ziara za kisiasa kwa kuwafikia Watanzania wote kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

"Pamoja na kuwapo zuio la kufanya siasa, lakini DP tutafanya siasa kwa nguvu zote ambapo itafanyika mikutano ya ndani na mikutano ya hadhara bila kuwapo kwa aina yoyote ya uvunjifu wa amani ya nchi," alisema.

Aliwataka waratibu wote kuhakikisha wanawatembelea watu ili kuwaelimisha namna siasa isiyokuwa na machafuko inavyofanywa.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kulia), akijadiliana jambo na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Abdi Kagomba (katikati), wakati wa kikao kazi baina ya kitengo cha mabaraza ya ardhi na nyumba na wilaya jijini Dodoma jana. Kushoto ni Wakili Msomi, Ally Nkangaa. **PICHA: WANMM**

# Wauguzi watakiwa weledi wanapohudumia wagonjwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imewataka wauguzi na wakunga nchini kufanya kazi zao kwa uadilifu, ufanisi na weledi wanapo wahudumia wagonjwa kwenye maeneo yao ya kazi.

Pia imewataka kufanya kazi zao kwa kutanguliza upendo kwa kuzingatia maadili ya kazi wanapohudumia wagonjwa na jamii.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menegimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA), uliofanyika jijini hapo.

Ndumbaro, katika mkutano huo mkuu wa 49 wa TANNA alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema wauguzi na wakunga kwenye maeneo yao ya kazi wanatakiwa kutoa huduma kwa wagonjwa kwa kuzingatia kanuni na sheria za kazi, huku wakionyesha upendo kwa wanaowahudumia.

"Sehemu zenu za kazi mnatakiwa kusimamia misingi ya kazi na kuwajibika wakati wote mnapotoa huduma za kiafya kwa wagonjwa na jamii," alisema.

Aliwataka wataalamu na wadau wa afya kuendelea kutoa elimu ya magonjwa kwenye maeneo mbalimbali ili waweze kuimarisha afya za watu.

Alisema kuwa uuguzi ni muhimili kwenye utoaji wa afya, pia ni wito katika kutekeleza shughuli za huduma za kiafya kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Katika risala yao rais wa Chama cha Wauguzi Tanzania, Alexander Baluhya, aliomba serikali kutoa nafasi za ajira ili kuondoa upungufu uliopo wa wauguzi.

Alisema kumekuwa na upungufu wa wauguzi katika sekta ya afya hasa kwa maofisa uuguzi ambao wamekuwa wakiajiriwa kwa uchache ukilinganisha na mahitaji halisi yanahitajika maeneo mbalimbali ya utoaji huduma za afya.

## Mamlaka ya maji yatakiwa kubadilika utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi, amesema imefika wakati kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kubadilika katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana katika mkutano uliowashirikisha wadau mbalimbali katika matumizi ya maji na kuangalia gharama halisi kwa Unguja na Pemba.

Alisema ZAWA imeonekana ipo nyuma katika mambo mbalimbali hasa katika ukusanyaji wa mapato.

Kadhalika, alisema changamoto ya uzalishaji wa maji na kuwapo kwa upungufu mkubwa wa nishati hiyo kwenda kwa wananchi na anaamini kupitia mjadala huo utawaongoza kwenda mbele na kuhakikisha maji ya kutosha yanapatikana kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Aidha, Kilangi alisema wanataka kuiona ZAWA inakuwa na mabadiliko makubwa.

"Hivi sasa tupo nyuma sana, upatikanaji wa maji ni mdogo na uzalishaji wake ni mdogo na mahitaji ya wananchi ni makubwa sana, tuna upungufu wa maji zaidi ya lita 18,000,000 kwa mwaka," alisema.

Alisema kupitia mkutano huo watajipanga ili kuwafikia wananchi wote wa Zanzibar kwa kufanya jitihada ili kuhakikisha kila mwananchi anayetumia maji anafungiwa.

Akizungumzia upotevu wa maji, alisema mengi yanapotea mitaani na uvujaji ni mkubwa kwa karibu asilimia 60 yanayozalishwa yanapotea barabarani na kuwaomba wananchi kushirikiana pamoja wanapoona bomba limepasuka kutoa taarifa mapema ili hatua za haraka zichukuliwe.

Mkurugenzi wa Biashara na huduma kwa mteja kutoka ZAWA, Kazija Mussa Msheba, alisema mkutano huo utaisadia kuona mamlaka hiyo inakwenda mbele na kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Akizungumzia changamoto hizo, alisema ni pamoja na kuwapo kwa watu wengi wanaotumia maji kinyume na sheria na jumla ya wateja 34,000 katika Mkoa wa Mjini Magharibi wanatumia kinyume na sheria.

Alisema katika mwaka huu wa fedha ZAWA imepanga kufunga mita 6,000 ili kuongeza idadi kubwa ya wateja wenye mita na mwaka 2025 asilimia 60 au zaidi ya wateja watakuwa wameshafungiwa mita.

# Watanzania waoneshwa fursa soko la korosho Marekani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Bodi ya Korosho Tanzania, Evance Alfred, amewataka Watanzania kutumia fursa za masoko zinazopatikana kimataifa kwa ajili ya kuongeza kipato.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa usafirishaji wa kontena la kwanza la korosho kwenda nchini Marekani hafla ambayo imefanyika Amani Mjini Zanzibar.

Alisema fursa za kimasoko zipo nyingi kinachohitajika kwa wakulima kuwa na mipango bora itakayowawezesha kuyafikia masoko hayo.

Alisema hatua hiyo imekuja baada ya kampuni ya Ward Holdings Tanzania, kufanikisha kupata soko la korosho nchini Marekani ambako ndiko kwenye walaji wakuu.

Alisema soko la korosho nchini Marekani linahitaji zaidi ya tani 200,000, lakini viwanda vya Tanzania vinauwezo wa kubangua (kuchakata) tani 60,000.

"Viwanda tulivyonavyo Tanzania vya uchakataji wa korosho vinauwezo wa kubangua tani 60,000 lakini kwa mwaka jana vilibangua tani 14,000 pekee," alisema. Aidha, alisema mahitaji ya soko la korosho ulimwenguni ni kubwa kinachohitajika ni kuongeza viwanda vya ubanguaji na kasi ya uzalishaji wa zao hilo kwenye ubora wa kimataifa.

Alitaka kampuni ya Ward Holding ambayo ina kiwanda cha kuchakata korosho na kusafirisha kontena nchini Marekani kutokumbatia fursa hiyo peke yake badala yake kuangalia namna ya kuwasaidia wengine ambao hawana masoko.

Alisema changamoto iliyoko wengi hawana masoko ya uhakika wa karosho zilizobanguliwa ambayo yameshikwa na nchi za Vietnam na India.

Naye Rais wa Kampuni ya Ward Holding, Godfrey Simbeye alisema tukio la usafirishaji wa kontena la korosho ni mabadiliko makubwa ya kiuchumi ya viwanda vya zao hilo tangu Uhuru wa Tanzania mwaka 1961.

Alisema ili kushughulikia fursa katika kuendeleza mnyororo wa usambazaji utakaokidhi mahitaji ya soko la kimataifa, taasisi yake imegusa hisia za wajasiriamali ambao miongoni mwao ni wasindikaji wa korosho.

Kwa upande wake, Ofisa Mkuu wa uendeshaji wa taasisi hiyo, Scott Karren, alisema taasisi hiyo imefanikiwa kushirikiana na wanunuzi wa korosho kimataifa ambao watanunua korosho zote zilizosindikwa na kuthibitishwa kuingia katika soko la Marekani.

Korosho hizo zilizosafirishwa nchini Marekani zimelimwa Tanzania mkoani Mtwara na kuchakatwa Zanzibar.




Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza katika uzinduzi wa utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi Tanzania wa mwaka 2022-2023, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman aeleza umuhimu matokeo utafiti wa Ukimwi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi Tanzania ni muhimu na utawezesha serikali na wadau tofauti kupata hali halisi ya mwenendo wa maradhi hayo na kusaidia kuweka mikakati ya kwenda sambamba na uhalisia katika kupambana na tatizo hilo.

Aliyasema hayo jana, Mtoji Mjini Unguja, alipozungumza katika uzinduzi wa utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi nchini utakaofanyika Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema kupatikana kwa takwimu sahihi ni silaha muhimu katika kupanga na kuandaa mikakati ya kupambana na maradhi hayo kwa kuwa itasaidia kufahamika mwenendo wa tatizo hilo kwa ukamilifu kote nchini.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa Zanzibar ni vyema utafiti huo kwenda sambamba na utafiti wa viashiria vya maambukizo ya Virusi vya Ukimwi kwa kuhusisha makundi maalum ambayo yanaaminiwa kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo ikilinganishwa na jamii ya kawaida.

Alisema kwamba utafiti huo utahusisha kaya zipatazo 20,000 kwa Tanzania Bara na Zanzibar na kuwataka wananchi kuondoa hofu juu ya suala hilo na kuwataka kuona kwamba kaya zote zina fursa sawa ya kushiriki kwenye utafiti huo. Makamu huyo alisema kwamba kwa ujumla inatarajiwa kwamba utafiti huo utahusisha watu wapatao 40,000 kushiriki kwa utafiti wa mwaka 2022/2023 na kwamba ni matumaini ya serikali kwamba kaya zilizochaguliwa na watu watakaohusika watatoa ushirikiano wa kutosha katika kufanikisha suala hilo muhimu na kwamba taarifa zitakazopatikana zitaendelea kuwa siri na zitatumika kitakwimu pekee.


Alisema kwamba Tanzania ina mikakati kadhaa ya kupambana na tatizo hilo kwa kuwa ni muhimu pia katika kusaidia nchi kupiga hatua kiuchumi kuwa kuwapo jitihada na mikakati imara ili wananchi waepukane na maradhi ikiwamo janga la Ukimwi.

Othman alishukuru Serikali ya Marekani kupitia kituo chake cha kudhibiti na kuzuia magonjwa kwa kuendelea kuisaidia nchi kitaalamu na kifedha kufanya utafiti huo muhimu katika kupambana na maradhi ya Ukimwi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Dk. Ahmed Khatib, alisema Zanzibar kuna mikakati mbalimbali ambayo imesaidia katika kupambana na kudhibiti janga hilo toka ilipobainika mgonjwa wa kwanza mwaka 1986 Zanzibar.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Salim Kassim Ali, alisema utafiti huo utawahusisha watu kuanzia umri wa miaka 15 na kuendelea na kwamba takwimu zitakazopatikana zitasaidia katika kubuni sera mpya na kupanga mikakati zaidi ya kupambana na janga hilo.

Utafiti huo unasimamiwa kwa pamoja kati ya Tume ya Ukimwi Zanzibar na Tanzania Bara, Ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na mashirika ya kimataifa ikiwamo Marekani, Shirika la Afya Duniani (WHO) na mengineyo.



# Machinjio ya mifugo yatafutiwa mwekezaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Shinyanga mkoani Shinyanga inatarajia kubinafsisha machinjio ya Ndembezi kwa mwekezaji ili kukuza ufanisi wa kuchinja mifugo 1,500 kwa siku badala ya mifugo 75 kwa sasa.

Akizungumza wakati kamati ya ukusanyaji wa mapato ya Manispaa ilipotembelea mradi huo, Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema malengo ya machinjio hiyo ni kuchinja mifugo mingi itakayosafirishwa nje ya nchi na kuongeza pato la taifa.

"Hadi sasa naona inakuwa tofauti na malengo yetu katika mradi huu, sasa mkakati wetu ni kuanza kutafuta na kuleta wawekezaji ili kunusuru mradi huu ambao ulitakiwa kuwa na machinjio ya ng'ombe 500 na mbuzi 1,000 kwa siku, lakini tunachinja ng'ombe 38 na mbuzi 37 tu na kushindwa kumudu soko la nje," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa kamati hiyo ya ukusanyaji mapato wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Dk. Kulwa Meshack, aliwataka wawekezaji kuchangamkia fursa hiyo ya kuwekeza katika machinjio hayo.

Dk. Kulwa alisema kuwa nchi ya Oman katika soko lake la nyama kwa mwaka wanahitaji tani 700,000, lakini wanapata tani 500,000 pekee.

Aidha, aliwataka wawekezaji wasilale wachukue machinjio hayo na kuyatumia vyema kwa kuwa soko la nyama ni kubwa katika nchi mbalimbali.

Machinjio hayo ya kisasa ujenzi wake ulianza mwaka 2012, na kuzinduliwa rasmi mwaka jana na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasnita Mboneko na yamegharimu Sh. bilioni 5.2.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kushoto), akizungumza na madereva wa bodaboda wilayani Bukoba, mkoani Kagera jana, wakati akizindua kampeni ya elimu ya ebola kwa kutumia madereva hao na magari maalum ya matangazo yatakayosambazwa katika halmashauri tano zilizo jirani na mipaka ya Uganda yenye wagonjwa wa ebola. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Waandishi wanolewa kujikinga ugonjwa wa ebola

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WIZARA ya Afya imetoa mafunzo kwa baadhi ya waandishi wa habari mkoani Kagera kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa wa ebola wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao.

Mafunzo hayo yaliyotolewa jana mjini hapo kwa kutambua kundi hilo asilimia kubwa linakutana na watu mbalimbali kila siku. Akizungumza katika mafunzo hayo, Ofisa Habari wa Wizara ya Afya, Said Makola, alisema ugonjwa huo bado haujaingia nchini, lakini ni lazima hatua za kujikinga zinazotolewa na wataalamu zifuatwe na jamii wakiwamo waandishi wa habari. "Huu ugonjwa umeonekana wilayani Mubende nchini Uganda ambako ni jirani na mkoa huu wa Kagera, wananchi wana mwingiliano wa mipaka kupitia Mtukula kuingia na kutoka na shughuli zinafanyika za kibiashara tuchukue tahadhari sana," alisema Makola.

Makola alisema waaandishi wa habari wanapokuwa katika kazi hukutana na makundi ya aina tofauti ambayo huwezi kutambua yametokea mazingira yapi na tahadhari lazima zichukuliwe.

Alisema ni vyema kuchukua tahadhari ya kunawa mikono kila wakati, kuepuka kushikana mikono, kukumbatiana kwa kuwa mgonjwa akipatwa na maambukizi ana asilimia 25 hadi 90 ya kifo.

Alisema dalili za ugonjwa huo ni kutoka damu sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha kifo na mwaka 1976 mlipuko huo ulitokea karibu na mto mmoja nchini Zaire.

Dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kuanzia siku mbili hadi 21 tangu mgonjwa anapopata maambukizi ya ugonjwa wa ebola.

## Malima ataka tahadhari zichukuliwe majanga

**Na Pelusy Yohana,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amewataka wakazi wa mkoa huo kuchukua tahadhari zote ili kujikinga na ugonjwa hatari wa ebola.

Malima alitoa tahadhari hiyo jana jijini hapo katika kikao cha wataalam wa afya kutoka Wizara ya Afya, mkoa na wakuu wa taasisi za umma.

Wengine waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Thomas Rutachonzibwa, wakuu wa wilaya, viongozi wa dini pamoja na viongozi wa machinga mkoani humo.

Malima alisema ugonjwa huo haujaingia nchini, lakini lazima zichukuliwe tahadhari za kiafya ili kujikinga na janga hilo.

Aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuwahimiza wananchi kuchukua tahadhari ili kuepukana na ugonjwa huo ambao umeripotiwa nchini Uganda.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Thomas Rutachonzibwa, aliwaomba wananchi wanaposikia homa, maumivu ya misuli, kutapika na kuona vipele, kuharisha na kutokwa na damu wafike kituo chochote cha afya ili kuchunguzwa.

Aidha, alisema ili kuepukana na ugonjwa huo, wananchi wanatakiwa kutogusa vitu kama damu, matapishi, kamasi, mate, machozi, kinyesi na majimaji mengine yanayotoka mwilini mwa mtu mwenye ugonjwa wa ebola.

Aliwaomba wananchi kuweka vyombo vya kunawia mikono katika sehemu mbalimbali kwenye mikusanyiko ya watu ili kukabiliana na ugonjwa huo.

"Ikumbukwe kuwa ugonjwa wa ebola ni hatari, huu ni miongoni mwa magonjwa ya milipuko yajulikanayo kama homa za virusi vinavyosababisha kutoka damu mwilini," alisema.

**Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Thomas Rutachonzibwa, aliwaomba wananchi wanaposikia homa, maumivu ya misuli, kutapika na kuona vipele, kuharisha na kutokwa na damu wafike kituo chochote cha afya ili kuchunguzwa.**

# Juhudi za Shirika la Posta Tanzania katika kuendeleza huduma za posta nchini

*NA Mwandishi wetu*

Huduma za posta ni miongoni mwa huduma kongwe katika historia ya dunia ambapo inaelezwa kuwa zilianza kutumika zaidi ya karne moja iliyopita.

Tangu kipindi hicho huduma za posta zimekuwa zikitumika katika kurahisisha mawasiliano, ufikishaji wa taarifa, vifurushi nk katika maeneo mbalimbali duniani.

Pamoja na kuwepo kwa maendeleo makubwa ya teknolojia ambayo yamefanya dunia sasa kuwa kama kijiji huduma za posta bado zinaendelea kuwa muhimu kila siku.

Kwa kutambua umuhimu wa posta katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kongamano la Umoja wa Posta Duniani (UPU) lililofanyika jijini Tokyo, Japan liliamua kuwa Oktoba 9 ya kila mwaka iwe siku ya posta duniani ikiwa ni tarehe ya kuanzishwa kwa umoja huo.

Siku hii ilianza kuadhimishwa mwaka 1969 na tangu kipindi hicho nchi zote duniani zinaungana kusherehekea siku hiyo kwa lengo la kukumbushana umuhimu wa huduma za posta katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Tanzania kupitia Shirika la Posta ni mwanachama wa UPU ambapo kama zilivyo nchi nyingine inashirika maadhimisho ya siku hii kwa kufanya shughuli mbalimbali kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa huduma za posta.

Katika kuelekea maadhimisho ya siku ya posta mwaka huu, ambayo kwa Tanzania yanafanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) Oktoba 8 na 9 Shirika la Posta Tanzania limeaandaa mashindano ya uandishi wa barua, makala, insha na ubunifu wa graphic kwa mwaka 2022. Shindano hilo limehusisha makundi yafuatayo;

**Barua**

Uandishi wa barua kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wenye umri usiozidi miaka 18. Kwenye kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kuandika barua akimuelimisha rafaiki yake anayeishi mkoa mwengine nchini umuhimu wa Anwani za Makazi kwa huduma za posta katika ujenzi wa uchumi wa kidijitali.

Washindi kwenye kipengele hiki walikuwa ni; Josephine Mlewa kutoka Shule ya Sekondari ya wasichana Msalato, Dodoma, Maurine Lyakurwa kutoka Shule ya Sekondari ya wasichana Anwarite iliyopo Moshi Kilimanjaro na Warida Mohamed kutoka Shule ya Sekondari Kashai mkoani Kagera.

**Insha**

Uandishi wa insha kwa makundi mbalimbali wakiwemo wachumi, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na wafanyabiashara. Kwenye kipengele hiki mshiriki alitakiwa kuandika insha yenye mada ya 'Sensa ya watu na makazi Tanzania itakavyochangia ukuaji wa uchumi wa nchi'.

Washindi katika kipengele hiki walikuwa ni; Oscar Senye kutoka Shule ya Sekondari Mawenzi mkoani Kilimanjaro, Dickson Haji kutoka NMCCE Incubation Centre, Mang'ula Morogoro na Lazaro Cosmas kutoka Geita.

**Makala**

Uandishi wa makala kwa wanahabari. Kwenye kipengele hiki mwanahabari alitakiwa kuandika makala inayozungumzia mchango wa uhuru wa habari uliopo kwenye Serikali ya awamu ya sita katika ujenzi wa Tanzania ya kidijitali.

Washindi katika kipengele hiki walikuwa ni; Jacqueline Liana kutoka vyombo vya habari vya Uhuru na Mzalendo jijini Dar es Salaam, Albuni Mwedadi kutoka Mlimani Redio ya jijini Dar es Salaam na Samwel Ndoni kutoka Highlands FM radio ya mkoani Mbeya.

**Graphics**

Kipengele cha ubunifu wa graphics bora kilikuwa kinamtaka mshiriki kubuni graphic ambayo itaelezea mada isemayo 'huduma za posta zitakavyorahisishwa kupitia miundombinu ya Anwani za Makazi'.

Mshindi katika kipengele hiki alikuwa Mgasa Robert kutoka Buni-Hub COSTECH jijini Dar es Salaam.

**Wabunifu wa TEHAMA**

Kipengele cha wabunifu bora katika matumizi ya Teknolojia ya Habarai na Mawasiliano (TEHAMA) kilikuwa na mada inayosema 'sekta ya habari na mawasiliano katika ujenzi wa Tanzania ya kidijitali'.

Washindi kwenye kipengele hiki walikuwa ni; Astarick Mcharo kutoka Dodoma, Walter Adrew kutoka Mwanza na Debora Mshauri kutoka Mara.

Kwenye kila kipengele mshindi wa kwanza amezawadiwa Sh 1.5 milioni, wa pili Sh1 milioni na wa tatu 700,000. Washindi wote wamekabidhiwa zawadi zao katika hafla ya kilele cha maadhimisho ya siku ya posta duniani.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

## WASHINDI WA SHINDANO

Shirika la Posta Tanzania linapenda kuutangazia umma na wananchi kwa ujumla matokeo ya washindi wa mashindano ya uandishi wa barua, insha, makala,wabunifu bora wa vibonzo na mifumo ya Tehama yaliohusisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wanamichezo, wanahabari, wabunifu wa vibonzo na Tehama kwa mwaka 2022.

Matokeo hayo yamehusisha mshindi wa kwanza hadi wa tatu kama ifuatavyo:

A) WASHINDI WA SHINDANO LA KITAIFA LA UANDISHI WA BARUA.

| NAFASI YA MSHINDI. | JINA LA MSHIRIKI | JINSIA | UMRI | SHULE/MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Josephine Charles Mlewa | Kike | 17 | Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato S. L. P. 933, Dodoma |
| 2. | Maurine Felichismi Lyakurwa | Kike | 14 | Shule ya Sekondari ya Wasichana Anwarite S. L. P. 120 Moshi - Kilimanjaro |
| 3. | Warida Ally Mohamed | Kike | 14 | Shule ya Sekondari Kashai S. L. P. 1873 Kagera |

B) WASHINDI WA UANDISHI WA INSHA

| NAFASI YA MSHINDI. | JINA LA MSHIRIKI | JINSIA | MAHALI ANAKOTOKEA |
|---|---|---|---|
| 1 | Oscar Vicent. Senya | Kiume | Mawenzi Sekondari S.L.P 478 Kilimanjaro |
| 2 | Dickson Gelas Haji | Kiume | NMCCE Incubation Centre Mang'ula Morogoro S.L.P. 98 Morogoro |
| 3 | Lazaro Daniel Cosmas | Kiume | S.L.P. 354 Geita |

C) WASHINDI WA UANDISHI WA MAKALA.

| NAFASI YA MSHINDI. | JINA LA MSHINDI | JINSIA | MAHALI ANAKOTOKEA |
|---|---|---|---|
| 1 | Jacqueline Jonathani. Liana | Kike | Uhuru na Mzalendo Dar es Salaam |
| 2 | Albuni Izadini Mwedadi | Kiume | Mlimani Redio S.L.P 4067 Dar es Salaam |
| 3 | Samwel Ndoni | Kiume | Highlands FM Radio S.L.P 1440, Mbeya |

D) MSHINDI WA UBUNIFU WA MIFUMO

| NAFASI YA MSHINDI. | JINA LA MSHINDI | JINSIA | MAHALI ANAKOTOKEA |
|---|---|---|---|
| **1.** | **Mgasa Robert** | **Kiume** | **Buni - Hub COSTECH Dar es Salaam** |

E) WASHINDI WA UBUNIFU WA VIDEO INAYOTUMIA VIBONZO

| NAFASI YA MSHINDI. | JINA LA MSHINDI | JINSIA | MAHALI ANAKO TOKEA |
|---|---|---|---|
| 1 | Astarick Mcharo | Kiume | Dodoma |
| 2 | Walter Andrew | Kiume | Mwanza |
| 3 | Debora Mashauri | Kike | Mara |

Washindi wote watapatiwa zawadi na vyeti vya ushiriki, mshindi wa kwanza kutoka katika kila kundi atapata fursa ya kupatiwa zawadi na Mgeni Rasmi Siku ya Kilele cha shamrashamra za Maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani tarehe 9 Oktoba, 2022 yatakayofanyika Jiji Dar es Salaam katika ukumbi wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

Washindi wote wa mashindano hayo wataalikwa kuhudhuria kilele cha maadhimisho ya siku ya Posta Duniani,Shirika linawapongeza washindi na wote walioshiriki katika mashindano hayo na kuwaomba waendelee kushiriki mashindano mengine mwaka ujao.

POSTA! KWA KILA MTU.

Imetolewa na.
**Idara ya Masoko**
**Shirika la Posta Tanzania**
**Jengo la Posta, Mtaa wa Ghana,**
**S. L.P. 9551, 11300 Dar-Es-Salaam**
**Simu: 0738 070 702**
**Tovuti: www.posta.co.tz**
**Baruapepe: marketing.hq@posta.co.tz**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na 59/ 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALUM LILA OMARY WA KILOSA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAMISI ABDALLAH**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi wa 10 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Imetolewa leo tarehe 2 mwezi 9 mwaka 2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GLORY STEVEN NYANDA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index **No. S3861- 0037** kilichotolewa na Baraza la Mitihani Taifa kupitia **ANDERLEK RIDGES SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakayekiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi **MAJ/RB/1548/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 11/2022**

**Jina la Mdai..................SALOME DAMIAN MCHIWA**

**Jina la Mdaiwa............. KELVIN LYIMO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA... KELVIN LYIMO**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA GARI LENYE THAMANI YA SH 8,000,000/=**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii Tarehe 18/10/2022 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

HAKIMU
38

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA SONGEA**
**ILIYOPO SONGEA**

**RUFAA YA MADAI NA 25 YA MWAKA 2022**

**LEODGAR SANGANA .......................MWOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**JULIUS ULAYA..................................MJIBU RUFAA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA:-**
**JULIUS ULAYA**

**POPOTE ULIPO**

Hii ni kukutaarifu kwamba rufaa ya madai tajwa hapo juu imepangwa kusikilizwa tarehe 19 mwezi Oktoba mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh. A.C.Jembe Hakimu mkazi wa wilaya ya Songea. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anaeruhusiwa kisheria. Endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hilo la rufaa litasikilizwa bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 05 mwezi Oktoba mwaka 2022

HAKIMU MKAZI WA WILAYA
YA SONGEA

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 186 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU KARIMABANU SULEMAN BADRUDIN SHARIFF**

**HUSSEIN OMAR CHAKI..........................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi wa 11, 2022.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 16 mwezi wa 09, 2022

NAIBU MSAJILI

**NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**M/MWANZO ILEMELA- SHAURI LA MIRATHI Na. 151/2018**
**MADUA RAMADHANI BARUTI __________MDAI**
**DHIDI YA**
**MOSHI RAMADHANI BARUTI ___________MDAIWA**

**M/MWANZO NANSIO - SHAURI LA MADAI Na. 08/2021**
**DEONATUS FIKIRI BEGA ______________MDAI**
**DHIDI YA**
**SADOCK ZAKAYO NTILUBETA ________MDAIWA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA **MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, MAHAKAMA YA MWANZO NANSIO** TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA 1, SHAMBA LA MICHUNGWA NA KIWANJA NUSU EKA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ZILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA 1 | MTAA WA NYAMANORO ILEMELA - MWANZA | TAREHE 17/10/2022 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | SHAMBA LA MICHUNGWA | MTAA WA BUHIMU UKEREWE - MWANZA | TAREHE 21/11/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | KIWANJA NUSU EKA | MTAA WA BUHIMU UKEREWE - MWANZA | TAREHE 21/11/2022 SAA 04 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**
1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI INAYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 872 OF 2022**

**In the matter of the Estate of the late ELINAMI MONYO SIFUEL**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by**
**JANEDINAH EDWARD KIWIA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above -named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate( or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of November 2022
Dated at DAR ES SALAAM this 29 day of September 2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Tunza Yamungu Idd**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T.258 BGP Toyota Ipsum** Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Tunza Yamungu Idd kwa simu namba **0710494484**, Rbnamba **SHI/SHI/RB/394629/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Seif Hussein Ramadhani**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T.952 AUC** Mitsubishi Rosa Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Seif Hussein Ramadhani kwa simu namba **0754-657775**, Rbnamba **SHI/SHI/RB/395653/2022**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



## H BABA: SIWEZI KUZEEKA

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa bongofleva, Hamis Ramadhani maarufu kama 'H-Baba' amesema kamwe hawezi kuzeeka kwa sababu hanywi pombe wala havuti sigara.

H-Baba alisema yeye ni mtu ambaye anajali sana afya yake na kuzeeka haraka kwake sio jambo rahisi.

Akizungumza na vyombo vya habari vya mitandaoni, H-Baba alisema, yeye ni msanii wa siku nyingi ana watoto wengi, lakini hawezi kuzeeka kwani hatumii vilevi.

"Situmii pombe, sivuti sigara wala bangi…siwezi kuzeeka nitabaki hivi hivi," alisema H Baba.

Aliongeza: "Mimi siwezi kuzeeka leo wala kesho, maana najua namna ya kujitunza tofauti na wasanii wengine."

## P DIDDY AMUUNGA MKONO KANYE WEST



**LOS ANGELES, Marekani**

RAPA maarufu, P Diddy mwenye umri wa miaka 52, ametoa maoni yake kuhusu rapa mwenzake Kanye West kuvaa tisheti zilizoandikwa "White Lives Matter" wakati wa onyesho lake la wiki ya mitindo lililofanyika jijini Paris nchini Ufaransa.

Katika mahojiano mapya kwenye kipindi cha "The Breakfast Club, P Diddy amesema Kanye ni mtu wake wa karibu na hivyo anamuunga mkono kwa kila jambo.

"Kanye ni kijana wangu," alisema P Diddy.

"Na mara nyingi, anachomaanisha ni kama, kueleweka vibaya, unajua ninachosema?, ni ngumu sana kuelewa anachomaanisha Kanye West na mara nyingi watu humwelewa vibaya.

"Ninaelewa maisha ya wazungu ni muhimu, lakini sivyo," alisema Diddy.

"Maisha ya Weusi (Black Lives Matter) ilikuwa kauli mbiu yetu. Hiyo haikuwa kauli mbiu yetu ya kwenda kushiriki na mtu mwingine yeyote … Kwa sababu sasa hivi, sisi ndio tunakufa, tumefungwa na tumeachwa katika umaskini."



## MLIMBWENDE WA KENYA AFUNGUKA MAKUBWA

**NAIROBI, Kenya**

MREMBO maarufu wa nchini Kenya, Vera Sidika, ameeleza amelazimika kufanyiwa upasuaji kwa ajili ya kujinusuru afya yake baada ya awali kufanya upasuaji wa kutengeneza shepu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Vera ameweka picha mpya inayomwonyesha akiwa mwembamba tofauti na mwanzo akionekana kuwa na makalio makubwa.

"Hii imekuwa awamu ngumu zaidi maishani mwangu, kwa sababu ya hatari na matatizo ya kiafya , ilinibidi kufanyiwa upasuaji.

"Bado haiaminiki sana lakini nimekubali na nimejifunza kujipenda bila kujali. Wanawake wenzangu jifunzeni kujipenda na usiruhusu shinikizo la rika likuharakishe katika mambo yatakayokuharibia siku zijazo.

"Nimebahatika kuwa hai, Mungu ananipenda sana. Kusema kweli imekuwa ngumu sana, hata sikusherehekea siku yangu ya kuzaliwa mwaka huu, lakini hapa tumefikia. Heri ya kuzaliwa kwangu.

"Mimi ni mpya. Nimekuja kuthamini maisha na kamwe sichukulii mambo ya kawaida. Asante kwa familia yangu, haswa mume wangu kwa kuwa karibu nami.

"Kwa mashabiki wangu: Mimi bado ni mrembo yule yule Vera Sidika na hilo halijabadilika. Nashukuru kwa upendo na sapoti yenu kupitia safari hii pamoja nami.

"Nitakuwa nikiweka video zangu za safari ya upasuaji hapa, kwa wale ambao wamekuwa wakifikiria kupata upasuaji wa kuongeza makalio au kubadilisha chochote kwenye miili yao."

# KMC FC, RUVU SHOOTING HAPATOSHI LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata pointi moja katika mchezo uliopita dhidi ya Namungo FC, KMC FC inatarajiwa kuikaribisha Ruvu Shooting katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

KMC itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka suluhu katika mchezo uliopita dhidi ya Namungo FC uliochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko mkoani Lindi.

Pia Ruvu Shooting watashuka uwanjani wakitoka kupoteza katika mchezo uliopita dhidi ya Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMC, Ahmad Ally, alisema wamejiandaa kuhakikisha wanazibakisha pointi zote tatu na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ally alisema nguvu zao zote wamezielekeza katika kupambana na wanatarajia kuwakabili Ruvu Shooting kwa mbinu tofauti na vile walivyozoeleka.

Kocha huyo alisema wanaenda kucheza mechi ngumu kwa sababu wanatambua ufundi wa Kocha Mkuu wa wapinzani wao, Boniface Mkwassa pamoja na uzoefu wake katika ligi hiyo.

"Kocha wao anajua kupanga kikosi chake, nasi tunaenda kwenye mchezo huo tukiwa tunawaheshimu wapinzani wetu na tunaingia kwa tahadhari zote ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, tuko nyumbani lakini hatutaweza kujisahau kwa sababu katika mechi lolote linaweza kutokea," alisema Ahmad.

Mwakilishi wa wachezaji wa KMC, Ismail Gambo, alisema kiujumla wamejiandaa vyema kuelekea mechi dhidi ya Ruvu Shooting na wataenda kuwakabili kwa tahadhari kubwa kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo mazuri.

"Tunafahamu Ruvu Shooting ni timu nzuri na ina walimu wenye uzoefu mkubwa, tunaenda kwa kuheshimu, tumejiandaa kisaikolojia kupambana kupata ushindi na alama tatu muhimu," alisema Gambo.

Naye Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Frank Msese, alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika kwa asilimia 90 na wachezaji wote wako tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri.

Msese alisema mechi hiyo itakuwa imetawaliwa na mbinu na ufundi mkubwa kwa sababu ya makocha wa timu hizo mbili ni waumini wa kucheza mpira hali ambayo itaifanya mechi hiyo kuwa na ushindani mkubwa.

"Tunahitaji kupata pointi tatu muhimu kwa ajili ya kujiweka katika mazingira mazuri katika msimu, ila mbinu za ndani ya uwanja ndio zitaamua mchezo wa kesho (leo)," alisema Msese.

Mshambuliaji wa Ruvu Shooting, Hija Ugando, alisema kikosi chao kiko tayari na imara kupata matokeo bora.

"Wamejiandaa vizuri, kazi kubwa imebaki kwetu wachezaji kufanya yale tuliyopewa katika uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kuwakabili Ruvu Shooting na kuhakikisha tunapata pointi tatu muhimu," alisema Ugando.



Mabondia chipukizi wa Kata ya Ngamiani Kusini wakipambana kusaka nafasi ya kushiriki katika fainali ya mashindano ya Mtaa kwa Mtaa yanayotarajiwa kufanyika Novemba 13, mwaka huu jijini Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtaa kwa Mtaa Tanga Nov. 14

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuongeza hamasa katika mchezo wa ngumi, mabondia chipukizi wanatarajiwa kupambana ili kupata wawakilishi watakaoingia katika mashindano rasmi ya kuwania mikanda mbalimbali ya kitaifa na kimataifa hapo baadaye.

Mashindano hayo ya kusaka vipaji yanaandaliwa na Kampuni ya Five Brothers na yalianza kufanyika Julai mwaka jana ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Meya wa Jiji la Tanga, Abdulrahman Shiloo na uzinduzi wa msimu wa pili ulifanyika Oktoba 4, mwaka huu kwenye Kata ya Mwanzage, Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Nassor Makau, Mkurugenzi wa Five Brothers, mashindano hayo yaliendelea tena juzi katika Kata ya Ngamiani Kusini ambapo mapambano 12 yalichezwa.

Taarifa hiyo iliongeza mashindano hayo yataendelea tena Oktoba 11, mwaka huu katika Kata ya Msambweni na siku inayofuata mabondia wa Kata ya Duga watapanda ulingono na Oktoba 13, mwaka huu itakuwa ni zamu ya chipukizi wa Kata ya Masiwani kuonyesha vipaji vyao.

"Sisi lengo letu ni kuzifikia kata zote za jiji la Tanga na hatimaye ikifika Novemba 14, mwaka huu, ndio itakuwa fainali ya Mtaa kwa Mtaa," ilisema taarifa hiyo.

Iliongeza ifikapo Novemba 15, mwaka huu, kutakuwa na mapambano yatakayohusisha mabondia wa kulipwa ambapo Allan Kamote, Juma Mustafa, Jacob Maganga, Saidi Mundi na wengine watapanda uliongoni.

"Tunaamini tutafikia malengo ya kuwapa fursa mabondia wachanga kufikia ndoto zao za kupanda ulingoni," iliongeza taarifa hiyo.

## Ihefu yatamba kuimaliza City

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata pointi ya kwanza msimu huu, Kocha Mkuu wa Ihefu SC, Juma Mwambusi, amesema safari ya kupata ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara katika timu yake imeanza rasmi.

Ihefu ilipata sare ya bao 1-1, dhidi ya Tanzania Prisons na mchezo wake uliopita na leo itashuka dimbani kuvaana na Mbeya City.

Mwambusi aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na timu yake imeendelea kuimarika, hivyo anaamini njia ya mafaniko imeshafunguka.

"Tupo vizuri kuwakabili Mbeya City, tunaomba mashabiki waendelee kutuunga mkono, tutazidi kupambana ili kujiondoa mkiani," alisema Mwambusi.

Kocha huyo aliongeza tayari ameyafanyia kazi makosa aliyoyaona katika mchezo uliopita na anampa umuhimu mkubwa mchezo huo ambao wanatarajia utakuwa na upinzani.

"Tutaingia uwanjani tukiwa na tahadhari zote ili tuzipoteze mchezo huo, tunatamani kupanda juu katika msimamo wa Ligi Kuu," Mwambusi alisema.

## Mbuni yaziwaza Simba SC, Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Mbuni FC ya jijini Arusha inayoshiriki Ligi ya Championship umesema timu yao itaendeleza ushindani itakapokutana na Transit Camp katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Mbuni FC, Leonard Gudeba, alisema timu yake inaendelea vizuri na mazoezi na wana lengo moja tu la kupata pointi tatu katika mchezo huo.

"Lengo letu ni kupata pointi tatu katika mchezo huo wa Jumamosi, kila mchezaji yuko tayari na ana utamani mchezo huo," alisema Gudeba.

Kocha huyo wa vinara wa ligi hiyo alisema hali za wachezaji kiafya ni nzuri na hana majeruhi hata mmoja katika kikosi chake.

"Mikakati yetu ni kuendelea kufanya vizuri katika kila mechi na hatimaye tupande daraja, ndoto yetu ni kushiriki Ligi Kuu katika msimu ujao," Gudeba alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ARSENAL YAMWINDA RASHFORD**

KLABU ya Arsenal inafuatilia hali ya Marcus Rashford katika klabu ya Manchester United kabla ya kutoa ofa ya kumnunua mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

**SOUTHAMPTON KUFUKUZA KOCHA**

KLABU ya Southampton iko tayari kumfuta kazi kocha wake, Ralph Hasenhuttl baada ya klabu hiyo kuanza vibaya katika Ligi Kuu England inayoendelea msimu huu. ***(Telegraph)***

**COOPER KUMRITHI RALPH**

BOSI wa Nottingham Forest, Steve Cooper ndiye anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Ralph Hasenhuttl. (Mail)

**FOREST, LEICESTER VITANI**

KLABU ya Nottingham Forest wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Leicester City kumpata Rafael Benitez kama kocha wao mpya, ikiwa wataamua kumtimua Steve Cooper. (***Football Insider***)

**STRUBER ANUKIA FOREST**

KOCHA Mkuu wa New York Red Bulls, Gerhard Struber pia anatajwa kuwindwa na Nottingham Forest ambayo haifurahishwi na mwenendo wa Ralph Hasenhuttl. ***(Sun)***

**MUSIALA ATAKIWA LIVERPOOL**

LIVEROOL itafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 19 iwapo watashindwa kumpata kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham (19). (***Mirror***)

**KEITA NA MKATABA MPYA**

KIUNGO wa kati wa Liverpool na Guinea, Naby Keita mwenye umri wa miaka 27, hatajadili mkataba mpya na Wekundu hao hadi Januari. Mkataba wake wa sasa unaisha msimu ujao wa joto. ***(Bild)***

**GRIEZMANN RASMI SOKONI**

BARCELONA wamekubali kumuuza kabisa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31 kwa Atletico Madrid kwa nusu ya bei yake ya euro milioni 40. Fowadi huyo wa Ufaransa kwa sasa yuko kwa mkopo Atletico. ***(Marca)***

**CHELSEA YAMTAKA RICE**

KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23, atakuwa analengwa zaidi na Chelsea katika dirisha la uhamisho wa mwaka 2023. ***(90min)***

**PSG YAMCHUNIA MESSI**

LIONEL Messi bado hajapokea ofa yoyote ya mkataba mpya kutoka Paris St-Germain, huku mkataba wake wa sasa ukimalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

**MARTINS ANUKIA HULL**

KOCHA wa zamani wa Olympiakos, Pedro Martins, ambaye alihusishwa na kazi ya kuifundisha Wolves, anakaribia kuteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa Hull City. ***(Talksport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AKANUSHA HAALAND KUONDOKA CITY

Asema ana furaha klabuni hapo na hakuna kipengele cha kuuzwa...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema ripoti za nchini Hispania zinazosema mkataba wa Erling Haaland una kipengele maalum cha kumwacha ajiunge na Real Madrid mwaka 2024 "si za kweli".

Akizungumza baada ya mshambuliaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 22 kuendeleza mwanzo wake mzuri hapo Manchester City kwa kufunga mabao mawili dhidi ya Copenhagen katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Guardiola alikanusha uvumi ambao Madrid wameandaa makubaliano ya kipekee ya kumsajili.

"Sio kweli," alisema Guardiola "Hana kipengele cha kutolewa kwa Real Madrid, au timu nyingine yoyote.

"Je, ninakerwa na uvumi? Hapana. Uvumi ni kawaida na watu wanazungumza, huwezi kudhibiti, kwa hiyo kila wakati tunapaswa kuwa na wasiwasi juu ya kile tunachoweza kudhibiti.

"Jambo muhimu ni amezoea vizuri sana hapa City. Nina hisia ana furaha sana hapa, na hili ndilo jambo muhimu zaidi."

Haishangazi kuona Haaland akihusishwa na wababe hao wa Hispania kutokana na kiwango chake cha ajabu kwa City, tayari amefunga mabao 19 katika mechi zake 12 za kwanza tangu ajiunge kutoka Borussia Dortmund msimu wa joto.

Haaland alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye ushindi wa mabao 5-0 wa Jumatano dhidi ya timu hiyo ya Denmark na mchezaji mwenzake, Jack Grealish alishangazwa na kiwango chake.

"Sijawahi kushuhudia kiwango kama hiki maishani mwangu, kwa bao la kwanza na la pili nilikuwa nacheka tu, yeye yuko kila wakati," alisema Grealish akiiambia BT Sport.

"Mlinzi wao aliniambia kitu nilipokuwa nikirudi. Alisema 'yeye si binadamu!' Nikasema 'unaniambia?' Natumaini anaweza kuendelea na kiwango hiki."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,037,3
MECHI KALI
KMC
VERSUS
RUVU SHOOTING
1 | 2.17
X | 2.86
2 | 3.44
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA: TUTAWAZAWADIA WACHEZAJI WETU MUHIMU



**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema klabu hiyo ina "mpango wa siku zijazo" na majadiliano juu ya mikataba mipya kwa wachezaji muhimu.

Beki, William Saliba, winga Bukayo Saka na mshambuliaji, Gabriel Martinelli wote wana umri wa miaka 21 na wamebakiza miaka miwili kwenye mikataba yao ya sasa.

Wamecheza mara kwa mara kwa Arsenal msimu huu na Arteta amesema klabu itaangalia "kuwazawadia" wachezaji muhimu.

"Lazima tujipange kwa siku zijazo na sote tunafanyia kazi hilo," amesema Arteta akinukuliwa na BBC Sport.

Arteta aliongeza: "Tutajaribu kufanya mambo kwa njia sahihi, tukiwa waadilifu na kujaribu kupanga njia bora zaidi na kuwazawadia wachezaji ambao kwa maoni yetu wana mustakabali mkubwa kwa klabu.

"Kwa sasa tuna jambo la kutangaza, tutafanya hivyo.

"Tutajaribu kuhakikisha kuwa klabu inalindwa kila wakati, klabu iko katika nafasi nzuri ya kusonga mbele na wachezaji wana furaha kuwa kwenye klabu."

# Obi aeleza alivyoitosa United

**LONDON, England**

NAHODHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Nigeria, John Mikel Obi, amesema kuchagua kujiunga na Chelsea na kuitosa Manchester United katika uhamisho uliokumbwa na utata mkubwa mwaka 2006 ulikuwa "uamuzi bora" kaika maisha yake ya soka.

Kiungo huyo aliyestaafu soka wiki iliyopita akiwa na umri wa miaka 35, alijikuta katika mzozo mkali akizihusisha United na Chelsea mwaka 2005, kabla ya kusajiliwa mwaka uliofuata.

Uamuzi wake wa kuhamia London, baada ya awali kutia saini United akitokea klabu ya Norway, Lyn Oslo, hatimaye umeonekana kuwa ni uamuzi uliokuwa na manufaa.

Obi alikua mmoja wa wachezaji wenye mafanikio zaidi katika klabu hiyo, akishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la Europa, Ubingwa wa Ligi Kuu England mara mbili, Kombe la ligi mara mbili na mataji manne ya FA katika kipindi cha miaka 11 ambacho kilimalizika alipoondoka Stamford Bridge mwaka 2017.

"Sijutii uamuzi wowote niliofanya kwa sababu nilifurahia kila kitu nilichofanikisha nikiwa Chelsea - ni uamuzi bora zaidi ambao nimewahi kufanya maishani mwangu," alisema Mikel akiiambia BBC Sport Africa.

"Nilisaini mkataba wa awali na Manchester United nilipokuwa na umri wa miaka 17. Ukiwa mtoto na unamwona Sir Alex Ferguson akiwa mbele yako ameshika mkataba, bila shaka utasukumwa kusaini."

Chelsea waliokuwa na imani kusaini kwao, walishtuka kusikia amesaini kwa wapinzani wao. Wakala wake, John Shittu alifunga safari mara moja hadi Oslo kumchukua mchezaji na kumpeleka London. Klabu yake ya Lyn ikatangaza kutoonekana kwake, ametoweka.

"Ulikuwa utoto na mara tu Chelsea iliposikia habari hizo, walikuja na kuniondoa Norway," amesema mshindi huyo wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2013.

HABARI MICHEZO

361,877/-

# TANZANIA MWENYEJI MICHUANO YA KUOGELEA KANDA YA 3 AFRIKA

**Na Saada Akida**

TANZANIA imeteuliwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya kimataifa ya kuogelea ya Kanda ya Tatu Afrika ambayo yanatarajiwa kushirikisha waogeleaji mbalimbali kutoka nchi 25.

Mashindano hayo yamepangwa kufanyika kuanzia Novemba 15 hadi 20, mwaka huu kwenye bwawa la kuogelea la klabu ya Gymkhana, ambapo hii ni mara ya pili kwa Tanzania kuwa mwenyeji kwa michuano hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Hadija Shebe, alizitaja nchi zitakazoshiriki mashindano hayo ni Kenya, Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Sudan, Rwanda, Somalia, Sudani Kusini, Uganda na wenyeji Tanzania.

Alizitaja nchi za Kanda ya Nne ambazo zinatarajia kushiriki katika mashindano hayo ni Angola, Botswana, Comoro, Lesotho, Madagascar, Malawi na Afrika Kusini pamoja na Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Zambia, Eswatini na Zimbabwe. Alisema wanatarajia kuwa na wachezaji na maofisa mbalimbali zaidi ya 300 ambapo anawaomba wadau kusaidia kudhamini mashindano hayo makubwa ya kuogelea barani Afrika.

"Tumepewa heshima kubwa kuandaa mashindano haya na Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea la Afrika, hivyo tunaomba wadau kutusaidia ili kufanikisha mashindano haya," alisema Shebe.

Naye Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Tanzania (BMT), Neema Msitha, alisema ujio wa timu zote hizo ni heshima kwa nchi na kuwaomba wadau kusaidia kudhamini michuano hiyo.

"Naipongeza TSA kwa kupewa heshima kubwa ya kuandaa mashindano haya. Ni faraja kwa nchi kwani mbali ya kuitangaza nchi, pia inatoa fursa kwa wachezaji wetu kupima viwango vyao kimataifa na vilevile kuutangaza utalii wa nchi," alisema Msitha.

Aliongeza serikali ipo pamoja na TSA katika kuhakikisha mashindano hayo yanafanikiwa pamoja na ukweli wanahitaji msaada kutoka kwa wadhamini.

Naye Meneja Msaidizi wa timu ya kuogelea ya Tanzania, Asha Gomile, alisema waogeleaji wa timu hiyo wanaendelea na maandalizi kuelekea mashindano hayo na wanatarajia kufanya vyema.

Asha maarufu kwa jina la Mama Natalia alisema wanatarajia kufanya vyema katika mashindano hayo kama ilivyokuwa mwaka 2017 ambapo walitwaa ubingwa katika mashindano yaliyofanyika hapa nchini.

"Waogeleaji wetu wapo tayari na ikumbukwe mwaka uliopita, tulimaliza katika nafasi ya pili katika mashindano yaliyofanyika Uganda. Tupo tayari kwa mapambano na tunatarajia kufanya vyema," alisema meneja huyo.



Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Neema Msitha (wa nne kulia) akiwa pamoja viongozi wa Chama cha Kuogelea Nchini (TSA), wakionyesha ishara ya mshikamano wakati wa uzinduzi wa mashindano ya Kanda ya Tatu ya Afrika yatakayofanyika nchini hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mayele, Aziz Ki

INATOKA UK. 32

hasa ukizingatia Jumamosi tunacheza mechi ya kimataifa dhidi ya Al Hilal, kila mmoja wetu amejiwekea imani ya kushinda mechi ya nyumbani na kwenda kupambana ugenini na tucheze makundi," alisema Mwamnyeto.

Beki huyo alifunga bao la ushindi dakika ya 71 na kuifanya Yanga ikae katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara nyuma ya vinara, Simba, lakini wakiwa na pointi sawa 13.

# Simba yajiandaa kushusha jembe

INATOKA UK. 32

wakati huo alikuwa akiichezea Vipers ya Uganda.

Usajili wa Manzoki katika dirisha dogo la usajili uliingia changamoto kutoka katika Vipers ambaye sasa anaichezea Dalian Professional ya China kwa mkataba wa muda mfupi.

Kuhusu Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, mwenyekiti huyo alisema walifanya uamuzi sahihi, akiongeza hata kwenye kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wakati wamewasilisha jina la kocha huyo ili kulipitisha hakukuwa na mjumbe yeyote aliyepinga.

"Tulikuwa wajumbe saba, wote tulikubali jina lilipowasilishwa, na hata tulipompigia simu na yeye (Mgunda), wala hakuchukua muda kukubali, kwa hiyo hatukumpata kwa bahati. Kwa sasa ndiyo Kaimu Kocha Mkuu, kama kuna kocha mpya atakuja, au ataendelea yeye, tuvute subira," alisema bosi huyo.

Aliongeza wanaamini Mgunda ataisaidia Simba kufikia malengo yao katika mashindano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo msimu uliopita walivuliwa ubingwa.

"Tunapambana katika kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri, lengo letu ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika mashindano yote tunayoshiriki, tunajua mashabiki wetu wanahitaji furaha, hicho ndio tunachokitarajia sisi viongozi pia," Salim aliongeza.

Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini kesho kuelekea Angola kuwafuata Primiero De Agosti katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa keshokutwa.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/10/22 | 17:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 02. 08/10/22 | 17:00 | Swansea vs Sunderland | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 08/10/22 | 17:00 | Wigan vs Cardiff | 2.35 | 3.18 | 3.08 |
| 04. 08/10/22 | 17:00 | Birmingham vs Bristol City | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 05. 08/10/22 | 19:30 | Brighton vs Tottenham | 2.90 | 3.35 | 2.37 |
| 06. 08/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 07. 08/10/22 | 22:30 | Pacos Ferreira vs Vitoria Guimaraes | 3.00 | 3.10 | 2.48 |
| 08. 09/10/22 | 14:00 | Huddersfield vs Hull City | 2.36 | 3.33 | 2.93 |
| 09. 09/10/22 | 15:00 | Valladolid vs Betis | 3.03 | 3.33 | 2.30 |
| 10. 09/10/22 | 16:00 | Salernitana vs Verona | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 11. 09/10/22 | 16:00 | Udinese vs Atalanta | 2.63 | 3.37 | 2.58 |
| 12. 09/10/22 | 16:00 | Angers vs Strasbourg | 2.44 | 3.33 | 2.78 |
| 13. 09/10/22 | 17:15 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.88 | 3.18 | 2.48 |
| 14. 09/10/22 | 18:30 | Arsenal vs Liverpool | 2.64 | 3.45 | 2.53 |
| 15. 09/10/22 | 18:30 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 3.02 | 3.41 | 2.25 |
| 16. 09/10/22 | 19:30 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 17. 09/10/22 | 20:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.61 | 3.15 | 2.71 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 07/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2647 | SHB DA Nang vs B. Binh Duong | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 13:00 | 5589 | Binh Phuoc vs Cong Anh Nhan Dan | 5.83 | 3.84 | 1.50 |
| 16:00 | 1357 | Bnei Yehuda vs Maccabi Jaffa | 2.60 | 3.00 | 2.85 |
| 16:00 | 1440 | Hapoel Acre vs Hapoel Kfar Saba | 2.89 | 2.89 | 2.64 |
| 16:00 | 2249 | Ahi Nazareth vs Hapoel Ramat Gan | 2.42 | 2.99 | 3.09 |
| 16:00 | 4837 | Kustosija vs NK Dubrava | 2.39 | 3.06 | 2.82 |
| 16:00 | 5646 | KMC vs Ruvu Shooting | 2.17 | 2.86 | 3.44 |
| 16:15 | 3386 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Ittihad Kalba | 1.60 | 3.90 | 4.58 |
| 16:30 | 4526 | Esteghlal Tehran vs Foolad Khuzestan | 2.00 | 2.73 | 4.29 |
| 17:30 | 4183 | Ural Yekaterinburg vs FK Khimki | 1.90 | 3.47 | 3.76 |
| 17:55 | 3397 | Al Fehaheel vs AL Tadamon | 2.11 | 3.45 | 3.30 |
| 18:00 | 2745 | Voluntari vs CS Mioveni | 2.11 | 3.07 | 3.57 |
| 18:30 | 2213 | Naft Masjed Soleyman FC vs Gol Gohar | 3.60 | 2.68 | 2.23 |
| 18:30 | 2839 | Abha vs Al Nasr Riyadh | 6.25 | 4.43 | 1.46 |
| 19:00 | 1439 | Jazira Abu Dhabi vs Al Sharjah SC | 3.02 | 3.51 | 2.07 |
| 19:00 | 1648 | Apoel Nicosia vs Karmiotissa | 1.26 | 5.61 | 10.02 |
| 19:00 | 4116 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Sibenik | 1.80 | 3.68 | 3.68 |
| 19:00 | 4293 | Dinamo Brest vs Dnepr Mogilev | 1.43 | 4.28 | 6.02 |
| 19:10 | 4256 | Amstetten vs SV Lafnitz | 2.11 | 3.51 | 2.92 |
| 19:30 | 1036 | Arminia Bielefeld vs Karlsruher SC | 2.77 | 3.41 | 2.35 |
| 19:30 | 5665 | Sepahan Esfahan vs Persepolis FC | 2.58 | 2.67 | 2.96 |
| 20:00 | 3481 | Adanaspor vs Bandirmaspor | 2.88 | 3.37 | 2.20 |
| 20:00 | 4734 | Lyngby vs Viborg FF | 3.08 | 3.48 | 2.16 |
| 20:15 | 4841 | Al Jahra vs AL Nasr | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 21:00 | 1165 | Groningen vs Waalwick | 2.22 | 3.36 | 3.01 |
| 21:00 | 3642 | Dordrecht vs PEC Zwolle | 5.34 | 4.55 | 1.47 |
| 21:00 | 4126 | Jong PSV vs Telstar | 2.03 | 3.55 | 3.21 |
| 21:00 | 4835 | Jong AZ Alkmaar vs NAC Breda | 2.85 | 3.49 | 2.23 |
| 21:00 | 5612 | ADO Den Haag vs FC Eindhoven | 2.39 | 3.26 | 2.77 |
| 21:00 | 5911 | Roda Kerkrade vs VVV Venlo | 1.65 | 4.04 | 4.34 |
| 21:05 | 1369 | Ujpest FC vs Kecskemeti TE | 1.78 | 3.60 | 3.84 |
| 21:15 | 1475 | FC Aarau vs FC Thun | 2.14 | 3.51 | 2.87 |
| 21:30 | 1879 | Jagiellonia vs Wisla Plock | 1.99 | 3.40 | 3.30 |
| 21:30 | 1933 | Genoa vs Cagliari | 1.90 | 3.36 | 3.91 |
| 21:30 | 2224 | Hoffenheim vs Werder Bremen | 1.92 | 3.87 | 3.32 |
| 21:30 | 4133 | Wisla Krakow vs LKS Lodz Pss | 1.83 | 3.45 | 3.79 |
| 21:45 | 1505 | Inverness vs Partick Thisle | 2.75 | 3.19 | 2.45 |
| 21:45 | 1794 | Waterford Utd vs Treaty United | 1.38 | 4.53 | 6.50 |
| 21:45 | 1895 | UCD Dublin vs Sligo Rovers | 4.07 | 3.49 | 1.76 |
| 21:45 | 2127 | Derry City vs Finn Harps | 1.24 | 5.27 | 9.75 |
| 21:45 | 3178 | Galway United vs Athlone Town | 1.16 | 6.66 | 11.76 |
| 21:45 | 3440 | Royal Antwerp vs St Truiden | 1.92 | 3.49 | 3.74 |
| 21:45 | 4509 | Dundalk FC vs St Patricks | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 21:45 | 5576 | Bohemians FC vs Drogheda Utd | 1.68 | 3.64 | 4.36 |
| 21:45 | 5891 | Cork City vs Wexford Youths | 1.41 | 4.47 | 6.02 |
| 22:00 | 1838 | Lyon vs Toulouse | 1.48 | 4.67 | 5.37 |
| 22:00 | 2923 | Sporting Gijon vs Villarreal B | 1.92 | 3.41 | 3.76 |
| 22:00 | 3594 | Osasuna vs Valencia | 2.24 | 3.20 | 3.20 |
| 22:00 | 5649 | QPR vs Reading | 1.84 | 3.46 | 4.05 |
| 22:15 | 1263 | Gil Vicente vs GD Estoril | 2.03 | 3.38 | 3.48 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Oktoba 7, 2022
Nipashe





## Guardiola akanusha Haaland kuondoka City

# Mayele, Aziz Ki waongezewa dozi

### ●●●Lengo la Nabi ni kuhakikisha mastraika wake wanatumia vyema nafasi ambazo...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inapata matokeo mazuri kwenye mechi zote mbili, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, jana aliwapa mazoezi maalumu mastraika wake ili wazitumie vyema nafasi watakazotengeneza katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal itakayochezwa kesho Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nabi alionekana akiwapa mazoezi washambuliaji wake ili kusaidia kumaliza tatizo la kupoteza nafasi ambao amelibaini katika mechi mbalimbali walizocheza.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga inaongozwa na nyota wa kigeni ambao ni Fiston Mayele, Heritier Makambo na Stephane Aziz Ki.

Yanga inaendelea na mazoezi yake katika Uwanja wa Avic Town, Kigamboni.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema katika programu yake hiyo amegawa saa moja kwa ajili ya wachezaji wake wote kufanya mazoezi ya mbinu na ufundi huku akitumia saa lingine kuwanoa washambuliaji peke yao.

Nabi alisema Jumatatu walifanya mazoezi asubuhi na jioni wakati juzi na jana walifanya mara moja kwa saa 2:30 lakini akiwa makini na washambuliaji wake kwa kuhitaji kuwaongezea mbinu za utulivu wanapokuwa jirani na lango la mpinzani.

Alisema anahitaji watumie nafasi vizuri hasa katika mchezo huo wa kimataifa ambao ni adimu kupata nafasi nyingi.

"Katika michezo ya kimataifa tunahitaji kutumia vyema nafasi tunazopata mwanzoni na kwa kufanya hivyo tutapata ushindi, ni muhimu kwetu kupata ushindi dakika za mwanzo ili kuongeza hali ya kujiamini, tutajitahidi kupata matokeo mazuri, tumejiandaa vizuri kuanzia kuwaweka sawa kisaikolojia wachezaji wetu pamoja na utimamu wao," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema hawawezi kuidharau timu yoyote inayoshiriki mashindano hayo na kuongeza umakini mkubwa unahitajika katika kikosi chake ili kufikia malengo.

Alisema pia anaendelea kusahihisha makosa ya wachezaji wake, lakini anayafanyika kazi mapungufu na ubora wa wapinzani wao.

Aliongeza amefurahi kuona morali ya nahodha wake, Bakari Mwamnyeto, ambaye alifunga bao katika ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Jumatatu iliyopita.

Alisema anaamini Mwamnyeto ataonyesha kiwango bora katika mechi dhidi ya Al Hilal na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayofuata.

Aliongeza mbali na nahodha huyo, kila mchezaji wa Yanga amejipanga kuonyesha kiwango kizuri ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika michezo iliyoko mbele yao.

"Bao alilofunga (dhidi ya Ruvu Shooting), limeongeza morali na kuongeza juhudi ya kufanya vizuri na kuisaidia timu kupata matokeo chanya katika michezo iliyoko mbele yetu, hasa kuelekea mechi ya Jumamosi tutakapowavaa Al Hilal," Nabi alisema.

Naye Mwamnyeto aliliambia gazeti hili wakati wote yuko tayari kuisaidia Yanga kupata matokeo mazuri kwa sababu hilo ndio jukumu lake kuu.

"Nimefurahi kufunga bao, imeniongezea hali ya kujituma zaidi na kupambana ili kusaidia timu yangu kufikia malengo tulijiwekea

INAENDELEA UK. 31



Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola (kulia), akifuatilia mazoezi ya wachezaji wa timu hiyo inayojiandaa kuwafuata Primeiro De Agosto ya Angola katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa keshokutwa mjini Luanda. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba yajiandaa kushusha jembe

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema itaziba pengo la mchezaji wake aliyevunja mkataba hivi karibuni, Dejan Georgijevic kwa kusajili straika mpya wa kiwango cha juu wakati wa dirisha dogo la usajili litakaposajiliwa, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema mpango mkakati umeshaanza ili kuhakikisha nafasi hiyo inazibwa na mchezaji wa daraja la juu kwa kushirikiana na benchi la ufundi.

Salim alisema kwa sasa wapo katika mazungumzo na wawakilishi wa Dejan na yatakapokamilika wataweka wazi, lakini kwa sasa wataendelea kuwaamini wachezaji wa nafasi hiyo waliokuwa nao.

"Jambo muhimu ni kuona nafasi hiyo inazibwa na straika mwenye uwezo mkubwa wa kufumania nyavu, lakini mchakato huu tunashirikiana na benchi la ufundi, sisi wenyewe umuhimu tunauona, tunalisikiliza benchi la ufundi linahitaji kitu gani, lakini kwetu sisi mpango mkakati umeshaanza mara moja kuhakikisha nafasi hiyo inazibwa na siku zote, Simba huwa hatufanyi makosa kwenye jambo hilo ni suala la wakati tu. Sina shaka Wanasimba watafurahi na kile ambacho wanakitarajia, huenda ukawa ndiyo wakati wake umefika," alisema bosi huyo.

Ingawa bosi huyo hakumtaja mchezaji ambaye watamsajili, lakini zipo habari zinasema tayari klabu hiyo ilishampa mkataba wa awali Cesar Mandoki ambaye

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >